




SURA YA KWANZA

NAONANA NA CHIFU

Ndege ilitua kwenye uwanja wa ndege wa mjini Dar es Salaam kiasi cha saa moja na nusu asubuhi. Nilipita harakaharaka katika sehemu za afya, uhamiaji na ushuru wa forodha, kisha nikachukua tekisi iliyonipeleka moja kwa moja katika ofisi yangu ya 'Afrika International Agencies', iliyoko mtaa wa Independence karibu na ofisi kuu za shirika la Bima la Taifa.

"Hallo bosi, umerudi!", Rose mfanyakazi wetu sehemu ya mapokezi alisema.

"Naam nimepata ujumbe wa teleksi kutoka kwa Marcelina kuwa mama anakufa".

"Na kweli nenda ofisi kwako mwandishi wako mahususi alikuwa na wasi wasi maana huko juu wanakuulizia kila baada ya dakika kumi. Ama kweli huko juu kuna kitu kikubwa kinawawasha".

Nilielekea ofisini kwangu, nilipofika nikafungua mlango wa mwandishi wangu mahsusi, Linda.

Oh, Mungu wangu, afadhali umefika, kidogo nipate wazimu maana huko juu hawanipi nafasi hata ya kupumua. Naulizwa kila wakati kwanini hujafika, utafikiri mimi ndiye nakufuga".

"Poa sasa nimefika mwenyewe. Vipi shughuli hapa?".

"Mambo shwali, isipokuwa toka juzi kuna jambo limeharibika, maana jana nzima ofisi inawaka moto. Chifu huko juu ametingwa na mambo. Na afadhali uende sasa hivi, mimi nawajulisha kuwa uko kwenye lifti unaelekea ofisini kwake".

"Yaa fanya hivyo".

Niliacha mzigo wangu kwa Linda, nikaelekea ofisini kwa Chifu ambaye ofisi yake ilikuwa orofa ya tatu, na sisi tulikuwa chini katika jengo hilo hilo.

Nilifungua mlango bila kubisha hodi. Nikaingia ndani ya ofisi ya mwandishi mahsusi wa Chifu.

"Ooh, Mungu wangu! Afadhali umekuja!", Maselina alisema kwa moyo wa furaha.

"Hujambo lakini?".

"Sijambo ila wasiwasi ni juu yako tu. Pole sana, nafikiri tumekukatishia likizo murua kabisa".

"Wacha kusema. Tayari nilikuwa nimeshapata kipande cha msichana. Nilipopata ujumbe wako kidogo nipate ugonjwa wa moyo. Je kuna nini huku kinacholeta wasiwasi hivi?"

"Atakueleza mwenyewe kinachompandisha damu yake. Nakwambia amekuwa anakuhitaji kwa haraka sana, hata hivi anaona umechelewa. hivi sasa nilikuwa nataka kutuma teleksi nyingine".

"Mama yangu mzazi! mtafikiri nina roketi yangu mwenyewe!"

"Ngoja nimwambie kwamba umefika. Akifungua mlango kisha atukute tunapga soga sijui atafanya nini. Huenda atapasuka!"

"Mwache apasuke! Mnafikiri kunikatisha likizo yangu nilijisikiaje. Utadhani moyo wangu umetengenezwa kwa chuma, na wake kwa udongo".

"Kamwambie mwenyewe hayo huko ndani", Maselina alijibu akimwemwesa huku akiinua simu.

Huyu Maselina tumefanya kazi pamoja kwa muda mrefu kiasi ya kwamba uelewano wetu hauwezi kuelezeka kwa maneno. Huenda siku moja nitapata maneno ya kueleza, ila tu kwa leo naweza kusema ni rafiki yangu mkubwa.

"Chifu, namba moja yuko hapa", Maselina alitamka katika simu.

Nambari moja, ndivyo nilikuwa najulikana kikazi. Katika kazi yetu sisi hutumia namba, mimi nilikuwa namba moja hivyo unaweza mwenyewe kuchekecha ukajuwa kwa nini. Mimi Willy si mtu wa majivuno. Watu wengi, hasa wakubwa wa serikali walinijua kwa hii namba yangu. Wengi walikuwa hawajui namba moja ni Willy Gamba, ila kwa watu wachache sana. Hii ilinipa fursa hata nyumbani Dar es Salaam nijulikane kama mfanyabiashara wa kawaida tu, na si Willy Gamba ambaye ni namba moja katika Idara ya Usalama, Tanzania.

Maselina aliweka simu chini.

"Nenda ndani mara moja".

Nilifungua mlango, na nikamkuta Chifu akitembea toka kona moja ya chumba hadi kona nyingine. Kwa mtu ninayemfahamu nikajua hapo alipo alikuwa na matatizo makubwa sana yaliyomsakama rohoni mwake.

"Kaa chini namba moja', Chifu aliamru.

Chifu anaponiita kwa namba yangu ya kazi ujue kuna jambo kubwa. nilivuta kiti nikaa, yeye akazidi kutembea kona hadi kona nyingine, hatimaye akasimama nyuma ya kiti chake.

"Nashukuru kwa kufika kwako mapema, namba moja ndio sababu nakutegemea sana".

"Asante", nilijibu halafu nikaendelea.

"Mbona hivi, nini kinakuwasha?".

Alichukuwa mtemba uliokuwa mezani, akafungua mkebe wa tumbaku akaijaza, kisha akawasha na kuanza kupuliza. Alipuliza mara mbili, halafu akazungusha kiti chake ambacho kinazunguka kwenye tendegu, akaketi.

"Kina jambo kubwa limetokea!".

Aliweka mtemba wake mezani na kuweka mikono yake kwenye mezani.

Akaniangalia machoni, huku macho yake yakionesha ukali wake.

Akili yangu ikiwa tayari kusikiliza jambo hili huku moyo ukinidunda.

"Utanisikiliza, utauliza maswali baadaye".

"Sawa".

"Nafikiri nitaanza toka mwanzo. Ingawaje mambo mengine unayajua, nitayarudia tu kwa ajili ya umuhimu wa habari yenyewe ilivyo, unaonaje?".

"Utakavyoona wewe Chifu".

"Unajua nchi yetu inalea vyama vingi vya wapigania uhuru. Kama vile vyama vya wapigania uhuru toka Zimbabwe, Afrika Kusini n.k. Pamoja na kulea vyama hivi tunawapatia vijana wao ya kijeshi. Kwa vile mafunzo mengi yanapatikana hapa na makao makuu ya vyama hivi yapo hapa, basi silaha zao vile vile zinapitia hapa na sisi tunazipokea toka nchi rafiki na kuwapa wanaohusika.

"Hapa tuna vyama viwili vya wapigania uhuru katika Afrika kusini. Vyama hivi ni 'The Peoples liberation Front, of South Afrika (PLF)' kinachoongozwa na Ndugu Cecil Chimalamo na South Afrika National Party (SANP) kinachoongozwa na Ndugu Ray Simbuche. Miezi sita iliyopita Ndugu Cecil Chimalamo wa PLF

alikuwenda Urusi ambako alioba msaada wa silaha na akaahidiwa kupewa silaha hizo ambazo zingepelekwa Dar es Salaam mnamo muda wa miezi sita.

"Wiki iliyopita Ubalozi wa Urusi wa hapa mjini ulipata karatasi za maelezo ya silaha hizi ambazo tayari zilikuwa zimeshapakiwa kwenye meli siku nyingi na zilikuwa njiani kuwasili Dar es Salaam. Na makaratasi haya yalisema meli hiyo itawasili mjini hapa mnamo wiki hii'.

"Basi yalipofika, ubalozi uliyashughulikia kikamilifu kwa upande wake, kisha ukayapitisha kwenye kamati ya ukombozi ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU), maana kamati hii ndiyo inashughulikia mambo haya kama unavyofahamu. Kamati nayo ilianza kuzishughulikia karatasi hizi mpaka zikawa tayari, wakawa sasa wanangoja meli kufika. Habari kutoka kwenye Wakala wa Meli zilieleza kuwa meli hiyo itaingia bandarini Dar es Salaam tarehe tatu mwezi huu ambayo ilikuwa juzi ile".

"Baada ya kupata habari hizi kamati ilipanga pamoja na ofisi ya mambo ya silaha za wapigania uhuru pia na maofisa wa bandari wanaohusika kuwa mizigo hiyo ipakuliwe usiku wa tarehe nne yaani juzi kuamkia jana. Kwa sababu karatasi zote zilikuwa zimekamili na sehemu zote zikiwa na habari kamili, pande zote zilikaa zikisubiri silaha hizo mnamo siku hiyo kama ulivyopangwa".

Chifu alichukua mtemba wake tena akavuta kidogo kisha akauweka juu ya meza.

"Nafikiri umenielewa mpaka hapo?".

"Wakati huo mpango hii yote ya kupakua mizigo hii, ofisi ya PLF ilikuwa ikishirikishwa?", niliuliza.

"Ndio, kwa sababu huwa wanaelezwa mambo yote yanavyokwenda, hivyo huwa wana habari kamili ya mambo yote. Naweza kuendelea?".

"Unaweza".

"Sasa jambo la kushangaza likatoka juzi. Maofisa wa ofisi ya jshi la ulinzi inayoshughulikia silaha za wapigania uhuru walikwenda kwenye ofisi ya kamati ya ukombozi juzi mnamo saa nne ili kuchukua karatasi hizo za mizigo, wapate kijitayarisha kwa upakuaji wa mizigo hiyo wakati wa usiku. Walipofika kwenye ofisi hii wakakuta ofisa anayehusika hajafika kazini. Ikabidi wamwone ofisa wa juu katika ofisi hiyo kumweleza umuhimu uliopo wa kuandaa kupakua silaha hizo usiku.

"Huyu ofisa wa juu katika ofisi hii ya kamati naye alisema kuwa alikuwa ameshangazwa kwanini ofisa huyo alikuwa hajafika kazini. Hivyo wote kwa ujumla wakaondoka kuelekea nyumbani kwa ofisa huyo kuona kama anaumwa aweze kuwaelekeza wapi walipoziweka karatasi hizo. Huyu ofisa alikuwa akikaa sehemu za Upanga, Barabara ya Umoja wa mataifa, nyumba namba 1168".

"Walipofika nyumbani kwa ofisa huyo walimkuta mfanyakazi wake akiwa nje. Walipomuuliza kama wenye nyumba wapo aliwajibu kuwa yeye hakai hapo ila huwa anakuja kila asubuhi lakini alipofika asubuhi hii alikuta milango yote ya kuingilia ndani ya nyumba imefungwa. Hivyo mpaka muda huo alikuwa anasubiri kwani alifikiri wametoka. Ofisa huyo alikuwa anakaa yeye pamoja na mke wake na walikuwa bado hawajapata watoto. Ofisa mmoja wa jeshi alikwenda kuangalia gereji akakuta gari la ofisa huyu lipo na lilikuwa bado halijatoka. Kitu hiki kilimtia mashaka akawaeleza wenzake na akashauri wajaribu kuingia ndani ya nyumba huenda walikuwa bado wamo ndani. Kwani kama kutoka wangekuwa wametoka na gari lao, walikubaliane wavunje mlango wa kuingilia ndani".

Chifu alinyamaza kidogo akainua macho yake kuniangalia.

"Walishtushwa kwa kumkuta ofisa huyu amepigwa risasi amekufa sebuleni, huku akiwa amevalia vizuri kabisa kuonyesha kuwa alikuwa anatoka matembezini. Halafu ukumbini walimkuta mke wa ofisa huyo naye amepigwa risasi amekufa huku akiwa amevalia nguo za kulia. Haapo hapo wakanyanyua simu na kutoa ripoti ya vifo hivi kituo cha polisi Oysterbay ambacho hakikuchelewa kutuma maofisa wao kwenye nyumba hiyo. Baada ya polisi kufika, maofisa hao wa jeshi na ofisa kutoka kamati ya ukombozi ilibidi warudi upesi kwenye ofisi ya kamati, maana vifo hivi vilileta wasiwasi".

Wakati wote huu akieleza, mimi nilikuwa kimya kabisa na akili yangu ilichemka niliposikia habari hizi za mauaji.

"Halafu ikawaje?".

"Walirudi ofisi za kamati upesi upesi, na kuanza kutafuta makaratasi haya ya mizigo kila mahali ofisini hapa, lakini hawakuona kitu. Hapo ndipo jasho lilipowatoka. Jambo hili liliwapa wasiwasi zaidi ikabidi wakimbilie bandarini kutoa habari kwa maofisa wa bandari kuwa karatasi zimepotea".

Chifu macho yake yaliwaka nikajua karibu anasema kitu cha kustua.

"Walipofika katika ofisi za bandari, ofisa anayehusika na habari hizi, walipomweleza kuwa makaratasi yamepotea, alishangaa sana, ndipo mwishoni akawaeleza kuwa silaha zilikuwa zimeisha chukuliwa usiku uliokuwa umepita na wanajeshi waliovalia nguo za jeshi la ulinzi na wakiwa na karatasi zote za kuchukulia silaha, zikiwa kamili kabisa. Walikuwa wamefika na magari ya jeshi la wananchi, hata akawatolea namba za magari. Kundi hili lililochukua silaha liliongozwa na mtui aliyevalia nguo za cheo cha meja. Kusikia hivi kundi lote lililofika kwenye ofisi ya bandari lilichoka kabisa.

"Lakini si walikuwa wamekubaliana na ofisi ya bandari kuwa watapakua usiku wa juzi kuamkia jana, ilikuwaje yeye akaruhusu mizigo ipakuliwe usiku wa juzi ile kuamkia juzi?"

"Huko ndiko nakuja kufafanua. Ofisa wa bandari alieleza kuwa mnamo terehe tatu mwezi huu ambayo ni juzi ile kiasi cha saa kumi alipata simu toka ofisi ya Kamati ya Ukombozi. Simu hii ilikuwa inatoka kwa ofisa wa juu katika Kamati ya Ukombozi anayeshughulikia mambo ya silaha, Ndugu Jones Mantare. Ambaye ndiye aligundua maiti ya ofisa huyo wa kamati akiwa pamoja na wanajeshi. Yeye anasema sauti ya Jones Mantare anaifahamu maana ameshughulika naye siku nyingi, na sauti hii aliyoisikia kwenye simu ilikuwa kama ya Mantare hivyo akaamini kuwa anazungumza na Mantare".

"Simu hiyo ilieleza kwamba, kwa ajili ya usalama ratiba ya upakuaji silaha imebadilika, kwa hiyo silaha zilikuwa zipakuliwe siku hiyo kuanzia saa mbili za usiku kwani silaha zilikuwa nyingi. Hivyo akasema amtegemee meja mmoja wa jeshi kwa jina la Paul Liboi, atakuja pamoja na askari wa jeshi la wananchi kutoka kwenye ofisi inayoshughulikia silaha za wapigania uhuru ambaye atashughulikia kazi hiyo. Kwa hiyo, anasema alimwomba aiweke hiyo meli tayari kwa kupakuliwa saa mbili usiku. Yeye alikubali bila masharti maana kazi ya silaha ni muhimu".

"Na mnamo saa kumi na nusu wakati akishughulika na kutoa amri ya meli hiyo kupewa nafasi kwenye geti alipata mgeni mwingine. Mgeni huyu alijitambulisha kwa jina la Andrew Mwambina ofisa usalama toka kamati ya ukombozi ya OAU. Alitoa kitambulisho chake na ofisa huyu wa bandari alivyokiona kilionekana halali maana ameshawahi kuona vitambulisho vya watu hawa. Mtu huyu alimwuliza kama amepata habari kuwa upakuaji umebadilishwa na ilibidi silaha zipakuliwe usiku huo saa mbili. Yeye alikubali kuwa amepata ujumbe na muda huo alikuwa

anashughulikia jambo hilo. Ofisa huyo wa usalama alimwaga na kumwambia yeye na wenzake watakuwepo kikazi kama kawaida, akaondoka".

"Kwa taarifa yako. Namba moja maafisa watatu wa usalama wa Kamati ya Ukombozi ambao walipangiwa kufanya kazi bandarini tangu ilipofahamika kuwa meli hiyo inaingia walikuwa wameuawa na maiti zao zilikutwa sehemu ya Shimo la Udongo jana jioni".

Chifu alitua kidogo kupuliza mtemba wake.

"Taarifa ya ofisa wa bandari iliendelea kusema kuwa ilipofika saa mbili kamili za usiku magari manne ya jeshi tani kumi na mbili kila moja yaliingia. Na mtu aliyejitambulisha kama Meja Paul Liboi alifika ofisini kwake akiwa amevalia kijeshi na cheo chake kwenye mabega. Yeye alisema amekuja kushughulikia upakuaji wa silaha na kwamba aliamini ameshapewa habari na kamati ya Ukombizi mapema, na akatoa karatasi za kupokelea mizigo ya silaha ambazo zilikuwa sawa".

"Yeye alimjibu kwamba alishapata habari na mipango yote ilikuwa tayari, hivyo baada ya kumaliza shughuli za makaratasi alitoka na Meja huyu na kuwaelekeza meli ilipokuwa tayari kwa upakuji. Aliendelea kueleza kuwa magari haya manne yalikuwa na askari wengi waliovalia kijeshi. Hivyo silaha zilianza kupakuliwa saa tatu na kufikia saa kumi alfajiri gari la mwisho liliondoka. Silaha zilikuwa nyingi sana za kisasa na za hali ya juu. Nafikiri umenielewa mpaka hapo".

"Ndio nimekuelewa".

"Sasa kitu cha kutia huzuni ni kwamba silaha hizi zimepotea hazijulikani zilipo. Na wala watu na magari yaliyochukuwa silaha hizi hayajulikani yalipo mpaka dakika hii tunapozungumza. Idara ya polisi imejaribu kutafuta lakini mpaka sasa hawana hata fununu. Huu ni wizi wa silaha uliopandwa barabara na kwa serikali yetu hii ni "KASHFA", kwa taarifa yako habari hizi zimevunja na zimeshatangazwa na nchi za Magharibi pamoja na Afrika Kusini juu ya tukio hili. Na tayari nchi adui za Tanzania zimeanza kuropoka ovyo ili kulichafua jina la nchi hii".

"Mimi ninadhani hizi ni hila na Njama za mabeberu, wapinga mapinduzi wa mapambano Kusini mwa Afrika. Nia yao ya kufanya hivi ni kutaka mambo matu. Nia yao ya kwanza ni kuhujumu, kuchukua silaha hizi kusudi zisiwafikie wapigania uhuru ambao mapambano yao huko Kusini mwa Afrika sasa yanapamba moto, maana silaha hizi zilikuwa za kisasa na zingalifika kwenye uwanja wa

mapambano wanajua wangepata cha mtemakuni. Kwa hiyo hizi ni njama za kuhakikisha kuwa silaha hazifiki kwenye uwanja wa mapambano".

"Pili, wanataka kulipaka matope jina la Tanzania kwa vile Tanzania imeamua kuongoza ukombozi kusini mwa Afrika sasa ina maadui wengi sana, na maadui hawa wameanza kulipaka matope jina la Tanzania na kusema kuwa Tanzania huzitumia hizi silaha kwa majeshi yake. Wendawazimu wengine wameendelea kusema eti Tanzania kwa muda mrefu imekuwa inatumia misaada inayotolewa kwa faida yake!".

"Hivi hili jambo si geni. Nia yao ya tatu ni kutaka kuzikatisha tamaa nchi rafiki zinazotoa misaada kwa wapigania uhuru, zisizidi kufanya hivyo, kwa kufikilia kuwa wanapoteza mali zao kwa kufanya kazi ambazo wao hawakuzipangia. Kwa hiyo, namba moja unaona hali ya hatari nchi yetu ilimo".

"Lo! ni hali mbaya sana. sasa sisi tunatakiwa kufanya nini?".

"Jambo hili sasa linashughulikiwa na Idara ya polisi na ofisi ya usalama. Upelelezi wao bado unaendelea na ni mkali sana. Katika usiku wa kuamkia jana serikali imeamua sisi lazima tulishughulikie jambo hili. Maana inaamini wizi huu uliofanywa ni wa kimataifa, hivi polisi hawakuzoea kupambana na hali kama hii. Kwa hiyo ingawake wao wataendelea na shughuri zao, sisi itabidi tujishughulishe kikamilifu juu ya jambo hili maana ni kima chetu polisi wameagizwa kuleta nakala ya ripoti zao zote za upelelezi wanaoufanya. Hii itafanya kupata habari nyingine ambazo zitatusaidia sana".

"Serikali inataka jambo hili litatuliwe haraka kusudi tuweze kuwafichua hao maadui zetu wanaotaka kutupaka matope, maana itabidi tuionyeshe jumuiya ya ulimwengu jinsi maadui zetu wanavyojaribu kutupiga vita kwa ajili ya msimamo wetu thabiti katika ukombozi wa Afrika. Na hatuwezi kufichua ukweli wa jambo hili mpaka hapo tutakapowakamata hawa waliofanya kitendo hiki. Kwa hiyo kazi yetu sasa ni moja tu, nayo ni kuwakamata watu hawa. Na wewe namba moja umepewa jukumu hili kubwa la kulinda hadhi ya nchi yako, Tanzania. Una maswali?".

"Nipe muda kidogo nifikiri".

Nikasimama na muda huu kwa ajili ya mafikara niliyokuwa nayo nilianza kutembeatembea toka kona hadi kona ya chumba kama nilivyomkuta Chifu akifanya. Ilionekana Chifu alijisikia nafuu baada ya kutua mzigo huu kwangu ikawa zamu yangu kubanwa na mawazo ya tukio hili.

"Hizi habari zimevujaje?".

Niliuliza huku bado natembeatembea nimeinamisha kichwa chini.

"Naamini, maharamia hao hao ndio wamezitoa ili wafanikishe moja ya shabaha zao. Yaani kuivunja Tanzania hadhi".

Mara moja nikawakumbuka Sherrif na Veronika nikajuwa lazima habari hizi zilikuwa zimeshafika ofisi za gazeti la Afrika na Sherrif alikuwa anakuja Dar es Salaam ili kuja kuchunguza na kuandika juu ya tukio hili. Katika mipango yangu iliyokuwa inapita kichwani nilipata pointi moja ya kunisaidia.

"Huyu Jonas Mantare anasemaje juu ya tukio hili?".

"Baada ya kupata maelezo ya ofisi ya bandari, mara moja polisi walimkamata Jonas Mantare kwa kusaidia polisi katika uchunguzi, yeye alipoulizwa kama yeye ndiye aliyepiga simu, alikataa kabisa, na kukataa kwake kumedhihilishwa na Mwenyekiti wa kamati ya ukombozi kuwa Mantare alikuwa ofisini mwake toka saa tisa mpaka saa kumi na moja siku hiyo wakifanyakazi pamoja na wala hawakutoka hata dakika moja katika muda wa masaa hayo mawili".

"Kwa hiyo kutokana na usemi wa ofisa wa bandari, kuna mtu mwingine aliyeiga sauti ya Mantare. Hii ina maana mtu huyu amemzoea".

Nikarudi na kuketi kwenye kiti kwani akili zilianza kufanya kazi. Kwa mara ya kwanza nilitoa paketi yangu ya sigara nilizokuwa nimenunua katika ndege, nikaanza kuvuta.

"Bila ya shaka", Chifu alijibu.

"Ofisa huyo aliyeuawa anaitwa nani?".

"Anaitwa Kamara Frank, yeye ni mwenyeji wa Sierra Leone".

Unaona sasa mambo yanavyokuwa huyu mtu alikuwa rafiki ya Sherrif kama unakumbuka.

"Daktari anafikilia Frank na mkewe walikufa saa ngapi?".

"Daktari anakadilia kuwa walikufa kati ya saa sita na saa nane usiku. Na inavyoonekana ni kuwa kuna wakati alikuwa amefungwa kamba, maana alama zinaonekana kwenye mikono na miguu".

"Sasa Chifu kuna jambo moja ambalo lazima tuelewane. Tangu nimeanza kazi hii nimekuwa nikifanya kazi zangu nje ya Tanzania. Hapa nyumbani najulikana kama mfanyabiashara tu. Lakini kama nikianza shughuli hii lazima nitajulikana hasa mimi ndiye nani. Unasemaje?".

"Nani anajali", alifoka Chifu kwa sauti ya juu. "Kitu ninachotaka mimi ni kuona jambo hili linatekelezwa na washenzi hawa wamekamatwa. Kama itabidi ujulikane potelea mbali!".

"Lakini Chifu..."

"Hamna cha lakini hii ni amri ya serikali na serikali inataka matokeo juu ya suala hili na mapema iwezekanavyo".

Nilijuwa kuwa kweli iko kazi kama kweli Chifu kakubali mimi nitambulike kirahisi hivi nilikaa nikaanza kufiri jinsi ninavyoweza kufanya upelelezi wa tukio hili bila kutambuliwa maana mimi sikuwa nataka kabisa nijulikane kama mimi ni mpelelezi hapa nyumbani. Kwani watu wengi Tanzania wanajuwa wana mpelelezi mashuhuri, kiasi cha kujitapa mitaani lakini hawajui kuwa ni mimi Willy Gamba. Na hivi ndivyo nataka, vinginevyo kila nitakapokuwa napita nitakuwa nafuatwa na kundi la wapenzi.

"Najuwa waandishi wa habari toka nchi za nje watakuwa na shauku kubwa kuja kuandika habari hizi. Kuna msimamo gani?".

"Haturuhusu waandishi wowote toka nje. wamezuiliwa mpaka hapo tutakapokuwa msimamo kamili wa jambo hili. La sivyo watakuja kuzidi kuchafua mambo hapa. hatutawaruhusu kabisa idara ya uhamiaji imeshaelezea na imeshatoa amri kwa vituo vyake, na jambo hili limeanza kutekelezwa. Asubuhi hii nchi za Magharibi zimelalamika kusikia haturuhusu waandishi wa habari toka nje.

Nilichukua nafasi hii kumweleza Chifu juu ya kukutana kwangu na Veronika Sherref. Nikaendelea kumweleza kila kitu juu ya kuja kwao hapa.

"Hivyo nahisi gazeti la "Afrika" linawatuma waje kwa ajili ya tukio hili. Ni lazima wameishapata habari".

"Hawataruhusiwa kuingia".

"Mimi naomba hawa waruhusiwe kwa sababu nafikiria kuwatumia katika shughuri hii".

"Haiwezekani, watakuja tifuu mambo tu, sitaki kuona waandishi wa habari toka nje!", Chifu alifoka huku akionyesha hasira.

"Sasa Chifu, ni lazima tuelewane, hili jukumu umenipa mimi. Na inabidi mimi mwenyewe nipange ninavyoona, jinsi nitakavyoweza kulitua tatizo hili, na kama sasa hatuwezi kukubaliana, sijui shughuli itawezekanaje?"

Chifu alinyamaza kwa muda mrefu.

"Hebu ni majina kamili ya watu hao".

Nikampa. Akainua simu, akazungumza na Maselina.

"Hebu angalia kwenye mafaili ya waandishi wa habari hasa waandishi wa gazeti la "Afrika", angalia kama kuna faili zozote za majina ya Veronika Hamadu na Ahmed Sherrif wote kutoka Sierra Leone".

Akaweka simu chini, tukasubiri katika ukimya. Baada ya kitambo kidogo Maselina alifungua mlango akaingia na mafaili mawili, akampa Chifu. Chifu alipoinama kuyafungua kusoma,

Maselina alinikonyeza na kufua mlango, akatoka nje.

SURA YA PILI

CHIFU alisoma faili la kwanza, alipomaliza akanitupia. Lilikuwa faili ya Ahmed Sherrif. Na mimi nilianza kulipitia kwa makini sana nilipomaliza kulisoma Chifu alikuwa nae amemaliza kusoma faili la Veronika Hamadu, akanitupia. Nilisoma faili la Veronika kwa makini vile vile, lilikuwa na habari zilizonifanya nitabasamu mara kwa mara mpaka nilipomaliza. Nilikuta Chifu ameegemea kwenye kiti chake akaniangalia kwa makini.

"Oke, wataruhusiwa kuingia, inaonekana wanaweza kuwa wa manufaa kwako. Sijui unataka kuwatumiaje, kama hutajari kunieleza".

Baada ya kuwa nimesoma mafaili ya watu nilikata shauri namna ya kushughulika nao. Hivyo nilionelea juu ya mipango yangu maana huyu mzee kichwa chake kinafanyakazi. Kama akiona kuna kitu chochote hakifai atanikosoa mara moja. Waliompa kazi hii ni dhahiri walichagua mtu hasa anayefaa. Sidhani kuna mtu wa uwezo kama wake katika kuongoza kazi hii katika nchi hii. Yeye hiki ni kipaji alichopewa na Mungu. Na maendeleo yote ya idara hii ya upelelezi yamefanikishwa na uongozi wake ulio thabiti na wa busara.

"Mimi bado nahitaji kufanya upelelezi katika tukio hili, kujulikana kuwa mimi ni mpelelezi kwa watu wengi. Hivyo nimepanga kuwa kampuni yetu Afrikan International Agencies itakuwa wakala wa gazeti la Afrika. Kwa kufanya hivyo kampuni hiyo itawapokea hawa waandishi wa gazeti hilo kama wageni wake kwa sababu mimi najulikana kama meneja mkuu wa kampuni hivyo nitaandamana nao katika kutafuta habari zao nikiwa kama mwenyeji wao na kwa vile nafahamika hapa Dar es Salaam, nitawaongoza na wakati huo huo nitakuwa nafanya upelelezi wangu. Kwa kufanya huvi nitaweza kushughulika bila kutambuliwa kuwa mimi ni nani na ninafanya nini. Mpango kamili nitapanga na nitakueleza".

Alikaa kimya kutafakari mpango wangu.

"Vizuri sana, namba moja, akili yako inafanyakazi. Nimeishaona shughuli yote itakavyokuwa kwa urefu. Mpango wako ni mzuri, endelea nao. Unafikiri hawa waandishi watafika saa ngapi".

"Si zaidi ya usiku wa leo".

"Oke nitapeleka habari sasa hivi watu hawa waruhusiwe kuingia. Wewe nenda sasa ukapumzike maana najua haujalala tengeneza mpango wako wote wa upelelezi huo, na uniletee kesho asubuhi. Lakini kumbuka kazi hii ni kubwa na ya haraka, hivyo msaada wowote utakaoutaka utapewa. Ofisi yote imeweka kando kazi nyingine mpaka tutakapoona mwisho wa kazi hii. Mungu akusaidie kama amnavyo amekusaidia siku zote. Nina imani na wewe Willy. Najua utafanikiwa. Kwa heri Willy mpaka baadaye, kapumzike".

Chifu anapoanza kuniita Willy ujuwe kuna kitu kimemfurahisha hasira na wasiwasi wake umepungua. Na anakuwa na imani kuwa kazi itafanyika.

"Asante", nilijibu.

Niliangalia saa yangu. Ilikuwa saa saba za mchana mkutano huo ulikuwa umechukua muda mrefu sana. Nilimwaga Chifu nikamwahidi kumletea nakala ya mpango wangu wa operesheni hii asubuhi.

Nilifungua mlango nikaingia ofisini kwa Macelina.

"Kazi kubwa unayo, pole sana Willy".

"Nitafanyaje Macelina, mimi mwenyewe nilikubali kazi hii sasa siwezi kurudi nyuma. Na vile vile kwa sababu tukio hili linahusu wapigania uhuru, niko tayari kabisa kwa lolote. Wewe mwenyewe unajuwa moyo wangu ulivyo juu ya ndugu zetu wanaoteswa huko Kusini mwa Afrika".

"Naelewa Willy, naelewa sana roho yako ilivyo juu ya ukombozi wa Afrika Kusini. Vijana wote wa Kiafrika wangekuwa na roho kama yako sasa hivi kungekuwa hakuna ukoloni Afrika".

"Asante kwa kunipa moyo".

"Usiwe na wasiwasi, naamini mungu atakusaidia kama siku zote, maana wewe unatetea wanyonge wanaoonewa. Hata hivyo tukio hili ni hatari kuliko mengine yote. Pole sana".

"Asante tena Maselina. Vipi huendi kula mchana?. Twende nikakununulie chakula cha mchana".

"Ngoja nimwage Chifu".

Maselina aaliingia ndani, alipotoka akasema ameruhusiwa muda wa saa moja tu saa nane ilimbidi awe kazini.

"Yeye haendi kula?".

"Ana vitafunio vyake humo ofisini, ndio hatoki tena. Huyu mzee kazi itamwua".

"Shauri yake. Yeye ameshaula kidogo si kama sisi. Miaka sitini ni miaka mingi.

Maselina alichukua mkoba wake tukaondoka.

Niliingia ofisini kwangu mnamo saa nane baada ya kupata chakula kitamu na Maselina.

"Linda nipeleke Colt Motors nikachukue gari langu".

"Hamna taabu bosi, twende zetu", Linda alijibu huku akichukua mkoba wake. Gari langu ni aina ya Colt GallantCoupe hivyo kila nikisafiri huwa naliacha kwenye kampuni yao.

"Vipi bosi, naona umeitwa shauri ya wizi wa silaha wa majuzi", Linda alinidadi.

Huyu katibu wangu mahsusi alikuwa amefanya kazi nasi kwa muda wa miaka minne na mwaka huu alifikia kiasi cha kuaminika sana na kupewa nafasi ya kuwa katibu mahsusi wa Namba Moja.ambacho ni cheo cha juu sana. Kwa upande wa makatibu mahsusi yeye alikuwa amejipatia nafasi ya pili ya kuaminika baada ya Maselina. Alikuwa msichana mwenye akili nyingi, na alikuwa mzuri wa urubi. Alikuwa na kila sifa anazostahili katibu mahsusi kwa mpelelezi wa hali kama yangu. Nilimpenda kwa jitihada zake za kazi na nilimtegemea bila wasiwasi.

"Ndio Linda, matatizo kila wakati hutokea wakati niko katika kilelel cha maraha, sijui mkosi gani huu.

"Mimi huwa naamini huwa unapata raha fulani katika pilika pilika zako, maana kila ukimaliza shughuli fulani huwa nakuona katika hali ya furaha sana".

"Hiyo inatokana na kumaliza kazi yangu katika hali ya kuridhisha".

"Unafikiri watu hawa wameiba hizi silaha kusudi wazitumie kupindua serikali?", Linda aliuliza.

"La hasha, wanajua hawawezi kabisa kupindua serikali, maana wananchi wote wa nchi hii wamejidhatiti katika ulinzi. Mimi nafikiri wana sababu nyingine, na sababu hii nitaipata katika muda si mrefu".

Saa nane hii magari yalikuwa mengi maana watu wengi walikuwa wanarudi makazini. Hivyo barabara hii ya Pugu ilikuwa na msongamano wa magari. Linda alitumia ujuzi wake wote ili kujipenyezapenyeza tuweze kufika upesi.

"Lazima nikupeleke upesi bosi maana najua una bongela usingizi".

"Ndio sababu sikuchukii Linda, maana huwa ndiye mtu unayenionea huruma, wewe na Maselina, wengine wote wanafikiri mimi nimetengenezwa kwa chuma".

"Hata mimi lazima niungame kuwa huwa vile vile nafikiri wewe si binadamu wa kawaida maana mambo unayofanya nashindwa hata kueleza".

"Taa kwenye barabara hii zimezidi, hapa na pale taa, nadhani ndizo zinazosababisha msongamano wa magari", Linda alilalamika wakati tukiwa tumesimamishwa kwenye taa za usalama barabarani za karibu na Shirika la Usagaji na ofisi za Tazara..

"Hata mimi nafikiri hivyo hivyo. Nafikiri barabara hii ingefanywa barabara muhimu, na magari yote yatakiwe kwenda kasi, tuseme si chini ya kilomita themanini kwa saa. Hii ingesaidia watu kufika kazini haraka au wasafiri wanaosafiri kwa ndege wasingekuwa na wasiwasi wa kuchelewa kama ilivyo hivi sasa".

Tulipoingia Colt Motors tulimkuta meneja ndio anarudi kipindi cha alasiri.

"Mbona umerudi haraka nawe ulisema utarudi baada ya wiki tatu?," meneja wa karakana aliniuliza.

"Nilipata habari kuwa mama anaumwa ikabidi nirudi haraka sana".

"Oh pole sana, kuna kitu chochote tunaweza kusaidia?".

"Asante sana, nimemwona; anapata matibabu ya kutosha huko hospitali ya Muhimbili".

"Kama utahitaji msaada wakati wowote usisite kusema".

"Asante, nitakumbuka", nilijibu.

Tulikuwa tumejenga uhusiano mzuri wa kibiashara na kampuni hii. Nilifuatana na Linda mpaka kwenye gari lake nikachukua mfuko wangu.

"Linda itabidi umwambie Godwin aweke watu wa kuaminika sana kwa usiku wa leo maana nategemea wageni. Akipata habari zozote anieleze moja kwa moja

nyumbani, mimi sitakwenda mbali leo. Nitatoka kidogo saa mbili hivi na nitakuwa Palm Beach Hoteli kwa chakula cha jioni, lakini baada ya chakula nitarudi nyumbani.

"Usiwe na sahaka, yote yatatekelezwa kama ulivyotaka".

Tuliagana mimi nikaingia ndani ya gari langu na kuelekea nyumbani kwangu Upanga.

Wakati nilipokuwa nimeondoka, kwa kujua kwamba nitakaa nje karibu mwezi mzima, nilikuwa nimemweleza mfanyakazi wangu naye achukue likizo. Alikuwa amekwenda Morogoro.

Nilipofika nyumbani kwangu, nyumba ambayo iko barabara ya Upanga karibu na Hoteli ya Plm Beach, nilimkuta mlinzi niliyekuwa nimemwajiri kwa muda kutoka kampuni ya ulinzi.

"Hapa salama", niliuliza.

"Salama tu, Mzee", alijibu.

"Nimerudi, hivyo sidhani kama nitakuhitaji tena. Nitawapigia simu ofisini kwako, hivyo unaweza kuondoka.

"Asante sana Mzee", alijibu huku akiondoka.

Niliweka gari langu gereji, nikafungua mlango wa nyumba, nikaingia ndani. Nyumba ilikuwa shwali kabisa.

Nilipomaliza kuoga ilikuwa saa kumi kamili za mchana, nilijibwaga kitandani nikalala na kupata usingizi moja kwa moja. Nilipoamuka ilikuwa saa moja na nusu. Hivyo nilivaa nguo nikanawa uso na kuelekea Palm Beach Hoteli. Kwa sababu Palm Beach ni karibu na nyumbani kwangu nilitembea kwa miguu. Na nilipoingia Palm Beach niliagiza chakula nikaomba nipewe haraka kwa sababu mimi najulikana kwenye Hoteli hii, nilishughulikiwa haraka sana.

Nilikula chakula changu upesi upesi na kurudi nyumbani. Nilipofika nyumbani nilivaa nguo za kulalia na kuingia kitandani. Kwa vile nilikuwa na usingizi mzito nilikuwa nasikia uchovu tena nilijua huu ndio ulikuwa usiku wangu wa kulala, maana siku zifuatazo nilijua kulala kwangu kutakuwa haba kweli. Usingizi ulinichukua mara tu baada ya kujitupa kitandani.

Niliamswa na mlio wa kengere ya simu. Nilipoangalia saa yangu ilikuwa inasema yapata saa nane.

Niliinua simu.

"Hallo Gamba hapa".

"Hallo bosi habari za kulala?".

"Lo Linda vipi?, bado uko ofisini".

"Nilijua kazi uliyoagiza inaweza kuwa ya maana hivyo nilionelea niishughulikie mwenyewe".

"Oh, mtoto wewe, wacha kufanya hivyo wewe bado mdogo unahitaji usingizi wako, tuachie sisi mambo hayo".

"Ni lazima nianze kujikomaza, vinginevyo sitaweza kulingana na shughuli zako, maana nimejifunza toka kwa Maselina ambaye anaweza kukaa siku mbili bila kulala kama kuna kazi inayobidi kufanyika kiasi hicho. Hivyo na mimi lazima nijizoeze muda huo ufikapo nisiuone mgumu".

"Haya mama, nafikiri una sababu ya maana. Haya leta ujumbe, naamini hukunipigia kunielezea uko ofisini mpaka saa hizi".

"La hashu, kuna wageni wako wawili wameingia hapa mjini wameniambie nikupashe habari zao. Ahmed Sherref amefikia New Afrika Hoteli na Veronika Amadu amefikia Kilimanjaro Hoteli. wanasema kama inawezekana uwapigie simu sasa hivi".

"Asante nitafanya hivyo. Sasa wewe nenda ukalale. Mpigie Juma aje aendelee na kazi maana nitakuhitaji kwa kazi kesho asubuhi".

"Haya bosi nitafanya hivyo".

"Kwa heri, kalale salama mtoto wewe".

"Asante", alijibu na kukata simu.

Niliinua simu tena na kupiga New Afrika.

"Hallo New Afrika Hoteli habari yako ndugu?".

"Nzuri".

"Nipe mapokezi".

"Oke".

"Halo mapokezi hapa".

"Nina mgeni wangu hapa ameingia usiku huu anaitwa Ahmed Sherrif naomba kuzungumza naye".

"Subiri bado yuko hapa mapokezi".

"Willy hapa habari ya safari?".

"Ohoo Willy, ofisi yako inafanya kazi vizuri sana tayari umeshapata habari?".

"Ndio, mmefika salama?".

"Ndio salama, salimini".

"Tulifikiri hatutaruhusiwa kuingia kama waandishi wengine wanavyorudishwa uwanja wa ndege wasiingie Tanzania. Lakini sisi tumeruhusiwa ni ajabu sana".

"Usijali tutazungumza kesho".

"Oke tuonane hapa Hotelini saa nne maana nina usingizi tele hapa niliposimama".

"Oke, tutaonana saa hizo, lala salama".

"Asante sana Willy".

Nilikata simu kisha nikapiga Kilimanjaro Hoteli.

"Halo Kilimanjaro hapa".

"Habari yako ndugu?".

Nilimsalimia Opareta.

"Nzuri".

"Nina mgeni wangu amefikia Hotelini kwenu hapo nafikiri bado yuko mapokezi anaitwa Veronika Amadu".

"Subiri amepolekwa sasa hivi chumbani kweke".

"Halo", nilisikia sauti ya Veronika.

"Halo binti hujambo?".

"Halo Willy, hujambo mpenzi?".

"Sijambo mie, pole na safari".

"Asante nimepoa".

"Najua umechoka nilitaka kujua tu kama umfika salama".

"Nimefika salama. Njoo unione saa tatu hivi kesho nitakuwa nimeisha amka".

"Uko chumba gani?"

"Niko orofa ya pili 208".

"Oke binti, tutaonana asubuhi".

"Ukifika gonga mara mbili haraka haraka, halafu ya tatu subiri kidogo halafu gonga nitajua ni wewe".

"Asante nitafanya hivyo".

"Kwa heri mpenzi, tutaonana asubuhi".

"Asante, kwa heri".

Niliweka simu chini nikalala ili nipumzike tayari kwa shughuli za asubuhi.

SURA YA TATU

VERONIKA NA SHERRIFF

Asubuhi hii niliamka mapema, na baada ya kuoga na kuvaa vizuri niliamua nikastaftahi hapo Palm Beach Hoteli, kwani niliona uvivu kujipikia chai. Kama kuna kitu nachukua ni mambo ya kupikapika.

Nilikuwa mtu wa kwanza kufika Palm Beach Hoteli kwa ajili ya kusitaftahi. Kijana mmoja muuza magazeti alinifuata ndani ya chumba cha chakula na kuniuzia magazeti ya Daily News na Uhuru. Nilipitisha macho kwenye magazeti haya huku nikisubiri niletewe chemsha kinywa.

Magazeti haya yalijaa habari nyingi kama kawaida, lakini habari juu ya tukio lililokuwa limetokea katika wiki hii haikuwemo. Bila shaka ilikuwa imeachwa kwa ajili ya usalama. Nilipoletewa chemsha kinywa niliishambulia haraka haraka, nikalipa na kuondoka kuelekea ofisini. Wakati huo ilikuwa yapata saa moja na nusu.

Nilipokuwa napita karibu na nyumba yangu, mara akili ikanijia kuwa afadhali nichukua bastola yangu kwani nisingeweza kuamini tu kuwa hali ilikuwa ya usalama. Nilirudi nyumbani kwangu, nikachukua bastola moja aina ya 38mm ya kipolisi na kuiweka ndani ya shati langu kwa jinsi ambavyo isingeweza kuonekana kwa urahisi.

Nilichomeka shati vizuri, nikafunga mkanda wa suruali na kuifungia vizuri bastola chini kidogo ya kitovu. Kwa sababu kulikuwa na hali ya mawingu-mawingu nilivaa jaketi juu. Kisha nikaelekea ofisini.

Nilikuta ofisi imeshafunguliwa, nikapita nikawasalimia maofisa wangu wadogo, kisha nikaelekea ofisini kwangu. Linda alikuwa tayari ameshafika.

"Halo bosi, umelalaje?", Linda alinisalimia nilipofungua mlango na kuingia ndani.

"Safi kabisa, je wee?".

"Mimi ndiye nimelala vizuri kabisa, hata sikuota leo ingawaje mimi ni muotaji".

"Itabidi uwe unalala si chini ya masaa sita, bado mtoto mdogo wewe".

"Sawa, lakini panapokuwa na shughuli maalum sina budi kukesha.

"Kama ndivyo hivyo naona kazi itafanyika".

"Na usiwe na shaka, itafanyika".

"Niitie Eddy aje ofisini kwangu".

"Sawa bosi".

Kwa sababu Namba mbili, tatu na namba nne walikuwa safarini huko Kusini mwa Afrika kwa shughuli maalum, ilibidi katika shughuli hii nishirikiane na kijana Eddy Kisanga, ambaye alijitokeza kuwa kijana shupavu sana katika kazi yetu hii.

Eddy alikuwa kijana mwenye umri wa miaka ishirini na mitatu, lakini alikuwa na akili za kuweza kumiliki matatizo na kujifunza mambo magumu katika kazi yetu hii kwa haraka sana.

Kitu cha kutufurahisha ni kwamba alikuwa mwanafunzi wangu mimi mwenyewe, hivyo matendo yake yalifanana na yangu, kiasi kuwa hapa ofisini aliitwa Willy mtoto. Na yeye alikuwa akifurahi sana kuitwa hivyo. Kwa hiyo nilipopeleka jina lake kwenye kamati ya upelelezi, nikawa nimeweka sifa zake kama mimi haikuwa ajabu kukuta amethibitishwa.

Baada ya kuthibitishwa ilibidi apewe kazi maaum ili kumpima na kuweza kumpa namba. Hivyo yeye na Sammy Rashid namba mbili walikuwa kwenye kazi maalum huko Johannesburg, Afrika Kusini. Kazi hiyo ilitekelezwa vizuri sana, na waliporudi namba mbili alitoa ripoti juu ya kazi hiyo na ikaonekana sehemu aliyofanya Eddy ilimshangaza hata Chifu, Eddy aipewa namba ya juu kuiko wote tuivyotegemea na kutokana na muda wake kazini; Kutoka kwenye kamati ya usalama alipewa namba 'TANO'.

"Eddy yuko hapa", Linda ainieleza kwa simu.

"Mwambie aingie", nilimjibu.

Eddy aiingia ndani nikamuonesha kwa ishara ya mkono avute kiti aketi.

"Habari za leo bosi", alisalimia Eddy.

"Nzuri, habari yako wewe?"

"Ni nzuri".

"Eddy natumaini umesikia jambo lililotokea hapa mjini siku chache zilizopita?"

"Ndio, lakini nimezisikia kwenye radio za nje, na rafiki yangu mmoja polisi wa kituo cha kati, ndiye aiyenielezea kwa kirefu kidogo. Vile vile alinieleza kuwa wao ndio wanapeleleza tukio hili lakini kufikia sasa hawajafika popote. Wanasema mpaka sasa hawajaona au kupata kitu chochote kinachohusika na tukio hilo. Hata hivyo wanasema watajitahidi".

"Kwa kutokana na hali ya namna hiyo serikali imeamua kutupa sisi jukumu hili, ingawa polisi wataendelea na upelelezi kamambe juu ya tukio hilo. Na ndio sababu nimeitwa kurudi mara moja toka likizo. Kwa hiyo toka sasa hivi ahirisha mambo yako mengine yote na tushughulikie tukio hili. Umenielewa?".

"Bila shaka".

Nilianza kumweleza jinsi nilivyoendesha mipango yangu yote nikiwatumia Sherriff na Veronika.

"Kwa hiyo Eddy, ninachotaka wewe ufanye, kwanza, nataka ukodishe magari manne kutoka kwenye kampuni mbali mbali zinazokodisha magari hapa mjini kama vile Co-cabs, Safari Toures Afrika Ltd., Takim's Agancies, nk. Gari moja kati hizi liegeshe mahali pa kuegesha magari New Afrika Hoteli na lingine liegeshe Kilimanjaro Hoteli. Magari mawili yatakayobaki nataka wewe pamoja na kijana mwingine kati yetu mtufuate kila mahali tutakapokwenda leo. Lakini mtufuate kwa siri kabisa kiasi kwamba mtu yeyote asitambue kama mnatufuata sisi. Mimi nitatumia gari langu. Nia yangu nataka muwe macho kama kuna watu wengine watakaoweza kuwa wanafuata safari yetu kwa siku ya leo. Umeelewa?".

"Nimeelewa vizuri kabisa bosi. Kazi itatekelezwa. Si ajabu hata wewe hutatuona."

"Kazi ya namna hiyo ndio nataka".

"Utapata, bosi."

"Gari zile utakazoziegesha New Afrika na Kilimanjaro Hoteli, weka swich ya gari hizi chini ya zuria kwa upande anaotoka dereva."

"Nitafanya hivyo."

"Haya sasa nenda ukashughulike na kazi hii ili saa nne muwe tayari nje ya New Afrika Hoteli ambapo ndipo tutaanza safari yetu."

"Tutakuwa hapo saa hizo, usiwe na wasiwasi".

ILIKUWA saa tatu kamili niliposimama mbele ya chumba namba 208 katika ghorofa ya pili ya hoteli ya Kilimanjaro, niligonga mlango mara mbili haraka haraka, halafu nikatulia kidogo kisha nikagonga tena. Hivi ndivyo nilivyokuwa nimeelekezwa.

"Karibu", nilisikia sauti kali ya juu ikitokea ndani ya nyufa za mlango. Nilifungua nikajikuta katika sebule ya chumba hiki ambamo Veronika alikuwa amevaa kaputula na sidiria tu akifanya mazoezi ya viungo. Alikuwa ameelekea upande mwingine na kunionesha mgongo na kuendelea na mazoezi yake kama kwamba hakuna mtu aliyeingia. Nilirudisha mlango, nikaugegemea na kutazama jinsi binti huyu alivyokuwa akichukua mazoezi.

"Karibu Willy Gamba, kaa kwenye kiti upumzike", alinielekeza bila kugeuka na huku akiendelea na mazoezi yake. Kisha akaanza kusema kana kwamba anajizungumzia yeye peke yake.

"Willy Gamba anayejiita mfanyabiashara huku ni mpelelezi mashuhuri wa Afrika. Afadhali ningejua mapema naamini ingekuwa furaha kubwa kuonana na mtu huyu mashuhuri nyumbani kwetu. Lakini nimekuja kujua mjini London katika ofisi za gazeti la 'Afrika', hasa ni hii teknolojia iliyoingia ulimwenguni maana tumeelekezwa na komputa ya pale ofisini. Sherriff aikuwa na mashaka kuwa amewahi kusikia jina la Willy Gamba mahali. Hivyo kufika tu London akailisha komputa hiyo jina la Willy Gamba. Maana komputa hiyo imeweka kwenye ubongo wake waandishi wote maarufu wa habari, wapelelezi wote maarufu ulimwenguni, wakubwa wote wa serikali mbali mbali na watu wote maarufu katika nyanja mbali mbali.

"Lo! Alipoilisha jina hili ndipo ikatutolea maajabu. Ilionyesha kuwa Willy Gamba mwenye umri wa miaka ishirini na tisa, mwenye urefu wa futi tano na inchi kumi na mwenye umbo la kupendeza sana ni mpelelezi maarufu ulimwengu mzima. Iliendelea kusema kuwa Willy Gamba amehitimu katika chuo kikuu cha Dar es Salaam na kupata shahada katika sheria. Baada ya kutoka chuo kikuu moja kwa moja aliteuliwa kwenda kujifunza mambo ya upelelezi kwa kutokana na sifa zake alizoandikiwa na wakubwa wa Jeshi la Kujenga Taifa, wakati akiwa katika Jeshi hilo".

"Komputa ilieleza kuwa Willy Gamba anasemekana amepata mafunzo katika nchi mbali mbali kama vile Uingereza, Cuba, Urusi, Marekani, China na Japan. Kutokana na mafunzo haya amejulikana kama mtu hatari katika kutumia aina yoyote ya silaha. Vile vile anajua karate na Kung-fu ya hali ya juu kwani wakati

akiwa Japan aliwahi kushindana na Inoki na kutoka sare naye. Watu wanashangaa kwanini hakuendelea maana bila shaka sasa angekuwa bingwa wa dunia. Zaidi ya yote anaaminika kuwa amehitimu mafunzo ya kikomandoo. Komputa ilizidi kuonesha kuwa Willy Gamba ana I.Q ya hali ya juu sana, hivi sasa ni mtu anayeweza kusokoraa matatizo yaliyojisokota sana. Na iliendelea kuonyesha kuwa ameifanyia 'OAU' kazi nzuri sana hasa kuhusiana na Ukombozi wa Afrika Kusini".

Alipofika hapa alinyamaza, kisha kama umeme alikatisha mazoezi yake na kunigeukia na kurukia kifuani pangu kwani bado nilikuwa nimesimama mlangoni nikisikiliza kwa makini.

"Kwanini usinieleeze toka mwanzo Willy mpenzi, kwanini?".

Nilimkumbatia kifuani kwangu na badaa ya kujibu swali lake nilisema. "Veronika Amadu".

Aliinua macho akaniangalia usoni, mimi bila kusita niliendelea. "Mwandishi maarufu wa gazeti la "Afrika", Veronika Amadu mwenye umri wa miaka ishirini na sita, mwenye urefu wa futi tano na inchi tano, mwenye macho na umbo la kupendeza la vipimo 38'-22'-36'. Alihitimu katika Chuo Kikuu cha Ibadani nchini Nigeria na kupata shahada katika uandishi, baada ya kuhitimu aiajiriwa na gazeti la 'Newsweek' la Marekani, akiwa mwandishi wao katika Afrika Magharibi. Kwa vile gazeti lilitaka kumtumia mwandishi huyu kupata habari zingine ambazo kuzipata kwake itabidi uhatarishe maisha yake, lililazimika kumpeleka Japan kujifunza namna ya kujikinga kwa mikono, hatari yoyote itokeapo, hivyo mwandishi huyu amehitimu katika Judo na Karate na kupata mkanda mweusi. Baada ya kuwa na gazeti hili kwa muda mrefu aliacha na kujiunga na gazeti a Afrika. Anajuikana kuwa msichana mwandishi jasiri sana, amewahi kusafiri na majeshi ya Chama cha wapigania uhuru wa Sahara Magharibi kiitwacho "The Popular Front for the Liberation of Saguiet el-Hamara na Rio de Oro" yaani "POLISARIO", katika mapambano yao dhidi ya majeshi ya Morocco ambayo yameshika sehemu hiyo, inasemekana mwandishi huyu alikaa na majeshi haya na kuandamana nayo katika uwanja wa mapambano kwa muda wa miezi sita na kuwa mwandishi wa kwanza kuandika habari kamili za mapambano haya akiwa shahidi wa macho. Je unasemaje Veronika Amadu".

"Sasa naamini kabisa wewe ndiye Willy Gamba, maana mimi nilifikiri tumekutangulia kumbe wewe ndiye umetutangulia zaidi. Naamini hata Sherriiff sasa umamfahamu kama nyuma ya kiganja chako hebu nieleeze".

Nilimweleza. "Ahmed Sherriff mwandishi mashuhuri wa gazeti la Afrika hasa juu ya mapambano ya Kusini mwa Afrika. Ahmed Sherriff mwenye umri wa miaka thelathini na mbili, mwenye urefu wa futi tano na inchi kumi na moja na mwenye masharafa mengi, alihitimu katika Chuo kikuu cha Patrick Lumumba mjini Moscow, Urusi. Baada ya kuhitimu kwake alipotea isijulikane aliko kwa muda wa mwaka mmoja. Lakini habari za kuaminika zinasema kwamba alikuwa akichukua mafunzo ya kijeshi katika kambi za kijeshi za Wapalestina huko Mashariki ya Kati. Baada ya kuonekana alipatiwa kazi moja kwa moja na gazeti la Afrika ambalo linaaminika lilipata fununu juu ya mafunzo ya kijeshi ya Sherriff huko Mashariki ya Kati. Kwani baada ya kumwajiri tu alipelekwa moja kwa moja Kusini mwa Afrika ambako aliandamana na majeshi ya wapigania uhuru wa Frelimo, MPLA na siku hizi anaandamana na majeshi ya SWAPO katika uwanja wa mapambano huko Namibia.

"Vile vile kuna habari zinazosema kuwa alikuwepo katika mkasa uliotokea Soweto na ndiye aliyeandika habari za kuaminika juu ya tukio hilo. Hivyo ujasiri wake huu umemfanya kuwa mwandishi maarufu sana anayechukiwa sana nan tawala dhalimu za Afrika Kusini na Rhodesia na nchi zote zinazopinga mapinduzi ya Afrika na harakati zake za kujikomboa kutokana na ubeberu. Umeridhika sasa."

"Sasa naamini ukiambiwa mtu ana I.Q ya hali ya juu, lazima utambue kuwa kwa kila jambo unalotaka kufanya yeye yuko hatua nyingi mbele yako", Veronika alijibu na kuanza kunibusu huku midomo yake ikiwa ya chumvi chumvi sababu ya mazoezi.

"Ngoja nioge mara moja ili tukaonane na Sherriff tukaanze mazungumzo yetu ya kwanza."

"Sawa". Aliniacha na kwenda maliwatoni. Mimi nikabaki katika mawazo makali jinsi ya kuanza kulishambulia tatizo hili.

Niiegesha gari langu kwenye maegesho ya Hoteli ya New Afrika. Nikatelemka na kuzunguka ili nimfungulie Veronika. Tuliingia New Afrika Hoteli katika sehemu iitwayo duka la Kahawa tukatafuta meza tukaa.

"Ulishastafutahi?", nilimuuliza Veronika.

"Kawaida yangu huwa ninastafutahi kabla ya kufanya mazoezi kila siku, ili kujiweka katika hali nzuri".

"Ndio sababu umbo lako linapendeza namna hiyo".

"Asante".

Mtumishi wa hoteli alifika na kutuuliza mahitaji yetu.

"Mimi nitakunywa maji ya machungwa kama yapo".Veronika alisema.

"Mimi niletee maji ya ndimu" niliagiza.

Alipoondoka mtumishi huyo nilimweleza Veronika kuwa mimi nitakwenda mapokezi kumwita Sherriff, ambaye niliamini alikuwa bado chumbani.

"Habari za leo Tom?", nilimsalimia kijana wa mapokezi ambaye tunafahamiana vizuri sana.

"Aha mzee, shikamoo", alinisalimia.

"Marahaba", nilimjibu.

"Sijui nikusaidie nini mzee?".

"Kuna mgeni wangu hapa anaitwa Ahmed Sherriff, alifika usiku".

"Ndio ndio, yuko yuko namba 406, unahitaji kwenda huko au nimpigie simu".

"Mpigie simu nizungumze nae".

Alimpigia simu na alipompata akanipa.

"Halo Sherriff habari za leo?".

"Ohoo, Willy salama?, nilikuwa ninakusubiri kwa hamu".

"Oke, telemka chini. Tuko hapa duka la kahawa pamoja na Veronika".

Oh, amekwisha wahi namna hii?".

"Sana tena".

"Oke nakuja sasa hivi".

"Haya tunakusubiri", nilimjibu na kukata simu.

"Oke Tom asante sana", nilimwambia kijana wa mapokezi.

"Asante mzee karibu", alijibu Tom.

"Asante niko hapa duka la kahawa".

Niliporudi nilikuta vinywaji tayari.

"Yupo?", aliuliza Veronika.

"Yupo, anakuja sasa hivi", nilimjibu.

Haukupita muda Sherriff alitokea na kuja moja kwa moja mezani kwetu.

Tulisalimiana akavuta

kiti na kuketi. Mtumishi aliyekuwa anatuhudumia alipomuona alikuja mara moja.

"Mzee nikusaidie nini?," alimuuliza Sherriff.

"Kuna maji ya nanasi?".

"Ndio, yapo".

"Haya niletee hayo, lakini weka barafu nyingi, maana si joto hili".

"Bila ya wasiwasi mzee".

Mtumishi alipoondoka tulikaa kimya tunatazamana kwanza kila mtu anashindwa kuanza mazungumzo. Veronika aipoona hivi akatabasamu kisha akasema. Sherriff wewe kidogo uko nyuma

ya habari, lakini nitakueleza kwa kifupi ili kukuweka pamoja nasi katika habari zinazotuhusu wote".

"Nitakushukuru", alijibu Sherriff.

"Willy nimemweleza yote tunayojua juu yake, na jambo la kushangaza ni kwamba na yeye anatufahamu sisi huenda kuliko tunavyojifahamu wenyewe".

"Usitie chumvi", nilimuasa.

"Ala!", Sherriff alitamka kwa mshangao mkubwa. "Kama ni hivyo basi ni vizuri sana. Kwani wote sasa tunafahamiana misimamo yetu. Unajua mimi nilishangaa sana usiku pale uwanja wa ndege. Waandishi wote wengine wa magazeti mbali mbali ulimwenguni tuliokuja nao wamekatajiwa kuingia hapa nchini, na tumewaacha uwanja wa ndege wakilalamika vibaya sana wakiomba kuonana

na mabalozi wao, lakini sisi tumeruhusiwa kwa urahisi sana, kitu hiki kilinishangaza sana nikahisi lazima huu utakuwa mpango wa Willy. Sasa nimeamini kabisa. Uongo au kweli".

Sherriff aliuliza huku akiniangalia.

"Bila shaka niliwaahidi toka tukiwa Freetown kuwa mnakaribishwa kwa dhati Tanzania, sasa nimetimiza ahadi yangu".

"Asante sasa", Sherriff alijibu.

"Mimi naamini unajua tumekuja kwa ajili gani, na vile vile naamini likizo yako imekatishwa kwa ajili sababu hiyo hiyo tuliyoijia sisi", Veronika aieleza huku macho yake yaking'aa kuonesha kuwa sasa tulikuwa tunazungumza kikazi.

"Sawa, endelea", nilimjibu.

"Mimi naonelea tungeliungana na wewe, kwani wewe ukiwa mwenyeji itakuwa kazi rahisi kwetu kuweza kupata habari. Sijui wewe unaonaje?".

"Kwa taarifa yenu lazima niwaeleze kuwa tukio hili lililotokea si la kawaida. Mnaweza kuwa mmeshiriki katika mambo ya hatari sana kama vile mambo ya vita, lakini lazima niwatahadharishe kuwa kutafuta habari za aina yoyote zinazoweza kufichua kundi lililofanya ujahiri wa hari ya juu ni hatari sana kwa maisha yenu kuliko hatari yoyote mliyokwisaha kuikabiri. Nadhani mmenielewa. Ningewaomba ili kuponya maisha yenu muwe watoto wazuri, muachane kabisa na kuuliza uliza habari za tukio hili".

"Kabla hatujatoka ofisini kwetu London, tumetahadharishwa kama unavyotutahadharisha sasa, lakini tulikaa tukaamua kuwa tutaendelea; Lolote baya litakalotupata tutakuwa tumetoa damu yetu kwa ajili ya ndugu zetu. Kwani sisi tunaamini watu waliofanya kitendo hiki si watu wengine bali ni mabeberu wapinga ukomboni wa kusini mwa Afrika", alijibu Sherriff kwa nia moja.

"Kama uamuzi wenu ni huo basi tutashirikiana kwa kadiri tutakavyoweza".

"Mlikuwa na nia ya kuanza kutafuta habari tokea lini?".

"Tokea sasa hivi kama unaweza kutupa fununu tuanzie wapi!", Sherriff alijibu.

Kwa vile katika mpango wangu wa upelelezi nilikuwa nimepanga kuwatumia ndugu hawa. Niifurahi sana kuona kuwa mambo yaikuwa yanakwenda kama nilivyopanga. Hivyo niliamua kuwaeleza kwa

kirefu maelezo aliyokuwa amenieleza Chifu.

"Ili kuwaweka sawasawa ninyi katika picha ya tukio hili mtakuwa wageni wa kampuni yangu. Kwa

hiyo mimi naona tangia sasa nitakuwa ni wakala wa gazeti lenu, kwa kufanya hivi nitapata kisingizio cha kutembea na kupeleleza na nyinyi mkiwa kama wateja wangu; nafikiri mmenielewa?".

Wote walitingisha vichwa kuonesha kuwa wamenielewa. Kutokana na mipango yangu ilivyokuwa nilionelea tokea wakati huo tuanze kazi bila kupoteza muda.

Nilitoa onyo tena "Kukubali kwenu kushiriki na mimi katika upelelezi wa tukio hili mjue kabisa mmejiwekea sahihi ya kifo. Natoa natoa muda wa mwisho kama kuna mtu anaona wasiwasi katika moyo wake nampa nafasi aache shughuli hii", niliwaasa na kuwaangalia kwa makini sana.

Mwisho Veronika akasema

"Unajuwa Willy dakika ile mtu anapozaliwa pale pale anapewa huku ya kifo. Nina maana ya kusema kuwa binadamu hata aishi vipi kufa lazima atakufa. Kule kuishi baada ya kuzaliwa ina maana kuwa ile hukumu ya kifo inaahirishwa kutekelezwa.

"Unajuwa Willy dakika ile mtu anapozaliwa pale pale anapewa huku ya kifo. Nina maana ya kusema kuwa binadamu hata aishi vipi kufa lazima atakufa. Kule kuishi baada ya kuzaliwa ina maana kuwa ile hukumu ya kifo inaahirishwa kutekelezwa. Wengine huahirishwa kwa mwezi mmoja. Hivyo mtoto anazaliwa na baada ya mwezi mmoja anakufa. Hii si ajabu maana hukumu yake ya kifo imetekelezwa baada ya mwezi mmoja. Wengine huishi hata miaka mia moja. Hii ina maana kuwa hukumu yake aliyopewa dakika alipozaliwa imetekelezwa baada ya miaka mia. Hivyo kila mtu na sehemu yake ya kuishi. Kwa hiyo kuogopa kufa ni ujinga."

"Mimi sina wasiwasi, maana kifo cha namna hii, nitakuwa nimekufa kifo cha heshima", alisema

Sherriff.

"Okke, sasa naamini nina watu. Tokea sasa nyinyi si ndugu tena ila ni makomredi", niliwaeleza.

"Kwani komredi ina maana kubwa zaidi ya ndugu?", Veronika aliuliza.

"Hasa, ina maana kali zaidi. Komredi ina maana mwenzi katika harakati".

"Asante komredi Willy, naona tunywe maji haya katika jina la komredi", Veronika aliomba. Wote tukagonganisha glasi zetu.

"Sasa mimi naonelea itabidi tuanze upelelezi wetu bandarini. Itabidi tukamuone ofisa aliyehusina ili na sisi tupate habari toka kwake ana kwa ana ingawaje atakuwa amekwisha sumbuliwa sana na polisi na maafisa usalama kwa maswali. Huenda sisi tukapata jambo ambalo huenda wao wameliruka. Halafu tukaendelea hivyo hivyo katika ofisi zote zilizohusika kabla hatujachukua hatua kali zaidi", mnaonaje.

"Sawa", walijibu kwa pamoja.

Tulinyanyuka na kuelekea kwenye gari langu, nikawafungulia milango. Veronika alikaa mbele na mimi. Sherriff akakaa nyuma. Nilipotaka kuwasha gari moto niliona kijikaratasi chini, nikakiokota taratibu nikakisoma. Eddy alikuwa ameniandikia namba zote za magari aliyokodi.

Akionesha namba za magari aliyoacha kwenye maegesho ya New Afrika na Kilimanjaro Hoteli kama nilivyokuwa nimeamru. Nilianza kusikia msisimko wa damu ikionyesha kuwa kazi imeanza. Nilipiga gari moto tukaelekea bandarini.

SURA YA NNE

"**SAMAHANI** binti tunaomba kumuona Meneja", nilimwambia mwandishi mahsusi wa Meneja wa Bandari.

"Sijui nyinyi ni akina nani?", aliuliza msichana huyu aliyeonekana amechoka choka.

"Mwambie ni Willy Gamba na wateja wake kutoka gazeti la Afrika".

Meneja wa Bandari tulikuwa tunafahamiana kikazi, hasa kutokana na shughuli zingine tulizokuwa tunazifanya katika kampuni yetu ya Afrika International Agencies.

Yule msichana alizungumza na bosi wake kwa simu, alipomaliza alinyanyuka na kutufungulia mlango tukaingia ndani. Tulimkuta Issack Mlingi ambaye ndiye Meneja wa Bandari aliyehusika na tukio hili akionyesha hali ya kuchoka sana. Nafikiri hii ilitokana na bughudha alizopata toka kwa polisi na watu wengine wanaohusika na upelelezi wa tukio hili. Macho yake yalikuwa mekundu na yamevimba.

"Karibuni ndani", alisema huku akinyanyuka ili tusalimiane.

"Samahani ndugu Mlingi, naamini una shughuli nyingi sana", nilimuomba radhi.

"Si kitu Gamba, karibuni".

"Hawa ni wateja wangu Sherriff na Veronika kutoka gazeti la Afrika ambalo kampuni yangu ni wakala wake, na jamani huyu ni Issack Mlingi, Meneja wa Bandari", walipeana mikono kisha wote tukavuta viti tukakaa.

"Ndugu Mlingi ni imani yangu kuwa umeisha ulizwa maswali mengi juu ya tukio hili lililotokea

hapa bandarini. Lakini naamini hatutakuwa tumekuhangaisha kama tutakuuliza maswali. Kama nilivyokwisha kwambia hawa waandishi wa gazeti la Afrika na ni waandishi pekee walioruhusiwa kuingia hapa nchini kuandika juu ya tukio hili, naamini unajua msimamo wa gazeti la Afrika.

Hata hivyo tutakuuliza maswali kidogo tu kusudi tusikuchoshe sana".

"Hebu nipeni vitambulisho vyenu niviangalie", aliomba.

Sherriff na Veronika walimpa vitambulisho, akaviangalia na aliporidhika akavirudisha.

"Haya ulizeni maswali yenu, maana ikiendelea hivi naweza kupata wazimu", alisema huku akitoa tabasamu la uchovu.

"Tumesoma maelezo yako uliyotoa polisi, ila tumekuja hapa kukuuliza maswali machache juu ya mambo ambayo hatukuwa tumeyaelewa vizuri", alisema Sherriff.

"Ulieleza kuwa ulipata simu kutoka kwa Jones Mantare ambaye umezoea sana sauti yake, kiasi kwamba huwezi kuikosea ukiisikia. Lakini jambo la kushangaza ni kwamba, Mantare anasema hakuwa amekupigia simu kwani alikuwa na mkutano na Mwenyekiti wa Kamati na Mwenyekiti amethibitisha kuwa ni kweli walikuwa wote toka saa tisa hadi saa kumi na moja. Baada ya kupata maelezo hayo bado unaweza kusema kuwa sauti ile ni sawa kabisa na ya Mantare?"

"Kwa sababu wakati ule nilikuwa sina wasiwasi kuwa kuna jambo baya roho yangu iliridhika kuwa ni Mantare. Lakini sasa kwa sababu Mantare anasema hakupiga simu, ndipo nakumbuka kuwa nilimwuliza kama ana mafua, maana kwa mbali alikuwa akizungumzia puani, na yeye alijibu kweli mafua yalikuwa yamemkaba sana. Lakini maelezo mengine, mathalani ambayo huwa tunataniana na Jonas, yalikuwa yote sawa. Kusema kweli inawezekana kabisa alikuwa mtu mwingine anayemfahamu sana, lazima niseme sana maana isingekuwa hili jambo la mafua bado ningeendelea kung'ang'ania alikuwa Jones. Lakini Jones amekuja hapa hana mafua hata kidogo kwa siku nyingi".

"Hebu fikiria tena kidogo juu ya sura na sauti au umbile na tabia ya huyu mtu aliyekuwa akijiita Meja Paul Liboi, unaweza kuwa na uhakika kabisa kuwa mtu huyu ni mzalendo wa Tanzania?", Veronika aliuliza.

Ndugu Mlingi alisita kidogo kujibu swali hili na uso wake ukakunjamana kidogo. Baada ya kufikiri sana akasema.

"Nafikiri anaweza asiwe mzalendo".

Wote tukamwangelia.

"Kwanini unafikiri hivyo?", mimi nilimuuliza.

"Wazo hili lilikuwa halijaingia kichwani mwangu, lakini sasa baada ya kuuliza swali hili inawezekana mtu huyu asiwe mtanzania maana kwanza kiswahili chake hakikuwa kimenyooka na alipenda sana kuchanganya na kiingereza. Mimi

nilimfikiria kuwa huenda ni Mjaruo, lakini alikuwa hajang'oa meno. Vile vile alikuwa na haraka haraka na maneno ya mkato mkato. Nikifiri sana hakuna na ile hali ya kirafiki waliyonayo watanzania wengine wengi. Lakini kwa sababu nilijuwa ni mwanajeshi nikafikiri ndio sababu aikuwa na tabia ya namna hiyo".

"Una jambo jingine ambalo huenda sasa unafikiri halikuwa lakawaida juu ya tukio lolote baada ya kujuwa watu hawa walikuwa majahiri?".

"Nafikiri nimeshasema yote, ila tu huenda kitu kimoja, sijui kama kinahusika ama vipi".

"Ehe, kitu gani".

"Baada ya kuzungumza na huyo anayejiita Jones Mantare, simu za jengo hili hazikufanya kazi tena. Tulipowaeleza Posta kesho yake, walikuja mafundi na kusema waya inayounganisha jengo hili na waya zinazokwenda Posta ilikuwa imekatika kwa kuangukiwa na mti. Sasa nilianza kuona picha kidogo ya tukio hili. Nilijua mara moja kuwa watu waliokuwa wameshughulikia tukio hili ni watu wenye kujua ujasusi wa hali ya juu; kwani walihakikisha kuwa kila hatua wanayoichukua na nyayo zake wanazifuta ili asiwepo mtu wa kuzifuatia".

Tulijikuta tumeridhishwa sana na safari yetu ya bandarini hivyo tukaona tuondoke.

"Asante sana ndugu Mlingi, kama tukihitaji mambo zaidi tutakuona tena, na kama utakumbuka kitu cochote kinachoweza kutusaidia nipigie simu. Nafikiri simu yangu unayo?", nilimuuliza.

"Ndio ninayo", alijibu.

"Na tahadhali usizungumze ovyo juu ya tukio hili, maana si tukio zuri", nilimwonya.

"Bila shaka nitajitahidi".

Tuliagana nae, tukaondoka kuelekea mjini.

Nilijaribu nilivyoweza kuangalia kama naweza kumwona Eddy na mwenzake, lakini wapi hakika vijana walikuwa wanafanya kazi nzuri sana, maana kama mimi Willy sikuweza kuwatambua basi hakuna mtu mwingine tena, si kama najisifu ila huo ndio ukweli, mtu akitaka kunitafuta mimi basi ajiweke sawa, la sivyo shauri lake.

"Kamara kama ulivyomjua alikuwa mtu wa namna gani, unafiri anaweza kwa njia yoyote akawa kajiingiza katika jambo hili?", nilimuuliza Sherriff huku tukiwa tumesimama kungojea kuingia barabara ya site drive, tukutokea bandarini.

"Mimi nakuhakikishia komredi kuwa Kamara alikuwa hawezi kufanya jambo kama hilo, ni lazima tu iko namna ambayo alishambuliwa na kunyang'anywa karatasi hizo, alinihakikishia Sherriff.

"Oke, naona sasa twende kwenye ofisi ya kamati ya Ukombozi ya OAU", nilimweleza huku nageuza gari kuingia site drive na kuelekea kwenye ofisi ya kamati.

Tulipofika kwenye mapokezi ya ofisi hii ya kamati na kumkuta msichana mmoja akizungumza kwenye simu, ikatubidi tumsabiri kidogo amalize kuzungumza, niliangalia saa yangu ilikuwa yapata saa sita na dakika tano.

"Samani jamani, sijui niwasaidie nini", msichana alituuliza.

"Bila samahani binti, sisi tunaomba kumwona Jones Mantare", nilijibu.

"Mna ahadi naye?", binti aliuliza.

"Hapa, lakini nafikiri ukimwambia Willy Gamba wa AIA na wageni toka gazeti la Afrika, ambao wanataka kumwona, anaweza kutuona", nilimweleza.

"Msubiri basi", huyo msichana alijibu kisha akainua simu na kuanza kuzungumza na ofisi ya Mantare. Jones Mantare alikuwa ananifahamu, maana nilikuwa nimehakikisha kuwa nafahamiana karibu na kila mtu katika ofisi hii ya kamati, yeye alikuwa akinifahamu kama mfanyabiashara, maana ndivyo nilivyojulishwa kwake. Tokea hapo tulikuwa tunaonana mara kwa mara sehemu za starehe na kujenga uelewano wa kutosha, hivyo nilihisi kuwa asingeweza kunikatalia nisimuone, ingawa nilijuwa atakuwa katika hali isiyokuwa ya kawaida. Baada ya kuzungumza kwa muda kwenye simu msichana alitwambia.

"Mnaweza kwenda kumwona, ofisi yake ipo mwisho wa ujia mkono wa kulia".

"Asante sana binti", nilimjibu.

Tulimwacha tukaelekea alikotuelekeza. Tulibisha mlango pale tulipokuwa tumeelekezwa.

"Karibu", tulisikia sauti ya msichana ikitoka ndani. Nilifungua mlango tukaingia na tujikuta katika ofisi kubwa ya mwandishi mahsusi wa Mantare.

"Habari zako bibie", nilimsalimia kwa niaba ya mwenzangu.

"Nzuri, ni Gamba na wenzake nafikiri?", aliuliza.

"Hasa", nilijibu.

"Ingieni moja kwa moja anawasubiri", alisema huku akisimama na kutufungulia mlango wa bosi wake. Tulipoingia tu Mantare alisimama.

"Ahaa ndugu Willy, karibuni".

"Asante, asante Jones".

"Nafikiri niwajulishe, huyu ni ndugu Jones Mantare, ofisa katika kamati hii ya ukombozi, na hawa ni komredi Ahmed Sherriff na komredi Veronika Amadu. Ni waandishi wa habari wa gazeti la "AFRIKA".

Walipeana mikono kwa mara nyingine.

"Ehe, mlitaka kuniona, sijui niwasaidie nini?", aliuliza.

"Hawa makomredi ni wateja wangu, kampuni yangu ndio wakala wa gazeti la Afrika hapa nchini. Hasa kitu kilichotueta hapa ni kutokana na tukio hili la juzi. Nafikiri unaelewa msimamo wa gazeti la Afrika katika ukombozi, na kutokana na msimamo huo wameiomba serikali kama wanaweza kuandika habari za kuaminika juu ya tukio hili. Ni wasiwasi wao kuwa magazeti mengi ya kibeberu yataandika habari za kupotosha, na wao wako hapa ili waweze kueleza jumuiya ya ulimwengu ukweli mtupu. Kwa hiyo tutashukuru sana ukiweza kutusaidia katika kujibu maswali machache. Hatutataka kupoteza muda wako kutueleza mengi, maana nakala ya maelezo yako tumeipata toka polisi. Hivi ni nia yetu uweze kutufafanulia katika sehemu ambazo hazieleweki katika tukio hili".

Niliona kule kutaja nakala ya maelezo yake kutoka polisi kulimtoa wasiwasi aliokuwa ameuonyesha usoni mwake. Niliona macho ya Veronika yakiwaka kuonyesha kuwa nilivyoeleza nimeeleza vizuri sana na Sherriff alitingisha kichwa kuonyesha kuwa niliyoyasema ni sawa kabisa.

"Sawa ndugu Willy, nitakuwa tayari kuwajibu mwaswali yenu, kusema kweli kama ulivyosema, radio za kibeberu zimekwisha tangaza uongo ili kuridhisha maslahi yao. Kwa jinsi hii tutakuwa radhi kuona ukweli unaandikwa na gazeti hili. Haya sijui mna maswali gani?".

"Inasemekana kuwa hayati Kamara Franki ndiye alikuwa anashughulikia suala hili la silaha. Na amekutwa ameuawa. Nafikiria hizi karatasi zilitokatokaje mikononi mwa marehemu na kuingia mikononi mwa hawa majahiri?. Maana kutokana na maelezo ya Polisi ofisi yenu hii haikuvunjwa mahali popote", Sherrieff aliuliza.

"Sawa kabisa?, kutokana na maelezo ya mwandishi mahsusi wa marehemu, anasema ya kwamba?, wakati marehemu anatoka ofisini alimweleza aweke zile karatasi za kuchukulia silaha ndani ya mkoba wake, kwa sababu alikuwa anategemea kwenda kwenye kikosi cha Jeshi kinachoshughulikia silaha za wapigania uhuru kesho yake, kabla hajaja ofisini. Kwa hiyo, jibu kwa swali lako ni kwamba watu hawa walimnyang'anya marehemu karatasi hizo na ndio sababu wamemuua."

"Watu hawa unafikiri walijua kuwa marehemu atakuwa na karatasi hizi ndani ya mkoba wake?", Veronika aliuliza.

"Hapo ndipo hata sisi tumekwama".

"Huyu mwandishi mahsusi wa marehemu yupo", nilimuuliza.

"Ndio yupo".

"Unaweza kumwita tukazungumza nae kidogo?".

"Hali yake si nzuri sana, bado ana mshituko kwa ajili ya marehemu. Unajua mnapofanya kazi kwa uhusiano ulio karibu na mtu mnakuwa na urafiki wa hali ya juu sana. Hata hivyo nitajaribu kuwaitieni".

Alishika simu na kuzungumza na mwandishi wake. Wakati tukimsubiri Veronika alimuuliza tena. "Ofisa wa kule bandarini Ndugu Mlingi anasema mtu aliyempigia simu alikuwa na sauti kama yako, mathalani mambo mnayotania yalikuwa vile vile, unaweza kufikiri mtu yeyote hapa ofisini au hata nje anayeweza kuigiza sauti yako kiasi hicho?".

"Ni imani yangu kuwa mtu kukuigiza kiasi hicho lazima awe mtu aliyekuzoea, na mtu aliyekusikia ukizungumza mara kwa mara, hasa na huyu ndugu Mlingi".

"Kuesema kweli, nimefikiria kweli juu ya mtu huyu mpaka nimechoka, nitazidi kumfikiria kama wazo likinijia nitakupigia simu."

Mara mlango ulifunguliwa akaingia msichana mrefu mwembamba mwenye nywele nyingi. Kama unapenda wasichana warefu na wembamba, basi hapa pana msichana wa namna hiyo, jina lake Margreth. Ni mzuri kiasi chake.

"Karibu Margreth", Mantare alimkaribisha, wote tukasimama akatujulisha kwake. Mwandishi mahsusi alileta kiti kingine na Margreth akaketi.

"Samahani Margreth", hawa ndugu wana maswali kidogo ya kukuuliza," Mantare alimwambia.

Margreth hakujibu kiti bali alituangalia tu.

"Samahani sana binti, sisi wote yunaelewa hali uliyonayo, ila imetubidi tukuone tuweze kuzungumza nawe huenda utatusaidia kutatua huu mkasa uliompata bosu wako", nilimwelezea.

"Niko tayari kuwaelezea chochote kama kitasidia kuwapata watu waliomuua bosu wangu." Margreth alijibu huku machozi yakimlengalenga.

"Jaribu kukumbuka, nilimwambia, "wakati marehemu anakueleza uweke zile karatasi za kuchukulia silaha kulikuwa na mtu mwingine yeyote?".

Alikaa kimya kwa muda kisha akajibu, "Hapana", harafu kama amegutuka akasema, "Ndio nakumbuka sasa, alikuwepo tarishi wetu wa hapa ofisini".

Nikasikia kengere ya tahadhari inalia kichwani mwangu. Wote tulitazamana.

"Tarishi huyu yuko hapa?", niliuliza.

"Hapana, ni mgonjwa anaumwa na ameandikiwa kulala siku tano", Margreth alijibu.

"Toka lini?".

"Toka tarehe nne".

"Yaani siku ambayo ilibainika kuwa silaha zimeibiwa na bosu wako ameuawa?".

"Ndio".

"Yaani atakuwa kazini tarehe tisa".

"Ndio".

"Una uhakika kabisa alikuwepo?".

"Ndio".

Habari kama hizi mimi ndizo huwa zinanitibua, maana wakati kifo kinatokea haafu kinatokea kitu kingine chenye uhusiano wa karibu namna hii, basi hapo ndipo huwa naanza kujumulisha moja kwa moja na kupata mbili.

Nilimgeukia Mantare na kumwuliza, "Huyu tarishi ndiye alikuwa tarishi wa ofisi nzima?".

"Ndio".

"Anaitwa nani?".

"Anaitwa George Kiki".

"Mmekuwa naye muda gari?".

"Yapata miezi sita sasa".

"Ni MTANZANIA!".

"Hapana ni mkimbizi kutoka Afrika Kusini, aliletwa kwenye ofisi yetu na chama cha wapigania uhuru cha Afrika Kusini kilichopo hapa mjini cha SANP. Ili tumsaidie. Alipokuja hapa alitupa maelezo yake na kuonekana ni kati ya vijana walioanzisha maandamano ya kitongoji cha Soweto huko Afrika Kusini. Alieleza kuwa yeye alipata mwanya wa kutoroka gerezani ndipo akakimbia na kuweza kufika hapa baada ya safari ndefu ya taabu. Kwa vile alikuwa hana kisomo cha kutosha jinsi yeye alivyojieleza tuliamua kumpa kazi ya utarishi ili kumsaidia. Kusema kweli amekuwa kijana mwenye bidii sana, na anapendwa na kila mfanyakazi wa hapa, hasa kwa nidhamu yake, na utekelezaji wa kazi yake".

"Kwa hivi alikuwa na fursa ya kuingia ndani ya ofisi ya mtu yeyote wakati waowote ili kuchukua mafaili na mambo kama hayo?".

"Hasa ndivyo ilivyokuwa".

"Anaishi wapi?".

"Anaishi huko Kinondoni sehemu za Hananasifu Estate katika nyumba za shirika la nyumba".

"Nyumba yenyewe unaijuwa?".

"Mimi nimewahi kufika kwake; tumewahi kumpeleka na marehemu", alisema Margret huku tena machozi yakimlengalenga.

"Samahani Mantare, sijui unaweza kumruhusu Margret akatuelekeza kwa Ndugu Kiki?".

"Bila wasiwasi mnaweza kwenda nae".

Niliwaangalia wenzangu nikaona wameridhika na maswali na majibu ya hapa, hivyo kwa niaba yao nikamshukuru ndugu Mantare.

"Ikiwa tutahitaji jambo lolote tutarudi tena au tutapiga simu. Na wewe ukipata jambo lolote usisite kutufahamisha".

"Hamna tabu, nitafurahi kuwasaidia".

Tuliagana tukaondoka kuelekea Kinondoni.

"Mimi naona tukapate chakula cha mchana kwanza", Sherriff alishauri.

"Sawa", walijibu kwa pamoja. Sherriff alikaa nyuma pamoja na Margret na wakati huo mimi naendesha nikiwa katika mafikara mengi, Sherriff alichukua jukumu la kumtuliza Margret akimweleza mambo mengi juu ya matatizo ya binadamu na kumwambia kuwa asihuzunike sana maana ndiyo binadamu. Kadiri Sherriff alivyozidi kusema ndivyo Margret uso wake ulizidi kutokwa na huzuni kwani mimi nilikuwa nawaangalia katika kioo cha kuendeshea. Hata Sherriff alipofika kusema yeye huwa anaamini kuwa kwa kila linalotendeka linatendeka kwa ajili ya uzuri, nilimwona Margret anamwemwesa kwa mara ya kwanza, na ndipo sura yake ilionyesha uzuri aliokuwa nao. Niliona hata Sherriff aligundua uzuri huo, kwani uso wake ulibadilika kiasi cha kwamba moyo wake uliguswa.

SURA YA TANO

TULIFIKA New Afrika Hoteli, nikaegesha gari wote tukatoka nje. Basi, moja kwa moja tulifuliza kwenda kwenye lifti ya kutupeleka orofa ya kwanza ambapo ndipo Bandari Grill ilipo. Mbele yangu nilimwona Eddy anavuka sehemu ya mapokezi, halafu akazungusha kichwa akaingia kwenye choo kilichopo hapa chini. Hii ilikuwa ishara kuwa alitaka kuniona.

"Samahani jamani nasikia nimebanwa haja ndogo, tangulieni nakuja sasa hivi. Margret, we ndiye mwenyeji washughulikie wagaeni".

"Bila wasiwasi", alijibu akiwa anaanza kupona kutoka katika mshituko alioupata. Niliingia maliwatoni nikamkuta Eddy ananisubiri.

"Mpaka dakika hii hakuna chochote", aliniambia bila kuniangalia.

"Sawa, nendeni mkale halafu nenda ofisini nitakukuta huko kiasi cha saa kumi hivi".

"Oke", alisema huku akielekea kwenye mlango wa kutokea.

Mimi nilimaliza haja yangu ya uongo na kweli nikaondoka kujiunga na wenzangu. Tulipata muro safi sana hapa Bandari Grill, na kwa sababu kila mtu alikuwa na njaa tulikula kimya kimya.

"Nasikia kichwa kinaniuma", Veronika alilalamika.

"Nafikiri kwa ajili ya hali ya hewa. Joto jingi sana kuliko ulilozoea", nilimjibu.

"Kama ni hivyo afadhali ukameze dawa upumzike, sisi tutakwenda kumwona Kiki halafu tutakuja kukuona", Sherriff alishauri.

"Naona hivyo ni sawa", alijibu.

Basi tulikubaliana Veronika apumzike sisi tuendeleo na shughuli. Tuliondoka New Afrika na kumtelemsha Veronika Kilimanajaro.

"Vero mpenzi, kuna gari lile pale unaweza kulitumia wakati wowote. swichi iko chini ya zulia", nilimuonyesha gari ambalo Eddy alikuwa ameliacha hapo. Sisi tuliondoka na kuendelea na safari yetu ya Kinondoni.

"Twende kupitia barabara ya Upanga moja kwa moja, halafu tukivuka Salendar brijji mbele kuna barabara ya Kinondoni hivyo tutaingia kushoto. Sehemu iko mbele ya makaburi. Baada ya makaburi kuna barabara la vumbi, linakatisha barabara hii. Tukiacha hilo na kuendelea mbele tukakuta barabara nyingine ya vumbi inaingia kushoto na kuna kibao kimeandikwa Bamboo Baa and Restauranti, basi hapo ndipo tutakapoingia", alieleza Margret kwa ufasaha kabisa.

Mimi hupenda maelezo ya namna hii, siyo mtu amefika mahali pa kukata kona ndipo anasema, kata hapa kushoto. Maelekezo hayo ni ya kihuni na ndiyo anayosababisha ajali nyingi.

Nilifuata maelezo ya Margret vizuri kabisa, nilipotaka kuingia kushoto pale kwenye bao la tangazo la Bamboo Baa and Restauranti, Margret alisema, 'Njia hapa si nzuri twende pole pole, halafu mbele kidogo utakata kushoto tena tuelekee kwenye nyumba hizo pale', alinielekeza na kuonyesha kwa kidole.

Niliendesha pole pole nikaikuta njia na kuifuata kuelekea kwenye nyumba hizi za shirika la nyumba.

"Baada ya nyumba hiyo yenye bendera ya CCM, ambayo ndiyo ya mjumbe, ya pili yake".

"Hapa?".

"Ndio, mlango huu huu".

Nyumba hizi zinakaa familia mbili mbili, lakini zimetengwa katikati kiasi kwamba kila familia ina sehemu yake kamili. Tulitoka ndani ya gari, Margret akatangulia na kibisha hodi. Lakini hatukupata jibu. Nilisikia moyo wangu unapiga haraka haraka, hii ni sirika niliyojaliwa nayo, na ilikuwa ni ishara kuwa kuna hatari.

"Hebu ngoja Margret", nilimwambia nikimrudisha nyuma.

Niliujaribu mlango ukafunguka nikamwita Sherriff na kumwambia hakuna mtu, tulifungua mlango mwingine uliokuwa unaelekea jikoni, bafuni na chumba cha kulala. Tukiwa wote na wasiwasi tukibisha hodi kwenye mlango wa chumba cha kulala. Lakini hatukupata jibu. Nilitoa Bastola yangu, na kusukuma mlango wazi.

Tulimkuta mtu ambaye tuliamini ni Kiki amechomwa kisu kifuani!, nilipomshika nikajua alikuwa amekwisha kufa saa nyingi sana. Kisu kilikuwa kimeachwa pale kifuani. Kilikuwa kisu kikubwa na mpini wake mwekundu. Tulimwita Margret aje atuhakikishie.

Akiwa anatetemeka kwa woga alikuja na kusema, "Ndiye yeye masikini", akaanza kulia tena tulimbembeleza na kumvuta na kuondoka haraka haraka ndani ya nyumba hiyo. Tuliingia katika gari langu na kuelekea mjini. Sasa nilianza kuongeza hesabu kwamba mbili na mbili na kupata nne. Na vile vile majahiri hawa walianza kunitisha kwani mbinu zao zilikuwa kubwa. Lakini hata hivyo mbinu za Willy ni kubwa zaidi.

"Mapambano yameanza Sherriff", nilisema kwa sauti ambayo sikuamini ilikuwa yangu.

"Na kweli yameanza", Sherriff alijibu.

Wakati huo tulikuwa tumesimama kwenye taa za usalama barabarani za salendar briji tukuelekea New Afrika. Saa yangu ilisema ni saa kumi na dakika mbili.

"Naona mimi mnifikishe nyumbani", Margret aliomba.

"Unakaa wapi".

"Ninakaa kwenye orofa pale nyuma ya Rex Hoteli".

"Nazijua orofa hizo, uko orofa ya ngapi, maana tunaweza kukuhitaji ama kikazi ama katika hali ya kustarehe, unasemaje?".

"Karibu mimi niko orofa ya pili chumba namba kumi na nane. Simu yangu ni 22221".

Basi wakati huo tulikuwa tumefika Posta ya Azikiwe, tulipofika kwenye sanamu ya Bisimini, tukaingia Independent Evenue.

"Unajua", Margret alitugutusha.

"Ehee", nilijibu na kumwangalia ndani ya kioo cha kuendeshea, maana yeye alikuwa amekaa nyuma.

"Sijui ni mafikara yangu, ila tu limekuja kama wazo la kunishangaza, maana baada ya kutokea mambo haya kila kitu nakiona si cha kawaida kinanigutusha".

"Nini kimekugutuusha?", Sherriff aliuliza akionesha msisimko.

"Unajua pale kwenye lango la kuingia ndani ya ofisi yetu kumekuwa na mwendawazimu ambaye amekaa pale zaidi ya mwezi mzima. Amekuwa amevaa matambalatambala tu na amebeba makopo mengi, sijui mmemuona?".

"Mimi nilimwona", Sherriff alijibu.

"Mimi sikumwona".

"Polisi walikuja kumchukua siku moja, na kumpeleka kunakohusika lakini hazikupita saa tatu akarudi. Alikuwa hatoki pale hata dakika moja, usiku na mchana kutokana na walinzi wa usiku wanavyosema. Leo mlipokuja alikuwepo maana mimi niliona gari lenu linaingia wakati natoka kunywa chai. Gari lenu lilipoingia na yeye alivuka lango akaingia ndani. Hii ni kawaida yake, kwani huwa anaombaomba kwa kila mgeni anayefika pale ofisini na ndio sababu aliitiwa polisi kwa sababu anawafadhaisha wageni wetu. Gari lenu mliliegesha mbele kabisa ya mlango wa kuingia mapokezi na kutoka ndani ya gari haraka hivyo hakuwahi. Mimi nilipoingia pale mapokezi nilikuta nyinyi mmekwisha kwenda ofisini kwa Mantare ila nilimkuta yule kichaa anamuuliza yule msichana wa mapokezi. Hawa watu wanasema wanatoka katika gazeti la Afrika. Yule msichana wa mapokezi alikasirika na kumfokea, Toka hapa! kama wanatoka gazeti la Afrika watakufaa nini wewe?, wana kazi ya maana kuliko kuonana na mwendawazimu kama wewe. Toka!".

"Kitu cha kushangaza ni kwamba wakati tunaondoka pale ofisini kwetu nakumbuka sikumuona wala makopo yake na kilago chake hakikuwepo, sijui jambo hili lina maana yoyote au mnaonaje nyinyi wenyewe?", alimalizia Margret.

"Unasema alikuja hajawahi kutoka pale hata dakika moja, ila tu siku ile aliyochukuliwa na polisi kwa muda wa masaa matatu?", nilimuuliza.

"Nina uhakika kabisa maana mimi damu yangu ilikuwa haipatani na yule mtu kabisa, na ni mimi niliyefanya kampeni ya kumuitia polisi lakini aliporudi alionekana kuwa maafisa wote walidharau kumchukulia hatua tena".

"Ukimwangu alikuwa anaonekana kichaa au unafikiri anajifanya tu?", nilimuuliza.

"Kitu kilichonikosanisha naye ni kwa sababu siku moja aliniambia yeye si kichaa ila anajifanya tu ili kujipatia pesa bila jasho. maana ilikuwa ukimwangu sana wakati yeye hana habari anakuwa kama si mtu kichaa, ila huwa anapoona watu anakuwa kichaa kabisa".

"Asante sana, kumbuka jambo hili linaweza likawa na msingi tutaliangualia".

"Asante".

Niliegesha gari mbele ya Rex Hoteli.

"Wakati wowote tutegemee", nilimweleza huku akitelemka.

"Mnakaribishwa", akiwa zaidi anamwangalia Sherriff. Sherriff alitoa mkono wake wakapeana mikono. Tayari kulikuwa na kitu kinapita kati yao, maana nyuso zilikuwa wakati wanapeana mikono, mimi ndiye najua, maana hata mimi hali hii inanitokea. Walikuwa wameanguka katika penzi.

"Mimi naona turudi pale ofisi ya kamati tukahakikishe kama kweli hayupo pale yule kichaa", nikimwambia Sherriff.

"Sawa".

Tulikwenda kimya kimya kila mtu akichambua mambo, tuliyokuwa tumeyapata na kuyaona, tulipofika pale ofisini tulimkuta mlinzi wa jioni anayeingia kazini saa tisa wanapofunga kazi mpaka saa kumi na mbili asubuhi, ilionekana alikuwa anafanyakazi masaa mengi sana, lakini yeye alipenda kazi yake na kuridhika na kipato alichokuwa anakipata, baada ya kutusalimia na kutueleza hizo saa zake za kazi, nilimuuliza.

"Unajua kulikuwa na mzee mmoja kichaa hapa sijui amehamia wapi?".

"Hata mimi nashangaa, kichaa huyu alikuwa hatoki hapa hata dakika moja. Hata haja zake alikuwa akiifanya hapa hapa karibu. Polisi walimchukua hapa akawachenga akarudi mwishowe wakamwachia akae tu. sasa leo nafika nakuta kiisha ondoka na wala harufu yake hakuna. Nimeshangaa sana. Amekaa karibu mwezi mzima".

"Ulikuwa unapata fursa ya kuzungumza nae?".

"Si mara nyingi, ila tu siku moja nilikuja na akasita kusema.

"Sema tu usiogope, hata kama ni siri, sisi tutakufichia".

"Lakini nyinyi ni akina nani?".

"Sisi tunashughulikia wagonjwa wa akili, tumepata habari toka polisi kuwa kuna mwendawazimu hapa, hivyo unaweza kutueleza tabia yake ili tuweze kumtafuta. Kwa hiyo usisite kutueleza", nilidanganya.

Baada ya kutafakari mambo haya aliendelea, "Siku moja kulikuwa na tafrija hapa ofisini jioni. Mimi niliweza kwa mbinu zangu kujipatia mzinga mzima wa whisky aina ya 'Dimple' nikauficha wagaeni wote walipoondoka, nilitoka nje ya lango na kuanza kunywa huu mzinga wa whisky. yeye alipoona ninakunywa hii whisky

alikuja na kopo lake akaniomba kwa vile nilikuwa najuwa siwezi kumaliza chupa nzima nilimgawia nusu basi alikunywa ile pombe kama maji. Basi ilipomkolea akaanza kuzungumza Kiingereza ila mara kwa mara alisema neno sijui 'Sazafrika' neno hili alilirudia mara nyingi. Na nyinyi mnajua vichaa mimi niliachana nae nikaendelea na shughuli zangu. Sasa sielewi kama kilikuwa Kiingereza sawa sawa. Lakini kitu kilichonivutia ni kule kutamka hicho Kiingereza chake kama mzungu. Lakini husema kichaa ana mashetani saba, anaweza kuzungumza lugha saba tofauti."

"Asante sana, na samahani sana kwa kukubugudhi", Sherriff alitoa mfukoni shilingi arobaini akampa. Yule Mzee alifurahi sana.

"Mungu awaongezee wanangu".

Tuliingia ndani ya gari tukaondoka zetu.

"Unaona mambo yalivyo Sherriff?, hii inaonyesha wazi kuwa George Kiki alikuwa ni jasusi aliyepachikwa hapa na mabeberu na wakafanikiwa. Mimi simulaumu mtu yeyote, hata mimi huenda ningemsaidia kupata kazi. Baada ya mabeberu kujua mkataba wa silaha kati ya PLF na Urusi miezi sita iliyopita walichukua hatua ya kuhakikisha hizo silaha haziwafikii wapigania uhuru wa PLF maana inasemekana ni silaha za kisasa kabisa. Tutakapoonana na kiongozi wa PLF atatueleza zaidi, kuajiliwa kwa kiki miezi sita iliyopita kunaona kabisa na nyakati za mkataba huo. Inaonekana kazi ya jasusi huyo ni kujua mambo yote yanayotendeka juu ya huo ili mwishowe aweze kuiba hizo karatasi za kuchukulia silaha, jambo hili amefanikiwa", nilinyamazi kidogo.

"Kwanini wamwue?", Sherriff aliuliza.

"Kwa sababu hawakuwa na haja nae tena, asiye akashikwa na kutoa siri. Hii inanionyesha jinsi watu hawa walivyo wajuzi katika kazi yao, hawataki kufanya makosa".

Wakati huu tukizungumza tulikuwa tukielekea mjini.

"Juu ya huyu kichaa unasemaje?".

"Huyu kichaa nae ni jasusi. Ninavyoona mimi huyu aliwekwa pale ofisini kusudi aweze kuona nini kitatokea hapo ofisini baada ya silaha kuibwa. Aliwekwa mwezi mmoja ili kuondoa mashaka. Hivyo alikuwa anangoja kuona baada ya polisi na maofisa wa usalama ni nani mwingine aliyekuwa na dukuduku juu ya jambo hili. Aliposikia waandishi wa habari wa gazeti la Afrika nao wamejiingiza akawa

amemaliza kazi, akaondoka kwenda kupeleka ujumbe, ni wazi kabisa wao walijuwa polisi na maofisa wa usalama watalishughulikia jambo hili na ninafikiri walishapima uzito na kuona wanaweza kukabiliana nao. Hivyo walingoja wajue kama kuna kundi jingine litakalojiingiza katika katika upelelezi wa tukio hili. Sasa wamejua; kwa hivyo waandishi wa gazeti lazima muwe macho. Tokea sasa kaeni katika tahadhari; lolote linaweza kutokea. Unaonaje maoni yangu?'

"Lo Willy, ndio maana wewe ni mpelelezi maarufu katika Afrika. Maelezo yako yanaeleza hali halisi kabisa. Na swali ulilomuuliza Margret kama kuna mtu mwingine aliyeweza kuona akiweka karatasi ndani ya mkoba, mimi nilikuwa silifikilii kabisa na ndilo swali lililotupa mwanga. Kweli kila mtu na kazi yake", alisifu Sherriff.

"Lakini maswali mliyouliza ninyi vile vile ni ya maana sana, nafikiri kuliko waliyoulizwa na Polisi. Sidhani Polisi wameishafikia hii tuliyofikia kwa muda huu mfupi".

Mara wazo likanijia.

"Lile jambo lililokuwa linakutatanisha nimepata jibu lake. Swali la nani aliyepiga simu kwa Mlingi akiiga sauti ya Mantare na maneno ya Mantare aliyozoea kuzungumza na Mlingi".

"George kiki", alijibu Sharriff.

"Kabisa, unajuwa Kiki alikuwa anaingia ndani ya kila ofisi ya ofisa akiwa kama tarishi. Swali hili nilimuuliza Mantare akakubali. Hivyo Kiki akiwa jasusi aliyefundishwa, ninavyofikilia, haikuwa kazi kumsiliza Mantare katika simu zake nyingi na ninafikiri alifanya kila njia kusikiliza simu kati ya Mantare na Mlingi. Hii inaonekana wazi kabisa".

"Lo tunaanza kuona mwanga sasa", Sherriff alisema.

"Kweli tumeona mwanga, lakini ni mwanga unaotufikisha kwenye giza nene. Maana Kiki ambaye angetupa fununu ya watu hawa amekufa, yule kichaa lazima ameshapotea hewani, gtumerudi pale pale".

"Watu hawa ni akina nani na silaha hizi ziko wapi?", niliuliza swali hili wakati naegisha gari New Afrika.

"Hilo ndio swali gumu lakini afadhali tunajua Afrika Kusini inahusika, maana Kiki katokea huko. Na yule kichaa alipolewa alizungumzia Sozafrika ambayo nasadiki ni South Afrika".

"Sawa kabisa, lazima tujuwe tunapambana na South Afrika na haikosi shirika lao la ujasusi 'BOSS', linasaidiwa na mashirika mengine ya ujasusi ya nchi za kibeberu. Hivyo tutakuwa na kazi ngumu maana watu hawa nimewahi kupambana nao ni watu hatari kabisa".

"Tumwombe Mungu atasaidia".

"Na wewe ukijisaidia", nilijibu.

Wote tukacheka na kutoka ndani ya gari. Ilikuwa saa kumi na moja. Hivyo kabla hatujavuka barabara nilionelea nifike ofisini kidogo halafu niende nyumbani.

"Sheriff mimi nafika nyumbani kidogo, nitakuona saa kumi na mbili kamili".

"Sawa nitakusubiri hapa duka la kahawa".

oke basi saa kumi na mbili".

Niliingia ndani ya gari na kuondoka. Nilipofika ofisini nilimkuta Eddy na vijana wengine. Linda alikuwa ameshaondoka.

"Eddy kuna mtu mmoja anaitwa George Kiki, alikuwa akifanyakazi kwenye ofisi ya Kamati ya ukombozi kama tarishi?, hapa aliingia kama mkimbizi baada ya kutoroka Afrika Kusini. Alifika ofisi za chama cha SANP, ambao walimpeleka kwenye Kamati ya Ukombozi waweze kumsaidia angalau kazi yoyote.

Inawezekana hana kisomo cha kutosha. Nataka ukague habari hii kwa kutumia njia zetu za kawaida. Unaweza kuwajulisha makomredi wetu kule Soweto, nadhani watakuwa na maelezo kamili. Habari hizi nazitaka haraka. Kila kitu, aliingiaje hapa alikwendaje kwenye ofisi za SANP alikuwa anaishi namna gani, nani walikuwa rafiki zake nk. wewe unajua".

Eddy aliyekuwa anachuku maelezo haya alijibu.

"Atashughulikiwa bosi, usiwe na wasiwasi".

"Chifu yuko?".

"Kaondoka".

"Haya asante, usitoke mpaka nitakapokujulisha tena".

"Mimi nipo".

Ndio sababu nilimpenda mtoto huyu. Nidhamu yake kwangu ilizidi ya mdogo wangu ambaye tumetoka ndani ya tumbo la Mama Willy. Niliingia ndani ya gari nikaelekea zangu Upanga.

Niliposimamisha gari mbele ya mlango, moja kwa moja macho yangu macho yangu yakaangukia kwenye kitu kilichokuwa kwenye ubao wa juu ya mlango mkubwa wa kutokea nje. Nilitoka nje ya gari haraka haraka nikiwa tayari kwa mapambano.

Nilikuta ni kisu chenye mpini mwekundu kama kile tulichokikuta kwenye kifua cha maiti Kiki; ncha yake ilitumiwa kama kipini cha kubandika kipande cha karatasi pale mlangoni.

Niliking'oa nikachukua karatasi na kusoma yaliyobandikwa hapo yalisema.

Willy Gamba, kama unathamini maisha yako achana na hao watu wa gazeti la Afrika. na kama ni rafiki zako waambie waondoke hapa mjini tunawapa mpaka saa kumi na mbili jioni wawe uwanja wa ndege. Vinginevyo yaliyompata Kamara Frank yatawapata na nyinyi. Hili ni onyo kali na si mchezo. Shughulika na mambo yako usishughulike na mambo ya watu wengine. Wapo wenyewe wanaohusika waachie. Nasema tena saa kumi na mbili jioni leo wawe uwanja wa ndege na wewe baada ya kuwafikishia habari hizi tusikuone unashughulika zaidi ya kazi yako ya kawaida ya AIA Subiani.

Kwanza nilicheka maana niliona kazi sasa inaanza. Hii inaonyesha upelelezi wetu ulikuwa umewashitua kuliko wa Polisi. Nilijua yule kichaa alifanya kazi yake vizuri sana, maana ni yeye tu aliyetufahamisha kwa majahiri wenzake. Hiki kisu chenye mpini mwekundu ilimaanisha damu. Nami niljua damu imeanza kunuka.

Nilifungua mlango nikaingia ndani, nikakoga haraka haraka kisha nikabadilisha nguo nilifungua sanduku langu la silaha na kuchukua bastola zingine mbili kwa madhumuni ya kuwapa Sharriff na Verokika kwani hakukuwa na mchezo tena, maana upatapo onyo toka kwa watu kama hawa huwa hawatanii. Kisha niliinua simu na kupiga kituo cha Polisi cha Salendar Bridge.

"Halo kituo cha Polisi hapa".

"Sikiliza, nenda Kinondoni Hananasifu, Estate kwenye nyumba ndogo ndogo za shirika la Nyumba nambari IIC utakuta kuna maiti ambayo ina zaidi ya masaa ishirini na nne", kabla hajatamka neno nilikata simu. Niliangalia saa yangu muda

ulikuwa umekimbia na ilikuwa saa kumi na mbili kamili. Niliingia ndani ya gari nikakimbilia New Afrika.

Nilipoingia duka la kahawa sikumwona Sherriff nikapata wasiwasi. Nikaenda mapokezi kuuliza wakaniambia aliacha habari kuwa amekwenda dukani mara moja nimsubiri. Nilirudi nikasimama nje pale magari yanapoleta watu New Afrika yanapozungukia. Niliangaza huku na huku na mara nikamwona Sharriff anakuja akiwa anavuka tawi la Benki ya nyumba. ghafla alipokuwa anataka kuvuka barabara ilitokea gari sijui wapi ikapiga breki, wakatoka watu wawili haraka kama umeme, wakamvuta Sharriff ndani ya kiti cha nyuma cha gari, na gari hilo likaondoka tena kama umeme. Kitendo hiki hakikuchukua hata nukta tano.

Watu wote waliduwaa wasijue cha kufanya, lakini mimi Willy nilijua la kufanya. Nilikimbia kwenye gari Eddy alilokuwa amekodi na kuliacha New Afrika. Kwa vile alikuwa ameliagesha vizuri niliingia na kuondoka kama umeme. Nilikuwa nimeona lile gari linakata kulia kutoka barabara ya Azikiwe kuingia Azania Front. Nilipoingia Azania Front niliona gari lao linafika kwenye ofisi za NASACO nikacheka.

SURA YA SITA

TWATOANA JASHO

Niliongeza gari moto ili wasije kunipotea. walikata kulia wakaingia mtaa wa Railway, nilipoingia mimi mtaa huu wao walikuwa wamefika kwenye mzunguko wa 'Clock Tower' na kuingia mtaa wa Nkurumah.

Kwenye mtaa huu wa Nkurumah niliwakaribia kabisa, nikiwa nimeacha gari mbili tu kati yangu na wao. Niliona mmoja katika gari lao akitoa kichwa nje na kuangalia nyuma, nadhani wanadhani nitawafuata na gari langu ambalo wanalijua sana. Lakini hawajui Willy ni mtu wa namna gani. Wakati huo nilikuwa naendesha gari aina ya Fiat 132 GLS, na si Colt Gallant Sports kama ambavyo walikuwa wanafikiria.

Walikwenda moja kwa moja na kushika barabara ya Pugu. Walipofika kwenye njia panda ya barabara ya chang'ombe na Pugu, walikata kushoto na kuingia barabara ya Chang'ombe. Saa hizi magari hayakuwa mengi hivyo kila gari lilikwenda kasi. Nilikuwa na bahati kuwa magari yale mawili yaliyokuwa kati yangu na wao nayo yalikata na kuingia barabara hiyo hiyo kuzidi kunificha.

Walipofika kwenye sehemu ambayo barabara ya Mbozi inagongana na Chang'ombe walikata kulia na kufuata barabara hiyo. hizi gari mbili mbele yangu zilionyesha kuwa zilikuwa zinaendelea na barabara ya Chang'ombe. Nilipunguza mwendo ili wasije wajanitambua. Mara nilisikia wanapiga honi ya namna ya pekee kabla ya kufika kwenye jengo la Kampuni ya rangi ya Sadolins.

Ghafla lango la uwa la bohari moja lilifunguliwa na bila hata kupunguza mwendo, gari hii ilikata kushoto na kuingia ndani na hapo lango likafungwa. Mimi nilipitiliza kama kwamba sina habari na watu hawa. Ilikuwa inakaribia saa moja za jioni, hivyo giza lilikuwa limeanza kuingia. Nilisimamisha gari langu kama mita mia mbili hivi, nikaanza kurudi haraka kwa miguu.

Bohari hili ambalo lilikuwa limezungukwa na ukuta wa matofali ya saruji, lilikuwa limeandikwa 'Mamlaka ya Pamba'. Mimi nilishangaa sana kwani sikujua hii ni maana gani. Ukuta wa uwa huu ulikuwa na urefu usiozidi futi kumi na mbili, hivyo kwangu ukuta kama huu kuupanda ni kazi ndogo. Nilikwenda kwenye upande wa lango kubwa, nikazunguka pembe ya kushoto ya uwa huu. Ukuta huu ulikuwa

unapakana na ukuta wa bohari nyingine la namna hiyo hiyo kwa upande huu wa kushoto.

Nilikwenda kama hatua tatu hivi kwenye nafasi hii ya kati ya mabohari haya, nikavua viatu, nikarudi nyuma kidogo halafu nikaurukia huu ukuta na kuukwea huku mikono yangu ikikamata juu yake. nilivuta mwili wangu wote kimya kimya kama paka nikachungulia ndani ya uwa.

Pale karibu na mlango nilimwona mtu amevaa koti refu la khaki rangi nyekundu lililokuwa linavuka magoti yake kidogo huku ameshikilia bunduki ya aina ya 'SMG' na akiangalia mlangoni. Bila kufanya hata chembe ya kelele nilivuta mwili wangu wote na kutambaa kama nyoka juuya ukuta huu uliokuwa na upana wa futi moja. Nilitambaa mpaka nikawa karibu kabisa na mtu huyu kwa juu yake bila yeye kufahamu. Nilijirusha chini na kufanya kishindo kidogo nae akageuka. Mimi nilikuwa tayari nikamkata karate ya shingo kabla hajajua nini kinamjia. Akazilai. Nikamshikilia na kumlaza chini taratibu. Muda kitambo aloikufa.

Nilimvua lile koti lake nikalivaa mimi, halafu nikamnyanyua tena nikamlalisha chini na kumwegemeza kwenye ukuta. Nilichukua bunduki yake ambayo ilikuwa imejazwa risasi, nikafurahi sana kishika silaha namna ile. Mimi nikiwa na silaha namna ile hata likija jeshi la watu mia hawaniwezi. Nilijidhatiti tayari kwa mapambano zaidi nikanyata kwenda nyuma ya jengo la bohari ambako niliamini kuna mlango mwingine. Nilipofika kwenye pembe ya ukuta wa kushoto nilichungulia. Niliona kuna mlango wa mbele wa mlango alisimama mlinzi mwingine akiwa amevaa sawasawa na yule wa kwanza; koti refu jekundu.

Alikuwa nae ameshika bunduki ina ya 'SMG', niliona anafungua mlango anasema kwa sauti kali "Fanhyeni haraka bwana, kama hataki kueleza si niambieni mimi akaonane na babu zake huko ahera". Alirudisha mlango akaangaza huku na huku. Kutokana na maelezo yake ni kwamba Sherriff alikuwa anaswalishwa na majahiri na bila shaka alikuwa akipata kipigo kikubwa.

Nilitumbukiza mkono ndani ya mifuko ya koti nililovaa nikakuta mna sigara na hamna kiberiti. Wazo likanijua nikamfanyia yule mlinzi 'sss' aligeuka akaniona akidhani ni mwenzake, nilimuonyesha sigara na kuwa nataka moto. Bila kusita akaja akatoa kiberiti na kwa ajili ya giza sasa hakuweza kunitambua sababu ya lile koti. Aliponyoosha mkono kunipa kiberiti. Kama radi nilimrukia na kumpiga karate ya mikono miwili shingoni. Sikuwa na haja ya kumwangalia maana nilijua kwa kipigo hicho hawezi kuishi. Nilimvutia upande huu wa kushoto na

kumwegemeza kwenye gari lao. Nilichukua bunduki yake iliyokuwa na ukanda mrefu nikaingika begani na kuiweka mgongoni.

Sasa njia ilikuwa wazi kwenda mpaka mlangoni, kwa kutokana na ujuzi wangu wa kuiga sauti ya yule mlinzi wa nje kwa maneno yake aliyosema mimi nilisema. 'Vipi hajasema lolote?,' nikiwa nimefungua mlango kidogo na kuchungulia ndani. Bohari lilikuwa limejaa robo tu ya marobota ya pamba. Sherriff alikuwa ameshikwa na watu wawili na mmoja alikuwa amebeba bao akimtandika tumboni kwa nguvu sana.

"Sema nyie si waandishi wa magazeti ila ni wapelelezi, ndio".

"Yote ya kweli nimeshaeleza ".

Kabla hajaanza kumpigab tena nilisema. "Mmoja wenu aje hapa, mimi mnanijua hivyo hatachukua dakika kabla hajasema uweli wake".

Shomvi alikuja akikimbia, nikamfungulia mlango na kurudisha mara moja. Alipoangalia ba kutambua mimi si Luis akataka kupiga kelele lakini nilimwahi karate ya katikati ya kichwa akafa bila kelele. Watu wa mle ndani waliokuwa wamemshikilia Sherriff walikuwa hawana bastola mikononi ila zilionekana kwenye mapaja. Nilifungua mlango ghafla SMG mkononi nikamwahi mmoja wao kabla hata hawajaelewa nini kinatokea.

"Ukijaribu chochote umekufa", nilisema kwa sauti ya kutetemesha.

Sherriff alishangaa kuniona akaruka ile maiti akasimama upande mwingine. Niliona ile SMG ya pili nikampa, akatabasamu. Jinsi alivyoijaribu mkononi nilikua huyu mtu anajua kuitumia.

"Chukua hizo silaha zake", Sherriff alimkagua akatoa bastola mbili zenye sailensa na visu viwili vyenye mpini mwekundu.

"Ah, ni wakati wako sasa kujibu maswali yetu, nyinyi ni nani", nilimwuliza.

"Mimi sijui, mimi niliajiriwa tu leo hii asubuhi na Kimkondo, huyu uliyemwua hapo chini, kuwa kuna kazi ya kumkamata mtu mwenye habari ambazo wakubwa wake wanataka. Pesa tulizolipwa zilikuwa nyingi, shilingi elfu kumi kwa kila mtu kwa kazi ya masaa machache tu nami nikakubali, kusema ukweli sijui lolote".

"Yeye Kimkondo anafanya kazi gani?".

"Yeye ni jambazi tu anayepewa kazi ya ujambazi hapa na pale".

Kutokana na maelezo ya huyu mtu nikajua anasema kweli. Nilijilaumu kumwua Kimkondo maana yeye huenda angetupa mwanga zaidi. Lakini hii yote inaonyesha jinsi majahiri hawa yalivyokuwa yamepanga ujahili wao kwa ufundi.

"Lo Willy asante sana".

"Sahau", nilimjibu kwa mkato.

Ile sura ya kikatili ilikuwa tayari imekuja usoni mwangu. Katika hali kama hii sura yangu hubadilika na kuwa mtu tofauti kabisa. Hivyo nilipomwambia Sherriff sahau niliona anashituka kidogo.

"Twende zetu tutoke hapa Sherriff, huyu nitajua mahali ya kumpeleka".

Tulimtangulia, tukafungua mlango wa bohari tayari kurudi mjini. Tulipokuwa tumefika kwenye kona niliyotokea, tukasikia honi ya gari ya namna ile ile waliokuwa wamepiga hawa majahili wa kwanza.

"Sherriff na wewe mtu mjifiche nyuma ya hili gari, kwa vile mimi nimevalia koti lao ambalo naona ndicho kitambulisho chao nitakwenda kufungua lango, unayo ile bastola uliyochukua kwake?".

"Ndio".

"Basi akifanya ushenzi unajua la kufanya; maiti hazisemi".

Niliwaacha nikakimbia mpaka kwenye lango nikafungua. Gari aina ya VW Kombi iliingia imejaa watu wamevalia makoti kama langu, Gari hili lilisimama nyuma ya lile gari la kwanza. Milango ikafunguliwa wakaanza kutoka. Mimi nilikuwa tayari na SMG yangu.

"Rudini ndani....." niliona yule mtu tuliyekuwa tumemshika ameruka juu ya gari na kutoa onyo, lakini kabla hajamaliza Sherriff alimlamba risasi ya kichwa akaanguka juu ya gari, mimi nikajua tayari mambo yametibuka, hivyo sasa ni kazi.

Dereva wa gari hii na watu wengine waliokuwa bado ndani ya gari walifunga mlango ili waondoke. Wale waliotoka nje walianguka chini na kutoa bastola tayari kwa mapambano. Mimi nilikuwa nimeishavua koti nimerukia ukutani na tayari SMG mkononi. Nilikuwa nimelalia tumbo juu kabisa ya ukuta. Lile gari lilipopiga moto, nililenga mlango wa dereva na kuachia risasi mfululizo kama mchezo.

Sherriff alikuwa bado kimya hajaanza shughuli. Wale watu watano waliokuwa wametoka ndani ya gari nao walikuwa wametambaa upande mwingine wa kombi.

Kumbe mmoja wao aliniona kule juu baada ya kuona risasi zilizoua wenzake zikitokea juu. Mimi nilikuwa bado sijamwona hivyo akainuka kunimaliza. Lakini kumbe Sherriff alimwona kabla hajafyatua risasi, akamwahi. Nilipomwona Sherriff akanionyesha ishara. Alikunja kiganja halafu akainua kidole kimoja kuonyesha kuwa ni watano na mmoja tayari kafa.

Mimi nilijirusha chini toka ukutani na kujiviringisha huku nakoswa koswa risasi za maadui. Niliposimama huku nikikimbia zigizaga na wakati huo nikipiga risasi ovyo kuwazuia wasipige. Nilifika mlango na kufungua kama ninakimbia nje. Wale kwa woga wao walipoona hivi nao walianza kukimbia kuwahi mlangoni.

Kumbe ndipo walikuwa wanampa fursa Sherriff kuwachukua mmoja mmoja vizuri sana. Na mimi ghafla nilijitokeza tena na kumimina risasi kwa wawili waliokuwa mbele. Bahati nzuri Sherriff alijitupa chini la sivyoyingetokea ajali kwani yeye alifikiri nitawasubiri nje hivyo naye alikuwa anawafuata nyuma.

"Kazi nzuri Sherriff, la sivyoyingekuua, pole sana", nilimpa mkono.

"Hali kama hizi nimezizoea sana hivyo huwa niko tayari katika tahadhari kila mara kwani lazima kama huna uhakika mwenzako atafanya nini baadaye tegemea lolote", Sherriff alijibu.

Tulikimbia kutoka pale mpaka kwenye gari langu. Tuliingia na kuwasha gari moto na kuelekea zetu mjini.

"Mimi nilijua ndio mwisho wangu", Sherriff aliniambia.

"Kwa nini?".

"Maana walivyoniwamia hata nilishindwa la kufanya halafu nilijua wewe utakuwa unanisubiri New Afrika na kumbe mimi nimeshauawa. Na kweli wangu".

Alitoa shati lake kuonyesha uvimbe mbaya sana kwenye tumbo lake.

"Nasikia maumivu ya ajabu. Watu hawa ni katili sana".

"Pole sana. Jambo la kusikitisha ni kwamba imebidi tuwaue wote. Hivyo bado tumerudi pale pale; hatujui lolote, isipokuwa tu kwamba watu hawa ni majahili wa hatari sana wanaovaa makoti mekundu na bunduki wanazotumia ni SMG za kichina, bastola za kirusi zenye sailensa. Zaidi ya hapo bado tuko mbali sana na ukweli wa mambo. Ila kinachonifurahisha ni kwamba sasa watashtuka baada ya mapambano haya ambamo tumeua watu wao karibu kumi na tano. Kule kushtuka ndiko kutatusaidia maana lazima watahaha na kufanya makosa".

"Sawa kabisa. Lakini mimi nataka kujua jinsi ulivyojua nimekamatwa na namna ya gari umeweza kuniokoa. Maana mimi sikuamini nilipokuona, nilidhani huenda ni malaika kashuka toka mbinguni katika sura yako".

Tukiwa bado tunaelekea mjini nilimweleza jinsi nilivyofanya.

"Lo ndio sababu wewe ni mpelelezi namba moja katika Afrika; mimi sasa nadhani hata katika dunia. Tukirudi London salama nitailisha komputa maelezo zaidi juu yako tuone itakuonyesha katika nafasi gani katika wapelelezi wa ulimwengu".

Mimi nilicheka tu sikujibu kitu.

"Na kule kubadili gari kulisaidia sana maana walipochungulia na kulikosa gari lako walinidhihaki kwa kusema kuwa sasa nitakufa peke yangu hata rafiki zangu hawatathubutu kuja hata kama wangeniona wakati ninakamatwa".

"Mimi ni mjuzi zaidi yao; lazima tuzidiane maarifa".

Tuliingia barabara ya Independece Avenue.

"Nitakupeleka kwa daktari wangu hapa Zanaki Street, na utalala hapo. Nafikiri kesho utakuwa katika hali nzuri, kwa leo lala hapo usirudi New Afrika ili daktari aweze kukupa matibabu kwanza. Nitakuja kukupitia asubuhi".

"Sawa wewe ndiye bosi", Sherriff alijibu.

Nilimpeleka kwenye zahati ya rafiki yangu Dk. Kiluwa na kumweleza amtibu na malipo yatalipwa na AIA. Nilimwacha nikawaahidi kuwaona asubuhi yake.

"Eddy nafikiri unaweza kwenda kupumzika. Acha vijana wa zamu waendele, maana kesho tunaweza kuwa na kazi nyingi sana".

"Asante tutaonana asubuhi", alijibu huku akikusanya kusanya karatasi zake.

Mimi niilimuaga nikaondoka zangu kuelekea New Afrika tayari kuonana na Veronika. Nilipofika New Afrika nilikuta duka la kahawa limejaa watu na ile sehemu ya Patio Baa ndio usiseme, maana vijana walikuwa wamejazana wakifurahia saa zao za baada ya kazi.

Nilishikashika mfukoni, nikachukua funguo za gari mkononi nikaelekea kwenye gari langu, niliona Vero alikuwa bado hajafika kwani hamkuwa na mtu ndani ya gari. Nilifungua mlango wa upande wa dereva ili nikae nimsubiri, maana nilijua asingechukua muda mwingi.

Nilipoingia na kukaa kitini na kuanza kutelemsha kioo, nilisikia kama kuna kitu kwenye viti vya nyuma vya gari langu. Nilipotaka kugeuka kuangalia nilisikia sauti ikisema. "Usigeuke la sivyo utakuwa ndio mwisho wako. Washa gari ondoka, na ufuate maelezo yangu".

Nilisikia mdomo baridi wa bastola ukigusa shingo yangu.

"Sawa mzee", nilijibu huku nikijifanya kama sijali.

"Siyo mzee, sema wazee. Tuko wawili na wote tuna bastola na tunajua kuzitumia hivyo usijaribu kitu chochote cha kuleta matatizo".

"Mimi sina wasiwasi, maana sijui kwanini natekwa nyara, kama nia yenu ni gari niambieni niwaachie. Mimi ni mfanyabiashara nitapata gari nyingine, kwangu pesa si tatizo".

"Funga domo lako, sisi hatuna haja na gari lako wala pesa yako, sisi tuna pesa kuliko wewe".

Kabla sijasema lolote aliniambia. "Kata kushoto ingia Independence Avenue, halafu ukifika 'Clock Tower' ingia mtaa wa Railway halafu shika barabara inayopita kwenye kituo cha polisi wa usalama barabarani, halafu ukifika kwenye mzunguko ingia kushoto, fuata barabara ya Kilwa mpaka nitakapo kueleza tena. Nasema tena ujanja wowote utakutokea puani".

"Usiwe na wasiwasi", nilijibu kiume.

"Nyamaza", alijibu kwa sauti ya ukali.

Nilijilaumu sana kwa kutochukua tahadhari zaidi kwa watu hawa.

Nilifikiria kama naweza kufanya lolote sasa nitakuwa kwenye upande wa hasara hivyo nikakata shauri la kufuata maelekezo mpaka mwisho ndipo nione la kufanya. Maana nafikiri kama nia yao ilikuwa ni kuniua wasingesita, walikuwa na mwanya mzuri sana nilipoingia bila tahadhari ndani ya gari. Nilijua nia yao si kuniua ila kuna habari walizozitaka. Nilimfikilia Veronika nikajua atahangaika sana kwani hatanikuta halafu hatajua Sherriiff aliko.

Tulipokaribia uwanja wa Sabasaba aliniamuru nikate kushoto kwenye njia inayoelekea kwenye ofisi mojawapo za reli ya Tazara ya Kurasini. Tulipotelema kidogo aliniamuru nikate kulia na kuingia kwenye mlango wa pembeni wa uwanja wa Monyesho ya Sabasaba.

Tulipofika kwenye mlango huu aliniamuru nipige honi. Nilipopiga honi mlango ulifunguliwa. Taa zangu zikamwulika mlinzi aliyevaa joho jekundu, nikajua mara moja ni nani nimepambana nae tena. Tena huyu mtu aliongeza na kofia nyekundu juu.

Nilishangazwa sana na mbinu za watu hawa, maana sehemu zo walizokuwa wanazitumia kama kambi zao za kufanyia uovu zilikuwa sehemu za kiserikali. Hii ilionyesha jinsi mbinu za watu hawa zilivyozidi kiwango.

"Ingia ndani moja kwa moja, fuata barabara mpaka nitakapokuabia simama", niliamriwa.

Uwanja ulikuwa kimya kabisa. Giza lilitanda kote ila taa za gari langu peke yake. Tulikwenda mpaka katikati ya vibanda.

"Simama hapa, zima taa na telemka taratibu. Ukifanya makosa usinilaumu", alinielea. Nilipozima taa tu niliona vivuli vya watu vikinyata polepole kuja kwenye gari. Nilipokanyaga nje tu gari likawa limezungukwa na watu watatu. Wale waliokuwa ndani ya gari walitelemka.

"Mmemleta?", mmoja wa wale waliozunguka gari aliuliza.

"Ndio", alijibu yule mtu aliyekuwa ananipa amri".

"Kazi nzuri, haya twendeni".

Yule mtu aliyezungumza alitangulia mbele mimi nikaambiwa nimfuate huku nimezingirwa na watu wanne. Yaani wale wawili walioniteka, na wengine wawili waliokuwa wamebeba bunduki aina ile ile ya SMG, ilionekana hawa watu walitumia sana aina hii ya bunduki.

Niliongozwa moja kwa moja mpaka kwenye kibanda kimoja katikati kabisa ya uwanja wa maonyesho wa Sabasaba. Nilikumbuka kuwa kibanda hiki kilikuwa kinatumiwa na nchi za Zambia katika maonyesho ya Kimataifa. Mlango ulifunguliwa tukaingia. Ndani tulimkuta mtu mwingine anavuta mtemba amekaa kwenye kiti huku akitabasamu. Watu hawa wote walivalia majoho mekundu. Na hawa wanne niliowakuta huku kiwanjani walivaa kofia nyekundu isipokuwa wale walioniteka ndio hawakuwa na kofia.

"Karibu Willy Gamba, keti chini kwenye kiti", aliniambia yule mtu tuliyemkuta ndani.

"Asante, mimi ningependa kusimama", nilijibu.

"Mimi sitaki kukukarisha kwa nguvu, lakini kama unaona ni lazima nifanye hivyo ninao uwezo, Willy", aliniambia taratibu huku wale watu wengine wakinisogelea. Niliona hakuna haja kuchachamaa hapa hivyo niliketi kwenye kiti.

Chumba hiki kilikuwa kimewekwa fenicha nzuri sana, hata nikashangaa saa ngapi watu hawa waliweza kuaandaa chumba hiki kama ofisi na huku uwanja huu siku zote unalindwa.

"Romano na Charles mnaweza kwenda nje kusudi muwe tayari kukabiri jambo lolote linaloweza kutokea hapo nje wakati nikiwa na mazungumzo mafupi na Willy hapa", alitoa amri polepole kiasi kwamba ungeweza kuamini kuwa ni mtu mzuri sana, lakini macho yake yalionyesha uovu usio kifani.

Nilifurahi sana kwani nilijua kuwa sasa ninaonana na mtu wa maana katika kundi hili la majahili. Macho yetu yalipokutana ana kwa ana mara moja tukatambuana, maana huyu alikuwa jasusi wa hali ya juu. Sisi tuko kama mbwa tunajuana kwa harufu. Wale watu wawili wenye SMG walitoka nje tukabaki na wale watu walioniteka nyara, yule mtu aliyetupokea na huyu mtu tuliyemkuta humu ndani. Walipotoka nje waliufunga mlango.

"Bwana Gamba, mimi ni mtu nsiyependa kuumiza kwa sababu mimi huwa sijisikii vizuri nikiona mtu anaumizwa. Lakini nikilazimika kufanya hivyo, basi mimi hufumba macho. Nisingependa nifumbe macho kwako kwa hiyo naomba sana uwe mtu mwungwana katika kujibu maswa yangu".

"Nadhani ungependa kujua sisi ambao tuko hapa ni nani, sisi ni WANAMAPINDUZI WAPINGA MAPINDUZI".

"Wanamapinduzi wapinga mapinduzi maana yake nini?. Sikuelewi.

"Ni kwamba sisi tunapinga watu wanaojiita Wana mapinduzi, wanaofikiri wataleta uhuru Afrika Kusini kwa njia ya vita. Sisi ni wanamapinduzi ambao tuna imani kuwa tutaleta uhuru Afrika Kusini kwa mazungumzo bila kuua mtu hata mmoja. Sasa swali langu ni hili; Wewe na rafiki zako mna nia gani katika kupeleleza upoteaji wa silaha?, Kwanini msiwaachie watu wanaohusika?".

"Mimi si mwana siasa hivyo unayonielea juu ya namna gani uhuru utakavyopatikana huko Afrika Kusini sina haja ya kujua. Lakini wageni wangu ni waandishi wa habari na kumetokea hapa mjini Dar es Salaam wizi wa silaha uliotingisha ulimwengu. Hivyo wakiwa waandishi lazima wapeleleze wapate kueleza ulimwengu mambo haya yametokeaje. Sidhani kama kitu hocho ni

dhambi. Ni kitu cha kawaida". Nilimjibu taratibu nikijaribu kupima hali ndani ya chumba hiki.

"Imeonekana hawa waandishi wa habari wamekwenda zaidi ya kiwango cha upelelezi wa kigazeti, kiasi cha sisi kuamini kuwa si waandishi wa gazeti ila wapelelezi. Jioni hii kama huna habari rafiki yako Sherriff ameua vijana wangu zaidi ya kumi. Mtu mmoja, Willy, mtu mmoja?, siamini kabisa kuwa yeye ni mwandishi".

"Swali langu la pili nataka nujue yeye ni nani na sasa hivi yuko wapi?. Ukijibu maswali haya nitakuachia, usipojibu jua ya kwamba kesho huioni".

"Mimi ninavyojua ni kwamba yeye ni mwandishi wa habari, kama ni mpelelezi haya ni maneno yako, Kampuni yangu ni wakala, hivyo nilivyofanya mkataba na gazeti la Afrika na watu hawa walipokuja nilijuwa ni waandishi. Pili sijui aliko sasa hivi, tuliachana saa nyingi na tulipanga tuonane saa kumi na mbili New Afrika Hoteli lakini sikumkuta.

Baada ya kufikiri kidogo akasema, "La hasa, unajua".

"Sijui".

"Au unataka mpaka nifumbe macho".

"Hata kama ukifumba macho, sijui".

"Lucas na Moshi hebu mmwonyesheni huyu namna ya kujibu", alisema tena pole pole.

"Simama", alisema Lucas.

Sikusimama. Basi walinijia wote pale kitini kama faru, na mimi Willy tayari nilikuwa nawashwa kumwonyesha huyu mkubwa wa kuwa Willy hasukumwi ovyo.

Kama umeme nilisimama upesi na kukwepa ngumi ya Lucas na kwa sababu alikuwa ameitupa kwa nguvu sana aliopesuka mimi nikampiga teke kwenye mapumbu akalia kama nguruwe na wakati huo shoto langu lilimfikia Moshi singoni nae akapesuka mpaka chini. Yule mtu mwingine aliyetuongoza toka mwenye gari alitoa bastola yake lakini mimi niliona hatua hiyo nikaruka upande mwingine wa chumba na risasi zikanikosa, na wakati huo mlango nao ulifunguliwa na mtu aliyevaa joho jekundu na kofia nyekundu akiwa na SMG mkononi akampiga risasi ya mgongo kabla hajanimaliza pale niliporukia, na yule mtu akafa pale pale. Huyu

mtu wa SMG alimimina risasi kwa wale wengine waliokuwa wanajaribu kutoa silaha zao na kuwamaliza hapo hapo. Mimi katika harakati za kujiokoa niona yule mkubwa wao anaruka nyuma ya kiti, nikatoa bastola yangu, lakini nikawa nimechelewa, kwani nyuma ya kiti chake kulikuwa na mlango mdogo kimo cha urefu wa kochi. Hivyo alijitumbukiza.

"Anaondoka huyo Willy", nilisikia sauti nya Veronika akimimina risasi pale kwenye mlango lakini yule mtu alikuwa anajua nini anachofanya, hazikumpata akakimbia nje.

Mimi nilishangaa sana kumwona Veronika katika joho jekundu na kofia nyekundu na SMG mkononi amefika wakati kabisa uliohitajika kuniokoa.

"Oh Vero mkombozi wangu, umetokea kama malaika vile".

Alitupa bunduki akavua kofia na joho, haraka hara akaja akanirukia shingoni na kuanza kunibusu, kisha akaniachia.

"Tutoke hapa mpenzi, nitakueleza baadae", alininong'oneza.

Tulitoka ndani ya banda hilo na kusikia gari linaondoka.

"Mshenzi amepona", Veronika alisema.

"Iko siku yake", nilijibu.

Niliokota bunduki mbili pale nje, tukaenda kwenye gari letu tukaziweka ndani. Tukawasha gari na kuelekea mjini. Tulipofika Kilwa Road Veronika alianza kunisimulia.

SURA YA SABA

CHIMALAMO

"Baada ya kuzungumza na wewe kwenye simu, niliondoka kwenda New Afrika kama tulivyoagana. Niliona hakuna sababu ya kuchukua gari, hivyo niliondoka kwa miguu kwani nilijua dakika kumi ningenitosha. Nilikuja moja kwa moja na barabara ya Azania Front nikakatisha pale kwenye kanisa la Kilutheri na kutokea barabara ya City Drive. Kama unavyojua New Afrika inajengwa kwa mbele kwa hivyo nilijipenyeza kwenye mwanya wa jengo la Benki ya Taifa ya Biashara tawi la City Drive na Azikiwe, nikawa nimetokea karibu kabisa na pale ulipoegesha gari lako".

Ghafla nikaona watu wawili, mmoja wao akifungua mlango wa gari lako. Mimi nikasimama na kujibanza kwenye moja ya nguzo za jengo hili la Benki huku giza likinisaidia. Yule wa mbele aliingia na nyuma akaangalia huku na huko hakuona kitu nafikiri, maana alitoa bastola mwenye joho lake nae akaingia. Kama unavyojua gari hili lina milango miwili tu, hivi waliinamisha kiti na kuingia nyuma ya gari.

Mara moja nikajua nia yao; nilijua wanakusubiri wewe ama kukuua ama kukuteka nyara. Nilipofikiri sana niliona nia yao kukuteka nyara kwani kama ni kukuua wasingeingia ndani ya gari, hasa nyuma, na mahali penyewe pakiwa karibu sana na New Afrika. Huwa naamini sana akili zangu zinavyonituma hivyo nikaona kuwa nia yao ni kukuteka nyara. nilifikiri nikufuate lakini sikuwa najua ofisi yako ilipo. Hivyo nikaamua kitu kimoja, kuingia ndani ya buti la gari kama iwazi. Kwa kuwa gari yako ina nyavu kioo cha nyuma, nilijua watu hawa hawataniona wala kunisikia, kwani nilijua na wao watakuwa wamelala chini ili usije ukawaona wakati unaingia".

Alinyamza kidogo ili kulegeza koo kwa mate, akaniangalia akanikuta mimi naendesha taratibu huku nikimsiliza kwa makini sana. Kisha akaendelea, "Nikisaidia na giza la ukuta wa mabati uliozungushiwa jengo hili la mbele la New Afrika huku nikinyata nimeinama kimo cha buti la gari. Kama bahati ilivyokuwa na mimi nilikuta buti lako halikufungwa na funguo. Jihadhari sana siku nyingine utabeba adui ndani ya gari lako".

"Nimekuwa sina aduini Tanzania, hivyo nimekuwa nikiamini kuwa hakuna mtu wa kunifanyia ubaya, maana hata sijawahi kugombana na mtu hapa Dar es Salaam".

"Haya sasa lazima utambue kuwa umepata maadui; lazima ujihadhari".

"Sawa nitajihadhari lakini vile vile kama ningekuwa nimefunga usingeweza kuniokoa, hivyo kujiachia mambo mara nyingine ni vizuri".

"Haya nimekubari kushindwa, lakini hata hivyo ningepata njia nyingine. Basi taratibu nilifungua buti la gari na kuingia ndani, kimya kimya kabisa bila kelele yoyote. Niliwahi kusafiri ndani ya buti wakati ninakaa na majeshi ya POLISALIO, hivyo najua sana hali ilivyo ndani ya buti la gari kiasi kuwa kwangu hewa ya mle ninaweza kuistahamili ingawa ni kidogo. Unajua gari linapoanza kutembea hewa inajaa kabisa. Basi baada ya kuingia na kulifunga kinamna, kiasi ambacho lisingeweza kunishinda kufungua, baada ya kuliangalia kufuli lenyewe.

"Muda si mrefu nilisikia mlango unafunguliwa; unajua hili gari lako lilivyo undwa ukiwa ndani ya buti unasikia maneno yanayozungumzwa ndani ya gari. Basi niliwasikia wakikuamrisha kuendesha gari ndipo nikajua nilivyohisi ni sawa. Ulipopiga honi na kusimama kama ulivyoamrishwa, nilijua tunaingia mahali na nikajua kuna mtu anayefungua na kufunga mlango ni wa kundi lao hivyo atakuwa ni mlinzi mwenye silaha.

"Tulipoanza kuondoka niliinua mlango wa buti kidogo sana na nikamuona mtu huyu nusu amebeba bunduki. Niliendelea kuchungulia hivi hivi nikaona njia tuliyotokea kutoka kwenye lango mpaka gari liliposimama nikabana tena mlango. Nikasikia wanakuamru toka kisha nikasikia sauti zingine hapo nje halafu pakawa kimya, ndipo nikafungua taratibu mlango na kutoka nje. nikakata shauri lazima nipate silaha ili niweze kukuokoa.

"Hapo ndipo nilipoanza kurudi mbio kwenye lango ili nikamnyanganye silaha yule mlinzi. Nilipokaribia lango nilimuona yule mlinzi amesimama anavuta sigara huku anaangalia upande wangu. Nililala chini na kusubiri. Alipogeuka na kuangalia upande mwingine nilianza kutambaa chini kimya kimya. Nilikuwa nimefundishwa na wanajeshi wa Polisalio namna ya kumnyemelea mtu kwenye giza bila yeye kushituka. Nilipokuwa karibu nae kabisa, nilisimama na kupiga kelele, "Yeeeeee".

"Alishituka na kuingiwa na hofu na kabla hajatokwa na hofu nilipiga teke mikono yake bunduki ikaanguka chini. Alipoona hivi akaanza kukimbia. Niliruka na kumpiga teke mgongoni akaanguka chini. Bila kuchelewa nilimrukia shingoni, ndivyo ikawa kwaheri. Nilimvua joho nikalivaa halafu nikatafuta kofia. Nilipoipata

nikaivaa halafu nikachukua bunduki nikakuta ni aina ambayo wanaitumia wana mapinduzi wa Polisalio, yaani SMG ya kichina, hii bunduki niliitumia sana wakati nimekaa na hawa mashujaa wa Polisalio.

"Nilipoipata silaha hii, nilikimbia kurudi kwenye kibanda mlichuingia nipokaribia nikaona watu wawili wenye bunduki nikononi wakizunguza. Mimi nilizunguka nyuma ya kibanda cha karibu, halafu nikakohoa kisha nikazunguka haraka kutoka pale nilipokoholea. Nilisikia mmoja wao akisema; "Umesikia hicho".

"Ndio", alijibu mwenzake.

"Wewe zunguka huku na mimi nitapita huku".

"Hii ilinipa nafasi kujitayarisha, sikuwa nahitaji kutumia bunduki maana mrio ungewashitua watu waliokuwa ndani ya kibanda. Kwa vile nilikuwa nimevaa nguo kama wao na kofia, nilizunguka na kukutana na mmoja wao, yeye alinichukulia ni mwenzake shauri ya mavazi na giza. Tulikaribiana sana akabweteka; "Umeona nini?". Mimi niliinua mkono kumuonyesha nyuma yake na alipogeuka tu nikamkata karate ya shingo iitwayo ua na bila shaka alikufa pale pale. Nilimdaka haraka haraka na kumlaza chini bila kishindo. Kisha nikageuka upesi upesi ili nikutane na yule aliyepita upande mwingie sikuchukua hata hatua tatu tukawa tumekumbana hata yeye mavazi yalimdanganya na kufikiri mimi ni mwenzake.

"Huku hakuna kitu", aliniambia kwa sauti ya chini chini. Nilimdanganya kwa kumuonyesha kwa ishara aangelie nyuma yake na yeye akadanganyika. Hapo ndipo nilipomrukia nikamtia kabali ya hali ya juu mpaka niliposikia shingo linakatika nikamwachia. Sina mkanda mweusi wa judo na karate bure Willy, najua jinsi ya kuutumia".

"Zaidi ya ambavyo ningetegemea mrembo kama wewe kuutumia", nilimjibu huku nikitoa tabasamu.

"Asante. Baada ya hapo ndipo nilikimbia na kupiga teke mlango kwani nilisikia mlío wa bastola kabla sijapiga teke mlango. nilipoingia nilikuona chini hivyo nikafanya kama ulivyoona. Lo! Willy mpenzi niliogopa niliposikia mlío wa bastola nikafikiri wamekuua!".

"Si lahisi kuniua".

Nia yao ilikuwa nini?".

Nilimweleza yote waliyoniuliza.

Wakati namaliza kumweleza nilikuwa nataka kutoka barabara ya Upanga na kuingia nyumbani kwangu na kupeleka gari moja kwa moja gereji. Tukashuka nikafunga mlango wa gereji.

Karibu ndani vero.Hapa ndipo nyumbani kwangu".

Nilifungua mlango na kuwasha taa ya sebuleni halafu nikamkaribisha ndani akaketi kwenye

kochi.

"Asante lakini sitakaa sana, maana nasikia uchovu, nataka kurudi hotelini nikalale".

"Hakuna haja Vero nina mengi sana ya kukusimulia, maana hata sijakueleza yaliyotupata na Sherriff. Halafu..... nikasita kidogo".

"Halafu nini?", aliuliza kwa shauku.

"Halafu uliniahidi tulipokuwa Siera Leonee kuwa tutafahamiana vizuri zaidi Dar es Saalaam, lazima ujuwe kwamba ahadi ni deni".

"Haya baba umeshinda".

"Asante".

Nilichukua vinywaji ndani ya barafu, halafu nikamkaribisha katika chumba cha kulala. Nilizima taa sebuleni nikafunga mlango wa mbele, nikakagua vyumba vyote vya nyumba pamoja na madirisha na milango. Nilipoona kila kitu ni salama nilirudi chumbani nikafungua mlango wa maliwatoni, nikajaza maji kwenye karai la kuogea. Nilimwita Veronika aje tuoge. Tulioga pamoja na mtoto huyu mara moja nikasahau matatizo yangu yote na uchovu wote wa jioni ile. Baada ya kutoka maliwatoni tulikuwa tayari kulala.

"Haya nieleze sasa wakati tukipumzika", Veronika alisema huku amelala karibu yangu.

Nilizima taa yenye mwanga mweupe, nikawasha yenye mwanga wa bluu. Nikaleta chupa yenye whisky kwenye meza ya kitanda nikammiminia Vero ndani ya glasi nikaweka mawe ya barafu na mimi nikatengeneza yangu.

"Na tunywe kwa usalama wa maisha yetu wote".

Tulianza kunywa huku nikimweleza yote yaliyotupata. Baadae tukaelezana mambo yetu binafisi ambayo yalitufanya tujishitukie tumekumbatiana na kubusiana.

"Amka", Vero alinishitua, "ni saa mbili sasa.

Nilimwangalia Vero ambae alionekana kuwa alikuwa ameamka kitambo kwani alikuwa na sahani ya mayai ya kukaanga na vikombe viwili vya kahawa. Alikuwa amevaa pajama zangu; alitoa sura ya kuchekesha, hivyo nilimcheka, maana zilimpwaya sana.

"Unapendeza katika pajama hizo", nilimtania.

"Kwenda huko".

Mimi nikaangua kicheko, nikatoka kitandani na kukaa.

"Mwenzangu umelala fofofo leo. Mimi nimeamka nikafanya mazoezi kisha nimekwenda jikoni nikatayarisha chochote. Haya tunywe kahawa utoe usingizi", alisema huku akikaa karibu nami.

"Mimi naona nikaoge kwanza".

"Hapana. Tunywe kahawa kwanza halafu tutafanya mazoezi ya judo na karate ili niwe katika hali nzuri, halafu ndipo tutakwenda kuoga".

Basi tulikunywa kahawa na mayai ya kukaanga, halafu tukatoka nje uani kufanya mazoezi. Nyumba yangu ilikuwa imezungukwa na ua mzuri wa michongoma iliyokatwa vizuri na yenye urefu wa futi saba. Hivi ukiwa uwani kwangu mtu anayepita nje ya ua hawezi kuona kitu chochote kinachofanyika ndani. Basi tulifanya mazoezi ya karate na judo ya hali ya juu sana. Hii ilinihakikishia kuwa Veronika alikuwan na ujuzi wa kutosha. Ilibidi tu kumwonyesha kuwa mimi najua zaidi nilipomwingizia staili nyingine za pekee ambazo hutumiwa na wajuzi wa hali nya juu katika karate na kung-fu kama mimi, ambazo zilimshinda kuzifuata.

"Ujuzi wako unatosha kabisa Veronika. Naamini unaweza kupambana na mtu yeyote, na nina imani ni watu wachache sana wanaweza kukushinda katika karate na judo".

"Asante kwa pongezi laki. Lo, lakini wewe mwenzangu ni zaidi. Mitindo mingine unayotumia sikuwahi kuona hata kwa walimu wetu huko Japan. Ndio sababu wanasema ulipambana na Inoki na kutoka nae sare. Nilivyani walikuwa wanaongeza chumvi lakini sasa ninaamini ni kweli. Kokote nitakapotembea na

wewe hata pakiwa ni pa hatari namna gani sitaogopa kabisa maana nina imani kubwa katika uwezo wako kwa jambo lolote sasa".

"Asante".

Baada ya mazoezi tuliingia pamoja maliwatoni tukakoga.

"Mimi itabidi unipeleke hotelini nikabadili nguo. Angalia hizi zilivgyochafuka kwa ajili ya matatizo ya jana usiku!".

"Usiwe na taabu, lolote utakalosema".

Mimi nilibadilisha nguo, nikavaa vizuri kabisa kama mfanyabiashara. Nilichukua silaha tulizokuwa tumeziteka nikaziweka sehemu yangu ya siri ambako huweka silaha zangu na ni mimi peke yangu ninayepajua mahali hapo. Na hata ukiwa mtu wa namna gani huwezi kupagundua. Nilichukua silaha nyepesi kwa ajili ya siku hiyo kama litatokea jambo lolote. Nilimpatia Veronika bastola yenya sailensa. Nilipoona mipango yote nimekamilisha tuliondoka kuelekea Kilimanjaro hoteli. Ilikuwa saa tatu na robo tulipofika Kilimanjaro.

"Nenda kajitayarishe, kabla ya saa nne mimi nitakuwa hapa".

"Utanikuta tayari", Veronika alijibu.

Niliondoka na kuelekea ofisini. Nilimkuta Eddy nae anaingia. Alipoona gari langu akasimama mlangoni kunisubiri.

"Habari za leo bosi?".

"Nzuri Eddy, umelala salama kijana?".

"Ndio, bila taabu".

"Twende ofisini kwangu". Tulielekea ofisini kwangu. Tulimkuta Linda anazungumza kwenye simu. Alipotuona akasema, "Huyu ameingia", Akanipa simu huku akisema "Maselina huyo.

"Halo mrembo, habari za asubuhi?".

"Nzuri tu, wasiwasi kwako ambaye unalala mpaka saa tatu na waandishi wa habari".

"Mwongo, nani kakuambia huyo mwandishi kalala kwangu?".

"Nani hakujui, danganya wengine lakini miye baba unajua kabisa kuwa nakujua kama nyuma ya kiganja changu".

"Haya umeshinda wewe".

"Njoo Chifu anakuhitaji, anataka kujua umefikia wapi mpaka sasa".

"Haya nakuja, nitamweleza mpaka yeye atachoka".

"Haraka basi", alisema Maselina na kukata simu.

"Eddy jambo lolote juu ya Kiki?".

"Si nilikwambia nitakuwa na habari zote saa nne, na saa nne bado". Eddy alijibu.

"Oke, je juu ya bohari la Mamlaka ya Pamba umepata nini?".

"Walinzi wote wa bohari hilo wamekutwa leo asubuhi wameuawa huko Temeke. Inaonekana walilichukua bohari hilo kwa nguvu ili wafanyie kazi zao kwa muda tu. Kila kitu kingine ni salama. Polisi wanashughulikia hayo ya jana na kujaribu kutambua maiti walizozikuta hapo. Wao wanafikilia ni wezi. Gari walilotumia nalo lilikuwa limeibiwa".

Kisha nikamweleza yaliyokuwa yametupata na Veronika, baada ya kuachana nae jioni ile.

"Sasa fanya uchunguzi ujuwe watu hawa wamejiingizaje huko uwanja ya maonyesho ya Saba Saba, maana uwanja huo unalindwa na polisi masaa ishirini na nne!.

"Nafikiri mtindo wao ni ule ule. Wanaua walinzi na kufanya makao ya muda. Wakimaliza shughuli zao wanakwenda kuteka mahali pengine lakini hata hivyo vijana watachunguza".

"Oke, ngoja mimi nikamwone Chifu halafu tutaanza upelelezi wetu, kama kawaida utatufuata toka New Afrika kama jana, sawa>".

"Bila wasiwasi bos, kiijana ninayefuatana nae ni mzuri sana nafikiri hata nyinyi mlitupoteza".

"Ndio, kazi yenu ya jana ilikuwa nzuri sana, nilimpongeza.

"Bossi unapendeza sana leo".

"Asante sana kwa pongezi lako. Ngoja nikamwone Chifu".

Nilimwacha akiwa anataka kuzungumza mengi na mimi. Nilipanda ngazi na kuingia ofisini kwa chifu.

"Anatusubiri, amesema nichukue ripoti yako", Maselina alisema.

Basi tulifungua mlango na kuingia ofisini kwa Chifu. Chifu alikuwa amekaa kitini mwake akivuta mtemba kama kawaida yake.

"Shikamoo Chifu".

"Marahaba, ketini chini".

"Asante..."

Maselina alichukua kitabu chake cha hatimkato na kukaa tayari kuandika mazungumzo yetu".

"Ehee, nieleze kwa kirefu mambo ambayo umeishafanya. Maana huko makamo makuu ya Polisi kuna kelele, mauaji ya ajabu yanatokea mjini hapa kwa mara ya kwanza mpaka wameshindwa mahali pa kuanzia upelelezi. Nilipopata ripoti yao juu ya mauaji haya, nilihisi hii ni kazi ya Namba Moja. Kwa hiyo naomba maelezo kamili ili nami niweze kuieleza serikali maendeleo yoyote juu ya jambo hili maana kuna wasiwasi mkubwa. Jumuia ya Ulimwengu inaikera serikali kwa kutaka kujua ukweli wa jambo hili, na wakati huo huo maadui zetu wanaendelea kutupaka matope bila kupata ukweli wa jambo hili".

Nilichukua muda huu kumweleza yote tangu nilipotoka ofisini mwake; kwenda kwetu bandarini na ofisi ya Kamati ya Ukombozi, barua niliyoikuta mlangoni kwangu; mapambano dhidi ya waliomteka nyara Sheriff na mwisho walioniteka nyara. Nilimweleza kila kitu kwa ufasaha bila kuacha tukio hata moja. Huenda jambo nililoacha ni juu ya tuliyoifanya nyumbani kwangu na Veronika ambayo ni siri yetu hata nyinyi sitaki mjue.

"Kwa kutokana na maelezo ya mtu wa kikundi hiki kinachojiita 'Wanamapinnduzi wapinga mapinduzi' mimi naamini hawa watu ni VIBARAKA wa serikali ya makaburu ambao wanataka kupiga vita harakati za ukombozi dhidi ya serikali hizi dhalimu. Na mtu huyu niliyezungumza nae nina imani ni mtanzania kutokana na sura yake na sauti yake ingawaje alijitahidi sana kunidanganya kwa sauti.

Mimi ninavyofikiri kuna chama kimojawapo katika vyama vinavyopigania uhuru, ambacho makaburu wamekidanganya kuwa kikiweza kupiga vita harakati za mapambano ya silaha dhidi ya serikali ya Afrika Kusini itakipa mwanya chama hicho katika serikali ya makubaliano.

"Kwa hiyo chama hiki kimekubali kuwa kibaraka wa Afrika Kusini na kuanza vita dhidi ya vyama vingine vinavyoendeleza mapambano ya silaha. Kwa vile isingekuwa rahisi chama hiki kufanya mapambano bila msaada. Serikali ya makaburu lazima inakipa misaada ya kila hali, yaani wagtu, silaha na fedha. Kwa hiyo Chifu, ni imani yangu kuwa silaha hizi hazikibwa na watu wengine ila majasusi wa makaburu ili kutimiza lengo lao hilo'.

Chifu alikuwa ananiangalia kwa makini sana kisha akatingisha kichwa.

"Nimekuelewa vizuri sana Namba Moja. Hata unavyofikiri mimi naona ni sawa. Lakini tatizo letu liko pale pale; watu hawa wamejipenyezaje nchini humu na sasa silaha hizo ziko wapi?. Maana silaha hizo ni za kisasa kabisa. Hatua uliyofikia kwa siku moja inaridhisha, tafadhali kazana zaidi katika masaa ishirini na manne yajayo tuwe na fununu zaidi.

"Hapa tuna vyama viwili, PLF na SANP na vyama hivi ndivyo vinaendesha mapambano ya silaha huko Afrika Kusini. Kwa hiyo tuna chama kimoja ambacho kiko nje ya nchi hii; ama kiko Afrika ya Kusini ama katika nchi jirani na ndicho kimejipenyeza kuvipiga vita hivi vyama viwili".

"Hata mimi nafiri hivyo. Kwani kuna vyama vingapi vinavyopigana na serikali ya Afrika Kusini?".

"Viko vingi, kati ya hivyo vitatu viko Afrika Kusini na vitano viko nchi ya nje, kwa hiyo jumla ni vinane".

"Hili ndilo tatizo la vyama vingi. kingekuwa chama kimoja yote haya yasingetokea", nilisema kwa huzuni.

"Siasa kijana, wanasiasa ndio wanaleta taabu ulimwenguni; ndio wanayumbisha vichwa vyetu. Kila mtu na siasa yake na imani yake, na kuna wengine hawana cha siasa wala cha nini; nia yao kutaka ukubwa ili wale", alijibu Chifu kwa uchungu mkubwa.

"Sawa, sisi tunaendelea na upelelezi wetu na ushauri wako nitauweka manani".

"Asante sana Namba Moja".

"Polisi wamefikia wapi?".

"Polisi hawajafika popote. Sasa ndio wamechanganyikiwa zaidi baada ya mauaji haya ya usiku. Hivyo mimi nakutegemea wewe, maana umefanya maendeleo mazuri".

Nilisimama nikampigia kope Maselina nae akaminyia midomo kuzuia tabasamu alilotaka kunipa. Chifu alinifungulia mlango na kuniambia. "Nakutakia mafanikio katika kazi hii kijana".

"Asante Chifu", nilijibu kisha akafungua mlango.

"Kavae upesi twende zetu Komredi", nilimwambia Sherriff aliyetaka kubadilisha nguo.

"Dakika tano tu", alijibu kisha akaenda haraka haraka.

Ilikuwa saa tano tulipofika New Afrika baada ya kumchukua Sherriff kutoka kwa daktari akiwa anajisikia vizuri kabisa. Veronika ndiye nilikuwa nimewahi kumchukua kabla ya Sherriff.

"Kavae upesi, twende zetu Komredi", nilimwambia Sherriff aliyetaka.

"Dakika tano tu", alijibu kisha akaenda haraka haraka.

SURA YA NANE

ILIKUWA saa tano na dakika kumi na tano tulipoondoka kuelekea Ofisi za PLF. Njiani tulimweleza yote yaliyokuwa yametupata jioni ile tukibakiza tu ile habari ya kwenda kwetu pamoja kulala nyumbani kwangu.

Ofisi za PLF zilikuwa mtaa wa Makunganya karibu na Achells Limited hivyo haikutuchukua muda kufika pale kutokea New Afrika. Tulitokea barabara ya Azikiwe, tukaingia mtaa wa Independence pale kwenye mzunguko wa sanamu ya Askari halafu tukakata kulia pale kwenye taa za usalama barabarani za mtaa wa Independence na Postway, na kuingia Postway. Tukatelemka kidogo mpaka kwenye mtaa wa makunganya moja kwa moja kwenye ofisi za PLF. Tuliegesha gari pale pale mbele ya ofisi tukatelemka na kuingia mapokezi. tulimkuta kijana mmoja akiwa mapokezi.

"Habari zako ndugu", nilimsalimu.

"Salama, sijui niwasaidie nini?".

"Tunaomba kumwona ndugu Cecil Chimalamo".

"Mna miadi naye?".

"Hapana, lakini ukimweleza kuwa kuna waandishi wa habari toka gazeti la Afrika natumaini anaweza kutuona".

"Subirini hapa kwenye viti".

Tulikaa kwenye makochi mazuri sana. Cecil Chimalamo nilikuwa ninamfahamu kwa sura na vile vile mambo yake kwani nilikuwa nimeshasoma faili lake mara nyingi ofisini. Kwa kifupi wanasiasa wengi walimpenda kwa sababu ya imani zake za kisiasa ambazo mara nyingi zilikuwa na msimamo. Alitambulikana kama kiongozi mmojawapo mashuhuri mpinga ubaguzi na mpenda serikali ya wengi katika Afrika ya Kusini, makaburu walimchukia sana.

Punde yule kijana alirudi akayakatisha mawazo yangu juu ya Chimalamo.

"Mnaweza kumwona chumba namba tatu".

"Asante", nilishukuru kwa niaba ya wenzangu.

Tulikwenda moja kwa moja mpaka chumba namba tatu tukabisha hodi.

"Karibu".

Nilifungua mlango tukaingia ndani tukajikuta katika ofisi.

"Karibuni", alitukaribisha huku akisimama.

"Asante".

"Nyinyi ndio mmetoka kwenye ofisi za gazeti la Afrika".

"Ndio".

"Twendeni mzee anawasubiri".

Alifungua mlango, tukaingia ndani na kumkuta ndugu Chimalamo amekaa anavuta sigara. Alipotuona alisimama.

"Karibuni, ketini chini".

Kabla hatujakaa nilichukua mwanya huu kujijulisha mimi pamoja na wenzangu kwake.

"Mimi naitwa Willy Gamba na ni Meneja Mkuu wa Kampuni iitwayo Afrika Internation Agencies (AIA), na hawa ni waandishi wa gazeti la Afrika. Huyu anaitwa Veronika Amadu na huyu ni Ahmed Sherriff. Wote ni wananchi wa Sierra Leonee", tulishikana mikono na kusabahiana halafu tukaketi chini.

"Imekuwaje wewe uwe pamoja nao?", aliuliza.

"Kampuni yangu ndiyo wakala wa gazeti la Afrika hapa Tanzania kwa hivyo haja zao zote naziwakilisha mimi.

"Aisii, nafikiri tumeshaonana mara nyingi. Wewe si mgeni kabisa kwangu ", aliniambia na kuniangalia kwa macho ya kudadisi.

"Bila shaka tumeonana mara nyingi hasa katika tafrija za vyama hivi ingawaje hatujawahi kujulishwa moja kwa moja".

"Ehe gazeti la Afrika linataka nini?", Nilishangaa sana maana hata hakuuliza vitambulisho. Mara moja nikajua mtu huyu aliweza kuwasoma watu na kujua ni watu wa namna gani. Alikuwa mtu mwenye busara nami nikaondokea kumpenda.

"Sisi tumekuja hapa mjini baada ya kupata habari za tukio lililokikabiri chama chako na serikali ya Tanzania kwa ujumla. Jumuiya ya Ulimwengu mpaka sasa imegawanyika katika pande mbili. Moja inalaumu Serikali ya Tanzania kuwa ndiyo inahusika na wizi wa silaha hizi ambazo ni za kisasa kabisa, upande wa pili

unaamini kuwa hizi ni njama za mabeberu zinazopiga vita harakati za ukombozi wa Afrika Kusini. Kwa hiyo gazeti la Afrika likiwa kila siku linafuatilia kwa makini harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika na kuweza kusaidia inapowezekana, linahitaji hasa ukweli wa tukio hili. Hii ndio sababu tuko hapa. Tumeshawaona wakuu wengine katika OAU na katika Serikali ya Tanzania na tumeona hatuwezi kufika mbali bila kujua mawazo yako wewe ambaye ndiye hasa uliyehusika na mali iliyopotea", Sherriff alieleza kwa kinagaubaga.

"Kwa hiyo mnataka kujua mimi niko upande gani katika mawazo hayo mawili ya Jumuiya ya Ulimwengu?".

"Hilo ndilo swali letu la kwanza", Sherriff alijibu.

"Mimi nawaunga mkono wanaoamini kuwa hizi ni njama za mabeberu. Wale wanaosema Tanzania inahusika wanajaribu kuongeza petrol kwenye moto huku wakijua kuwa Tanzania ni nchi pekee katika Afrika ambayo haiwezi kufanya jambo hili. Nakuhakikishia kwamba tangu nikae hapa nina miaka sita na sijaona Serikali ya kimapinduzi kama hii. La hashi, Tanzania haiwezi kabisa kufanya jambo hilo ila hizo ni mbinu za mabeberu za kutugonganisha sisi na wenyeji wetu ili mambo yaharibike kabisa. Mimi sitakubali washenzi hao watugonganishe. nafikiri umenielewa.

"Nimekuelewa sana. Sasa unafikiri silaha hizi zimepotea poteaje?. Hapa nataka mawazo yako binafsi".

"Hata mimi sijui. Ni njama ya hali ya juu iliyofanyika, hivyo nimeachia shauri hilo Serikali ya Tanzania ambayo imeniahidi itafanya juu chini kufichua njama hizi".

"Na isipowezekana?", Veronika aliuliza.

"Tutajua la kufanya wakati huo.

"Ilibainikaje kama wewe umekwenda Urusi kutafuta silaha za kisasa na hali naamini jambo hili lilifanywa kwa siri?", Sherriff aliuliza.

"Siku hizi hakuna kitu cha siri. Nafikiri hata kabla sijaondoka hapa Dar es Salaam kwenda Moscow ilikuwa imeshajulikana nini nafuata. Ulimwengu huu wa teknolojia hakuna kitu cha siri. Hata mkutano uliofanyika huko camp Davis Marekani, kati ya Marais wa Israel, Misri na Marekani na kuweka hali ya uficho wa hali ya juu, bado watu walijua kabla mazungumzo hayo ya kisiri ya hali ya pekee hayajatangazwa rasmi. ili kujibu swali lako hata sisi hatukutegemea tutajulikana.

"Watu wanafikiri kuwa, silaha hizo zimefanyiwa njama za kuibiwa kwa sababu ni silaha za kisasa kabisa na za hali ya juu. Ndio sababu watu wanasema Tanzania isingeweza kuziona zinakwenda hivi hivi. Sasa swali langu ni kwamba kwa nini uliamua kuomba silaha za kisasa za jinsi hii wakati vita havijafikia hali ya juu sana kuhitaji silaha za namna hiyo.

"Ahaa, swali lako zuri sana. Ili mwelewe kwa nini nilichukua hatua hiyo ni lazima niwape maelezo kamili, juu ya hali ya silaha alizonazo adui tunayepigana naye", alinyamaza kidogo akaegemeza mikono yake mezani.

"Maana mtu hawezi kupigana kwa rungu dhidi ya mtu mwenye bunduki. Kwa hiyo hamtajali naona nikiwaeleza kwa kirefu jinsi wapinzani wetu walivyojidhatiti kijeshi na ndipo tu mnaweza kuona kwa nini niliagiza silaha za kisasa".

"Sisi tutafurahi sana kupata fursa ya kusikia maelezo hayo", nilijibu kwa niaba ya wenzangu.

"Katika miaka 15 iliyopita", alieleza Chimalamo. "Makampuni ya kimataifa yamezidisha rasilimali zao ili kuimalisha uchumi wa Afrika Kusini. Makampuni makubwa ya Marekani na Ujerumani Magharibi yamepanua rasilimali zao katika sehemu muhimu za utawala wa Makaburu. Na makampuni haya yana ushirikiano mzuri sana na utawala wa Makaburu.

"Miaka michache iliyopita mabenki ya kigeni yameikopesha afrika Kusini mamilioni ya fedha ili kuwezesha kukabili migogoro ya kiuchumi iliyosababishwa na kulegalega kwa uchumi wa nchi za magharibi na kuendelea kukua kwa mapambano ya wazalendo wanaokandamizwa na utawala wa Makaburu.

"Mabenki ya kigeni yametoa mtaji mkubwa kwa utawala wa Makaburu kwa mahitaji ya fedha kwa ajili ya mambo ya kijeshi na kiuchumi, katika miaka michache iliyopita deni la kigeni la Afrika Kusini limeongezeka haraka kufidia gharama za mafuta yake, kupanua ununuzi wa silaha na gharama za mipango ya kuuwezesha utawala huo dhalimu ujitegemee. Kwa taarifa yenu mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka 1976 utawala wa Makaburu ulikuwa na deni lipatalo Shs.72 bilion, lakini idadi inaweza kuwa kubwa kuzidi hapo maana mikopo kwa Afrika Kusini ni siri. Sijui mnanielewa?".

"Tunakuelewa sana", tulijibu kwa pamoja, huku Veronika akiwa anaandika maelezo hayo.

"Kuna ukweli unaoonysha jinsi biashara ya makampuni ya kigeni na rasilimali zao zilivyosaidia kuimarisha viwanda vya kijeshi vya Afrika Kusini hata kuuwezesha utawala wa Makaburu kuwa na kiburi na kupuuza maoni ya dunia na kuendelea kudumisha udhalimu wake na kuwakandamiza wananchi walio wengi wa Afrika Kusini.

Makampuni ya kigeni yamejikusisha moja kwa moja katika kuimarisha kijeshi Afrika Kusini. Kumbukumbu za kampuni moja inayoshughulika na utengenezaji wa silaha katika nchi zinazoendelea zinaonyesha kuwa makampuni ya kigeni yametoa liseni kwa makampuni ya Afrika Kusini kutengeneza zana za kijeshi za aina mbali mbali, pamoja na ndege za kijeshi, mabomu, risasi na bunduki. Vile vile kuna makampuni yanayotengeneza vipuri na vifaa vingine kwa madhumuni ya kijeshi. Shirika la Baruti na madawa la Afrika Kusini 'AECI' linatajwa kuwa linamiliki viwanda vitatu vinavyotengeneza silaha na linashirikiana na kampuni moja ya viwanda vya madawa ya Uingereza. "Imperial Chemical Industries", Kampuni hiyo ya Uingereza., imetoa utaalamu na vifaa vinavyotumiwa na Shirika la AECI la Afrika Kusini. Na wakati huo huo kampuni ya Darman Long ya Afrika Kusini iliyounda manowari moja yenye uzito wa tani 220 inashirikiana na Shirika la vyuma linalomilikiwa na serikali ya Uingereza katika shughuli za utengenezaji silaha".

Alinyamaza kidogo, akachukua sigara akaiwasha kisha akavuta mara tatu hivi halafu akaendelea.

"Kutokana na misaada hii toka nchi za Magharibi, Afrika Kusini imejiimarisha sana kijeshi. Utaona kuwa miaka ya sitini, matumizi ya kijeshi ya Afrika Kusini yameongezeka mara sita kutoka Shg 520 milioni hadi mwaka 1977/78 matumizi ya kijeshi yalikuwa yameongezeka tena na kufikia kiasi cha Shg 16,450/- milioni kwa mwaka. Nimetoa maelezo hayo pamoja na tarakimu ili kuwaonyesha kimsingi kuwa Afrika Kusini ina uwezo kifedha kutengeneza au kununua silaha za kisasa kabisa.

Alitua tena ili kuvuta sigara yake kisha akaendelea huku sisi tukimsikiliza kwa makini kama wanafunzi wanavyomsikiliza mwalimu katika somo wanalolipenda.

"Vijana lazima mtu ujue nguvu za adui yako kabla hujamkabili, la sivyo, utakuwa unafanya mapambano yasiyo ya kimsingi. Ili kuwapa ukweli hasa uliopo, jeshi la Afrika Kusini limekuwa likitumia zana za kisasa zilizoko duniani tangu mwaka 1970. Matumizi ya kijeshi kwa ajili ya kununulia silaha na vifaa maalumu vya kisasa vya kijeshi badala ya vya zamani yaliongezeka kwa asilimia 32 mwaka

1971 kufikia asilimia 53 mwaka 1973. Kati ya mwaka 1970 na 1979 Shg 2,240 milioni zilitumika kwa mambo ya ndege za kijeshi, shs 1,000/- milioni kwa ajili ya kununua radio, mitambo ya kutazama ndege angani (radar) na vifaa vingine vya kisasa. Kama nilivyokwisha kuwaeleza hapo awali, wakati huo huo utawala wa Afrika Kusini umekuwa ukichukua hatua kuimarisha utengenezaji wa zana humo humo nchini kadiri vipuli na vifaa vya mahitaji yake ya kijeshi yanavyozidi kuongezeka.

"Kwa mjibu wa toleo moja la kijeshi la Marekani, tangu tangu mapema mwaka 1971 makaburu walikuwa wanaweza kutengeneza mabumu na baruti kiasi cha kujitosheleza na wanaweza kuuza nchi za nje. Juu ya risasi Afrika Kusini inatengeneza aina 100 za risasi. Kwa bunduki inajitosheleza kabisa. Kwa silaha za jeshi la nchi kavu, ama imejitosheleza ama imefikia hatua za utoaji, na itajitosheleza hivi karibuni kwa zana za jeshi la maji na sasa inatoa zana zote za moto inazohitaji. Bunduki za kisasa kama vile Rifle na Machine-gun vile vile zinatengenezwa. Hivi utengenezaji wa mizinga unaanza, na kuna huduma ya kuweza kutengeneza karibu kila aina ya magari ya kijeshi. Radio za ndege, vifaa vya kutegulia mabomu na vifaa vingine vya kisasa vya kijeshi vinabuniwa na kutengenezwa huko huko Afrika Kusini.

Alinyamaza na kuwasha sigara nyingine na kwa nguvu zile zile akaendelea kueleza.

"Hivi karibuni ilidokezwa kuwa Afrika Kusini inaunda aina fulani za bunduki, mabomu ya kudondoshwa na ndege yenye uzito wa kufikia ratili 1,000 kila moja na inaendelea na utengenezaji wa makombora ya kuangusha ndege. Mabomu hayo inasemekana yalifanyiwa majaribio mwezi Septemba 1977 kwa kutumia ndege za aina ya 'Mirage'. ndege hizi za mirage zilianza kuundwa huko Afrika Kusini chini ya liseni ya kampuni ya ufaransa ya Sessoult mnamo mwaka 1974. Kama hatua ya mwanzo. Afrika Kusini ilinunua vipande 50 vya ndege za aina hiyo na kuunda yenyewe ndege za mirage".

"Wakati huo vile vile ilikuwa tayari imeanza kuunda ndege za kijeshi aina ya Impala za muundo wa Italia-Armachi MB-326, magari ya kijeshi aina nyingi ya silaha ndogo ndogo pamoja na bunduki za aina ya rifle muundo wa Ubelgiji. Na kwa mjibu wa Waziri wa Ulinzi wa Makaburu. Afrika Kusini ilitegemewa ianze kutengeneza vifaru vyake. Vile vile Afrika Kusini inasemekana imeanza kuendeleza utengenezaji wa mizinga ya kutungulia ndege aina ya CAC-TUS, ikisaidiwa na kampuni moja ya Ufaransa".

Alipofika hapa aliinua simu na kumwamru mwandishi wake mahsusi atuletee vinywaji baridi na sambusa kisha akaendelea.

"Naona nitawachosha lakini kwa sababu nyie wenyewe mmeuliza mimi nitawapa hali halisi ilivyo na mkiwa kama waandishi wa habari ni vizuri kujua hali ya kijeshi ya huyu adui wetu mkubwa katika Afrika. Kwa kutumia gazeti lenu mnaweza kujulisha jumuia ya ulimwengu ukweli wa nguvu za adui yetu huyu zilivyo, hivyo msitahimili karibu nitamaliza.

Mwandishi wake alileta vinywaji barudi na sambusa.

"Habari unazotueleza ni za kosisimua mno kwani kwetu sisi wengine ni habari mpya, hivyo hata ukiendelea mpaka usiku tutakuwa tayari kabisa kukusikiliza", nilimhakikishia.

"Kama hivyo basi nitaendelea. Magari ni muhimu sana katika mambo ya kijeshi. Kuna makampuni kadha wa kadha ya kigeni ambayo yamekuwa yakiisaidia Afrika Kusini kijeshi katika mambo ya magari. Makampuni hayo ni pamoja na kampuni ya Marekani ya General Motors (GM), kampuni kubwa duniani inayotoa magari kwa wingi baada ya Vita Kuu ya kwanza. Hivi sasa ina mtambo wa kuunganisha na kuunda magari huko Port Elizabeth, na mtambo wa kutengeneza injini za magari nje kidogo ya mji huo.

"Kampuni nyingine ya magari ni ile ya Ujerumani inayotengeneza magari ya aina ya 'Benz'. Magari ya kijeshi ya aina hii ndiyo yanatumiwa sana na majeshi ya Afrika Kusini. Msemaji mmoja wa kampuni ya magari ya Benz na BMW, alijigamba hivi karibuni kwamba kampuni yake inatengeneza magari hayo Ujerumani kwenyewe na Afrika Kusini na inakusudia kutumia Afrika Kusini kama kituo cha kuuzia magari hayo kwa nchi za nje zilizoko Kusini kwa Ikweta. Hii inaonyesha dhahiri kuwa Afrika Kusini inayo magari haya zaidi ya mahitaji yake ya kijeshi".

Alinyamaza tena akachukua glasi yake iliyojaa Coca-cola akainywa kwa mara moja kisha akainua macho yake na sura yake ikageuka kuwa nzito kisha akaendelea.

"Na mwisho napenda kuwaeleza jambo la mwisho lakini muhimu si kwa sisi wapigania uhuru tu bali kwa Afrika nzima. Katika mwaka 1974 Shirika la Nyuklia la Marekani lililoko Oak Ridge lilipeleka kilo 45 za madini ya 'Uranium' kwa mtambo wa utafiti wa nyuklia uliopo Palandaba huko Afrika Kusini baada ya Tume ya Nyuklia, chombo pekee cha Marekani kinachotoa liseni za usafirishaji nje

vifaa vya nyuklia kukubaliana na Afrika Kusini kwamba haitaruhusu madini hayo yapelekwe pengine au kutumiwa vinginevyo. Marekani vile vile mwaka 1975 na 1976 iliipa Afrika Kusini madini hayo yanayotumiwa kutengeneza zana za nyuklia na kuahidi kuuza zaidi madini hayo kwa mtambo wa pamoja na nguvu za nyuklia wa Marekani na Ufarasa unaotazamiwa kujengwa Afrika Kusini mwaka 1984. Kwa jumla Marekani imeiuzia au imeahidi kuiuzia Afrika Kusini ratili 300 za madini hayo kwa ajili ya mtambo wa utafiti wa nyuklia uliopo Palandaba. Kwa taarifa yenu ratili 300 za Uranium zinawza kutengeneza mabomu 15 ya Atomiki".

Kila mmoja alipiga mluzi wa mshangao.

"Nafikiri ndugu Willy nimejibu swali lako kwa kirefu, kwa hiyo utaona sisi wapigania uhuru hatuna budi kuomba silaha za kisasa zinazoweza kukabili nguvu hizi kubwa ya kijeshi za adui yetu. Kwa hiyo tukio hili lililotokea linaonyesha dhahiri kuwa hawa makaburu wameona hatari inayowajia hivyo kuiba silaha hizi ni mbinu moja ya kujihami. Na mimi nimeapa sitarudi nyuma nitaondoka tena karibuni kwenda kutafuta silaha za kisasa na kali toka nchi rafiki ambazo naamini zitaamini kuwa tukio hili ni njama za mabeberu. Hivyo njama zao zinazidisha tu moto katika wapigania uhuru na ndugu zao wanaowasaidia. Huu si mwisho wa mapambano. Ila ni matayarisho tu ya mapambano - historia itanihukumu. Mna swali zaidi?".

Tuliangalia na kukawa hakuna mtu mwenye swali kwani risala yake ilituchoma mioyoni kama miali ya moto wa umeme.

"Asante, tumetosheka", nilijibu kwa niaba ya wenzangu.

"Oke mnakaribishwa tena siku yoyote kwani katika kuzungumza nanyi ndipo tunapoweza kujua hali halisi ya Kusini mwa Afrika. Asante sana vijana wa Afrika kuja kunitembelea". Alitupa mkono wa kuagana.

"Asante sana", tulijibu na kuondoka ofisini mwake kimya kimya.

Tulipofika kwenye gari langu niliona ni saa saba u-nusu, kweli tulikuwa tumekaa sana ndani. Tuliingia ndani ya gari.

"Sasa twende tukaonane na Ray Sikazwe. Rais wa Chama za SANP

Ofisi za SANP zilikuwa barabara ya Umoja wa Mataifa baada ya kuvuka barabara inayoingia Hospitali ya Muhimbili. Hivyo niliendesha moja kwa moja na kuingia barabara ya Morogoro kutokea mtaa wa Makunganya. Tulipofika kwenye taa za usalama barabara za Jangwani, nilikata kulia na kuingia barabara ya Umoja wa

Mataifa. Nilisimamisha gari karibu na mlango wa ofisi kwani kwa upande mwingine wa barabara kuna gereji na magari yalikuwa yamejaa kibao.

Tuliingia mapokezi na kumkuta binti mmoja anajipaka poda usoni. Alipotuona akaweka mkebe wa poda kando, alijifuta vizuri usoni halafu akatutolea tabasamu.

"Karibuni".

"Asante. Hujambo binti?".

"Mimi sijambo, sijui niwasaidie nini?".

"Tunaomba kuonana na Ndugu Sikazwe.

"Mna miadi naye?".

"Hapana".

"Basi hawezi kuwaona, ana kazi nyingi sana. Huenda mnaweza kumwona ndugu Amos Shumka ambaye naye ni ofisa katika ofisi hii".

"Wewe ni Mtanzania?".

"Ndio".

"Basi dada sisi hatutaki kumwona mtu mwingine ila ndugu Sikazwe".

"Basi kaka yangu, ndio huwezi kumwona leo. Amesema hawezi kumwona mtu yeyote hata awe nani kama hana miadi naye. Mimi ninatii amri ya wakubwa wangu kwa hiyo siwezi kufanya vinginevyo".

"Jaribu kumpigia simu umwambie sisi tunataka kumwona tunatoka gazeti la Afrika, mwache yeye aamue".

"Hata kama mnatoka katika gazeti la dunia, siwezi", alichukua rangi ya midomo na kuanza kujipaka.

"Naona tumenoa", alisema Veronika.

"Basi, tutajipeleka wenyewe, twendeni", niliwaambia wenzangu.

Yule msichana alisimama na kututangulia haraka haraka na kuelekea kwenye ofisi moja huku uso wake umejaa hasira. Na sisi tukamfuata mbio mbio nyuma. Alipofungua mlango wa ofisi hiyo tu na sisi tukaingia.

Hawa watu nimewakatalia kumwona mzee lakini wamekuja kwa mabavu", alimweleza msichana mwingine aliyekuwa anapiga taipu. Kabla yule msichana

hajajibu mimi nilipita mbele na kufungua mlango wa ofisi ya ndugu Sikazwe kwani bila huyu msichana kujua alikuwa ametuelekeza mwenyewe. Wasichana wote wawili walibaki wameshikwa na butwaa na kushika midomo yao. Mimi nilifungua mlango na wote watatu tukaingia ndani. Tulimkuta Ndugu Sikazwe anazungumza kwenye simu, na alipotuona tunaingia mara moja alikata simu na sura yake ikawa na hasira.

"Nani amewaruhusu kuingia ofisini mwangu kwa kikuku namna hii?"

"Samahani ndugu Sikazwe. Sisi tunatoka kwenye ofisi za gazeti la Afrika na tumekuja kukuona kwa jambo la maana sana kuhusu wewe na Afrika nzima. Sasa tulipofika hapa ofisini kwako mzee, msichana wa mapokezi akatukatalia tusikuone. Kwa sababu sisi tuna uhakika kuwa ungeturuhusu tuonane nawe, tumeona hatuna budi kufanya jambo lililo la busara, ambalo ni kujileta sisi wenyewe tukiwa na imani kubwa kuwa utatuona. Naamini umeelewa kwa nini tumechukua hatua hii, na ukiwa kiongozi mmojawapo mwenye busara kati ya viongozi wa vyama vya wapigania uhuru wa Afrika Kusini tuna imani utatupokea kwa mikono miwili. Jambo lililotuleta si jambo la kitoto", nilimweleza kwa utaratibu sana.

Ghafla uso wake ukabadilika. Tabasamu kubwa likaonekana usoni mwake naye akasimama.

"Samahani sana ndugu zangu katika jina la Afrika huru, naamini mtawasamehe hao wasichana pamoja na mimi, kwani ilibidi kutoa amri hiyo kwa sababu sasa hivi nashughulikia tukio ambalo limetokea hivi karibuni ambalo limevuruga vichwa vyetu. Msiwe na wasiwasi jioneni kama halikutokea jambo la kuwaudhi. Karibuni tuendelee na shughuli zilizowaleta".

Baada ya maelezo haya tulipeana mikono tukajulishana kisha tukaketi chini tayari kwa mazungumzo.

"Nafikiri ndugu Gamba tumewahi kuonana?", aliuliza.

"Ndio tumewahi kuonana kwenye tafrija nyingi".

"Umesema kampuni yako ndio wakala wa gazeti la Afrika hapa Tanzania?"

"Ndio".

"Aisee, haya mimi niko tayari tuendelee na mazungumzo yaliyowaleta".

Veronika alikohoa kuliweka koo lake vizuri kabla hajaanza kusema. Alipokuwa tayari alichukua uwanja.

"Gazeti la Afrika ni gazeti ambalo limekuwa na litazidi kutetea mapambano ya Kusini mwa Afrika. Hivi majuzi tumesikia tukio lililotokea hapa mjini, ambalo sisi tumelichukua kama pigo kubwa sana kwenye harakati za ukombozi wa Kusini mwa Afrika. Ndio sababu tuko hapa ili tuweze kuzungumza na viongozi wa Serikali ya Tanzania na Maraisi wa vyama vya wapigania Uhuru walioko hapa nchini hivyo tuweze kupata mwanga wa jambo hili. Kumekuwa na uvumi wa kutatanisha ulimwengu mzima juu ya tukio hili.

"Kuna mambo mawili yanazungumziwa. Jambo la kwanza ni kwamba tukio hili limetokana na njama za mabeberu za kutaka kuzima harakati za ukomboni Afrika Kusini na ndiyo sababu silaha hizi zimeibiwa. Wengine wanalaumu serikali ya Tanzania kuwa ndiyo iliyofanya njama hizi kwani silaha zilizokuwa zimekuja. Serikali yoyote hata iwe ya kimapinduzi namna gani ingeweza kupata kishawishi cha kuchukua silaha hizi kwa manufaa yake. Sijui wewe una mawazo gani juu ya jambo hili", Veronika aliuliza baada ya kutoa maelezo haya marefu.

"Kusema kweli mimi bado nimechanganyikiwa juu ya tukio hili. Mambo yote haya mawili nimeyasikia lakini bado mimi sijasikia uamuzi jambo lipi ni sawa. Kama mlivyonikuta hata mimi najaribu kuzungumza na maofisa mbali mbali wa serikali ya Tanzania na Ofisi ya ukombozi ya OAU ili na mimi nipate msimamo wangu. Tukio hili si la kukimbilia kuamua".

"Kwa hiyo tuseme una wasiwasi kuwa huenda ikawa kweli Serikali ya Tanzania ikawa inahusika?", aliuliza Veronika huku macho yake yakimwuliza Sikazwe.

"Sikazwe alisita kidogo akajaribu kukwepa macho ya Veronika.

"Sina wasiwasi na Serikali ya Tanzania kuhusika na tukio hili, lakini ili niwe na uhakika vile vile ni lazima nichunguze upande huo vile vile. Msinieleme vibaya, mimi ni mtu ambaye mara kwa mara hupenda kuchunguza mambo na nipatapo ukweli nang'ang'ania kwenye ukweli. Sijui mumenielewa?".

"Mimi nimekuelewa kuwa utakuwa na uhakika tu kuwa Tanzania haijahusika utakapopata ukweli wa jambo lilivyo", Veronika alijibu.

Sikazwe alisita tena.

"Kitu kama hicho. Mnajua sisi wapigania Uhuru tuko katika hali ya kutatanisha sana. Kwa sababu serikali za nchi huru za Kiafrika unakuta moja inapendelea chama hiki nyingine chama kile maana sisi tuko vyama vingi. Hivyo ili kuamua jambo hili ni lazima uangalie mambo mengi", alijibu.

"Kama nimekuelewa vizuri unatupa tena hali ya tatu kuwa huenda si Tanzania wala mabeberu waliohusika katika njama hizi ila inaweza kuwa nchi mojawapo katika nchi huru za Kiafrika", nilisema.

"Nafikiri sasa umenipata".

Sisi tuliangaliana kwa mshangao kwani fikra hii ilikuwa haijaingia vichwani mwetu.

"Vizuri tumejua msimamo wako", nilijibu.

"Kwa hiyo ili niweze kuwapa msimamo wangu kamili mnipe muda ili niweze kutuliza mawazo yangu baada ya kuzungumza na watu fulani".

"Unamjua kijana mmmoja aitwae George Kiki", Sherriff aliuliza.

Sura ya Sikazwe ilionyesha mshituko ambao ni mtu kama mimi tu ambaye angeweza kuona.

"Ndio ninamkumbuka aliwahi kuja hapa ofisini kwangu akiwa mkimbizi kutoka Afrika Kusini baada ya matatizo ya Soweto. Na sisi huwa ni wajibu wetu kama chama cha wapigania uhuru kuwasaidia. Tokea siku hiyo mpaka leo sijapata kumwona tena. Je ana nini?".

"Amekutwa ameuawa nyumbani kwake", Sherriff alimjibu.

Sikazwe alionyesha hali ya mshangao.

"Nimesikitishwa sana; alionekana kijana mzuri".

Simu ililia Sikazwe akaichukua.

"Sikazwe hapa".

Akaisikiliza kwa muda halafu akajibu. "Sawa, nakuja sasa hivi".

Akakata simu.

"Sijui mna maswali zaidi maana nahitajiwa ofisi za Ubalozi wa Botswana kwani kesho kutwa nina safari ya kwenda huko kuonana na wanachama na wanajeshi wangu walioko huko".

Tulitazamana tukaona hakuna zaidi.

"Nafikiri inatosha, tukikuhitaji naamini utakuwa tayari kutuona kabla hujaondoka".

"Bila shaka".

Tulisimama, tukapeana mikono na tukaagana. Tulitoka na kuingia ndani ya ofisi ya mwandishi wake.

"Hujambo mrembo, maana hatukusalimiana wakati tunaingia kwani tulikuwa katika haraka", nilimsalimu.

"Mimi sijambo", alijibu huku bado anatuangalia kwa macho ya kushangaa.

Tulimwacha ashangae tukatoka nje ya ofisi na kuelekea mapokezi. Hapo tulimkuta yule msichana.

"Siku nyingine ukitukatalia utafukuzwa kazi. Angalia vizuri sana sura hizi maana sidhani utapata kazi mahali pengine wanakochukua muda kujirembua wakati wa kazi. Hivyo chungu kazi yako", nilimshauri.

"Si nikikosa kazi kwa sababu yako nitakutafuta".

"Nani atataka msichana wa kujirembua huku chungu jikoni kinaungua nyumbani kwake?".

Msichana yule alivimba, tukaona tuondoke kabla hajapasuka. Tulipotoka nje tulielekea moja kwa moja kwenye gari letu tayari kwa safari ya mjini. Ghafla nikasikia sauti.

"Bosi, rukeni ua".

Kama umeme tuliruka na kuanguka chini upande mwingine wa ua wakati ambapo risasi zilimiminika pale pale tulipokuwa tumesimama.

"Nenda ofisini", tulisikia sauti ya Eddy ikiamru.

Kama umeme tuliruka na kuangukia mapokezi wakati tuliposikia mlipuko mkubwa wa bomu uliotingisha hata ofisi za SANP.

Baada ya dakika-mbili hivi Eddy alisimamisha gari lake mbele ya mlango na kuamru twende. Kama risasi tuliingia ndani ya gari na kuondoka kasi na kuacha gari langu likiwa limesambazwa vipande vipande.

SURA YA TISA

BINTI TANZANIA

"Lo, hiyo ilikuwa alimanusura", Veronika alisema huku jasho likimtoka na akihema.

"Nakuambia", Sherriff naye huku akihema.

"Eddy, moja kwa moja nyumbani kwangu, akili yangu imevurugika", nilimwambia Eddy aliyekuwa akiendesha kwa kasi sana.

"Huyu Eddy ni nani na katokea wapi?, maana bila yeye sasa hivi sote tungekuwa maiti", aliuliza Sherriff.

"Katika kazi hizi Komred Sherriff lazima uwe na plani bila plani huenda mimi ninge kuwa nimeuawa siku nyingi. Huyu kijana ni mfanyakazi mwenzetu, na toka asubuhi yuko pamoja nasi lakini kazi yake ilikuwa ni kutulinda sisi. Na kwa jumla ndivyo hivyo tunavyofanya kazi".

Eddy alisimamisha gari mbele ya nyumba yangu. Tulitelemka ndani ya gari, nikafungua mlango tukaingia sebuleni wote na kuketi. Nilikwenda katika barafu na kutoa chupa ya whisky na chupa za soda kali. Nilitenga glasi, wote wanne tukaanza kunywa. Nilipoangalia saa ilikuwa saa tisa kasoro robo.

"Eddy nafikiri hatuna muda wa kupika hapa nyumbani, hivyo nenda Palm Beach Hoteli wakakufungie chakula cha watu wanne", nilimwambia Eddy.

"Sawa".

Eddy aliondoka kwenda kutafuta chakula.

"Willy, watu hawa wamepania sana", Sherriff alisema kwa sauti nzito.

"Mimi nilijua watapania, ndio sababu nikaweka tahadhari yote hii. Ngoja Eddy arudi atueleze ilikuwaje mpaka wakaweza kutufuata mpaka pale walipotushambulia. Ni bahati nzuri sana kwamba wote mna mafunzo ya kijeshi hivi mlitii amri za Eddy bila hata kufikiri. Jambo hili limenifurahisha sana maana kama mtu angesita, sasa hivi tungekuwa tunamuombolezea".

"Naona wote tumejenga silika ya hali ya juu kwa wakati wa namna hii", Sherriff alijibu.

"Tukimsubiri Eddy, sijui mmewaonaje hawa Maraisi wa vyama hivi vile vile", Veronika aliuliza.

"Mimi moja kwa moja nimempenda Chimalamo maana ni mtu aliye wazi. Nafikiri ni kiongozi mwenye busara. Kutokana na maelezo aliyotupa nafikiri anajua anafanya nini, na mtu kama huyu anaweza kabisa kuendesha harakati za ukombozi dhidi ya Makaburu maana anawajua nje na ndani. Ukikumbuka mazungumzo yetu siku ile huko Freetown juu ya Afrika Kusini sasa ukiongeza haya aliyotupasha ndugu Chimalamo hata wewe unazidi kupata mwanga mkubwa juu ya Afrika Kusini. Kwa ujumla nafikiri Chimalamo ni kiongozi mzuri na halisi. Juu ya Sikazwe nina dukuduku nae moyoni, maana sikumwelewa sawasawa sababu si mtu wazi. Hata nidhamu ya ofisi yake ilivyo kabla hujaonana naye, inaonyesha kasoro fulani. Nafikiri bila Willy kuwa mtu anayejua mbinu nyingi tusingemwona maana mbinu aliyotumia mimi mwenyewe mkufu. Halafu kuna kitu fulani ndani ya Ndugu Sikazwe ambacho sijui ni nini lakini kinanidundadunda sijui wenzangu mmemuonaje?", Sherriff alieleza.

"Nafikiri mawazo yako na ya kwangu hayako mbali. Nakubaliana na wewe kuwa Ndugu Chimalamo ni kiongozi mzuri. Na vile vile kuhusu Sikazwe hata mimi kuna kitu fulani ambacho sikukielewa ni nini kilicho ndani yake, lakini huenda nitakijua nikipata muda mrefu kufikiri. Lakini huenda ni mtu wa tabia ya namna hiyo, na kwa namna yake hiyo anaweza kuwa ni kiongozi mzuri zaidi kuliko hata Chimalamo. Huenda kila kitu kilicho ndani yake ni uongozi bora", nilieleza.

"Mimi sina la kuongeza, naona mawazo yetu yameoana", Veronika alijibu.

"Kusema kweli jamani sijastuka kama leo, kweli tumeponea chupu chupu, asante sana Willy kwa kuweka tahadhari".

"Bila asante Vero, maana ni kazi yangu kuhakikisha usalama wenu na wangu, hivyo uwe na amani kuwa nitafanya kila jitihada kuhakikisha usalama wetu, kama nikishindwa itakuwa nje tu ya uwezo wangu".

"Naomba sigara", Sherriff aliniambia.

"Hapa mimi nina aina ya sigara iitwayo Tropicana, sijui kama itakufaa".

"Wewe nipe tu, sigara zangu ziko hotelini. Baada ya kashikashi nahitaji sigara kama kufa".

"Nilitoa pakiti ya Tropicana nikaiweka mezani tukaanza kuivuta.

"Lo, mbona sigara safi kabisa, ni sawa sawa tu na 555, zinatengenezwa wapi?", Sherriff aliuliza.

"Hapa hapa nchini kwetu".

"Lo, mmeendelea sana, mnaziuza na nje?", aliuliza Veronika ambaye naye alichukua moja akavuta ingawaje hakuwa mvutaji sana.

"Sijui maana wameanza kuzitengeneza hivi karibuni, lakini naamini watafanya hivyo".

Mara Eddy akawa amerudi tukapata chakula ambacho tulikishambulia vizuri sana maana njaa zilituuma vibaya.

Baada ya kula chakula cha mchana tulikaa kitako kumsikiliza Eddy, akitusimulia jinsi mambo yalivyotokea pale SANP.

"Baada ya nyinyi kuondoka kwenye ofisi za PLF, nilingoja hadi nikaona gari Peugeot 504 namba TZ 311251 likijitokeza kwa upande mwingine na dereva wake akichungulia kwenye kioo cha kuendeshea baada nafikiri ya kuona hakuna gari zaidi lililokuwa nyuma yake; liliongoza kufuata njia mliyofuata. Mimi nililitilia mashaka nikalifuata nyuma baada ya magari kama mawili hivi kuwa kati yangu na gari hilo. Gari hilo pia lilikuwa limeacha magari matatu kati yake na gari lenu. Tulifuatana hivyo hivyo mpaka kwenye taa za usalama barabarani za Jangwani.

"Hapo ndipo nilihakikisha kuwa huenda gari hili lilikuwa na jambo. Mlipoingia barabara ya Umoja wa Mataifa gari hili lilisita kidogo mpaka gari zingine zikalipigia honi kwani taa zingebadili kabla hatujapita. Inaonekana kulikuwa na ubishi. Baada ya hapo gari hili lilingia barabara ya Umoja wa Mataifa nami nikalifuata. Niliona nyinyi mnasimamisha gari kwenye ofisi za SANP. Nilitelemka na kufungua boneti ya gari langu kwamba limeharibika, huku nikifikilia kuwa lile gari litarudi.

"Nilichukua spana na kuanza kujifanya ninalishughulikia gari langu. Gari lile halikurudi. Mimi niliendelea kujishughulisha hivi kiasi cha nusu saa, wakati nyinyi bado mko ndani ya ofisi. Mara nilistukia gari moja linaingia pale gereji, kwa bahati lilisimama karibu tu na mimi. Ndani ya lile gari mlikuwa na watu wanne. Dereva wa gari hili alitoka na kuingia ndani ya ofisi ya gereji hii. Alikuwa amevalia vizuri sana. Nilimwangalia kwani alikwenda akazungumza na mfanyakazi aliyekuwa amekaa mezani akiandika risti na simu iko upande wake. Alizungumza na mtu huyu wakabishana kidogo kisha nikaona anatoa kitu kama shilingi moja akampa

yule mfanyakazi. Halafu yule mfanyakazi akachukua funguo na kufungua kufuli la kwenye simu. Yule mtu akapewa simu akaanza kupiga. Mambo yote haya niliyaangalia kwa chati huku nikiendelea kujishughulisha na gari langu".

Eddy alitua akachukua sigara nikamwashia, akavuta kidogo kisha akaendelea.

"Sura za wale watu wengine ndani ya gari hazikuwa za kawaidana vile vile walikuwa na wasiwasi. Kila mara walikuwa wakigeuka kuangalia upande wa SANP. Yule mwingine alipomaliza kuzungumza na simu alikuja moja kwa moja akaingia ndani ya gari na kulizungusha. Mimi pale pale nikafunga boneti ya gari langu, maana tayari akili yangu ilikuwa imeshakuwa katika hali ya tahadhari nami nikageuza gari langu kuangalia barabarani. Hapo ndipo niliona mnatoka nje ya ofisi. Nikaona mmoja wa watu wale katika gari anainua "machine gun" kutoka chini na kabla hajaweka sawa nyinyi mlikuwa mmefika kwenye gari. Niliruka toka ndani langu na kuwapigia kelele. Nashukru kuwa mlinitii mara moja, kwani wakati ule ule mliporuka alimimina risasi pale pale mliposimama nikajua alikuwa mtu mwenye shabaha ya hali ya juu kwani gari lilikuwa likienda polepole.

"Mliporuka tu niliona mtu mwingine anatoa bomu la mkono na kuuma kifungo chake. Hapo ndipo nilipopiga kelele ya pili kisha nikarukia ndani ya gari wakati yule mtu anatupa hilo bomu na gari lao linaondoka kwa kasi. Ndipo na mimi nikaja na kusimamisha gari langu pale mlangoni baada ya ule mlipuko wa lile bomu. Pole sana bosi gari lako zuri sana limeteketea".

"Siku Eddy, nitapata jingine aina hiyo hiyo, nimetokea kupenda sana aina hiyo ya magari.

"Lo, inaonekana watu hawa wamejitayarisha vizuri sana", Veronika alisema kwa mshangao.

"Toka niliposikia jinsi walivyoiba zile silaha sikuwa na hamu nao tena. Nilijua ni watu wanaojua wanafanya nini. Ndio sababu niliwaasa hatari zitakazotokea toka mwanzo. Nafikiri sasa mnaamini mawazo yangu", hakuna aliyejibu; wote walinyamaza tu. Nafikiri walikuwa wakijutia kwa nini wamejiingiza katika janga hili.

"Vipi Eddy umepata habari zozote juu ya Kiki?", nilimwuliza.

"Kama nilivyokuahidi nimepata habari za kutosha".

Sisi wote tukawa tena tayari kumsikiliza huyu kijana na kusahau yote yaliyopita.

"Ehee hebu lete habari", nilimwambia.

"Nitaanzia toka ripoti nilizopata toka kwa makomredi wetu wa Soweto.

Makomredi wetu huko wanakataa katakata kuwa hakukuwa na mtu mwenye jina au wa sura kama nilivyowaeleza huko Soweto. Wanasema mtu aliyetoroka gerezani kati ya wale waliokamatwa na kutiwa ndani, yuko huko huko Soweto na wanaye sasa hivi. Hivyo ni uongo mkubwa kuwa huyu mtu alihusika na matatizo ya Soweto. Inasemekana kuwa mara ya kwanza mtu huyu kuonekana Tanzania ni wakati alipofika Mbeya akiwa na hiyo hadithi yake kuwa ametoroka gerezani huko Afrika Kusini baada ya kutiwa ndani kutokana na machafuko ya Soweto. Habari hii aliitoa kwa ofisi ya Chama huko Mbeya na ofisi hiyo ndiyo iliyomleta Dar es Salaam baada ya kusema kuwa yeye ni mwanachama wa SANP. Hivyo alipofikishwa hapa alipelekwa kwenye ofisi za SANP ambako inasemekana aliwaonyesha kadi yake, hivyo katika hali ya kumsaidia wakampeleka kwenye Kamati ya Ukombozi ya OAU.

"Je umepata habari zozote kuhusu maisha yake hapa mjini".

"Ndiyo, vijana wetu wamefanya kazi nzuri sana. Wameweza kupata habari kuwa Kiki alikuwa mtu asiye na rafiki. Ila alikuwa na rafiki mmoja wa kike Mtanzania anayeitwa Zabibu Abeid. Wanasema msichana huyu aliingia hapa mjini toka Tanga miezi minne iliyopita kwani alikuwa amepatiwa kazi na Meneja wa Kampuni iitwayo Twiga Safari ambayo inashughulikia mambo ya watalii. Msichana huyu amesoma mpaka kidato cha Nne alichomaliza mwaka jana. Anasemekana kuwa na uuzuri wa pekee. Katika ripoti yao wanasema kuwa kama hujamwona msichana huyo basi hujamwona binti Tanzania. Hivyo baada ya Kiki kufanya urafiki na msichana huyu mrembo, muda wake na maisha yake aliyatoa kwa msichana huyu.

"Zababu anakaa mtaa wa Jamhuri, kwenye orofa karibu ya mzunguko wa mtaa wa Zanaki na Jamhuri. Yuko mwenye nyumba ya orofa ya Msajili wa Majumba. Jengo Nambari K orofa ya tatu, nyumba nambari 7a. Nyumba hii amepewa na waajiri wake. Inasemekana kuwa fanicha yote ya mle ndani imenunuliwa na Kiki pamoja na gari moja zuri aina ya Ford Mustang"

"Na huku Kiki alikuwa tarishi tu... nilimkata kauli Eddy.

"Ofisini alikuwa tarishi, lakini nje alikuwa na fedha nyingi za kutosha. Hivyo kwa nje alikuwa ofisa wa mkubwa katika Kamati ya Ukombozi ya OAU".

"Na ndio sababu aliweza kumpata msichana mrembo kiasi hicho?", Sherriff aliuliza.

"Bila shaka maana sura ya Kiki ilikuwa ya kupendeza sana hivyo sioni ajabu kumpata msichana mrembo kiasi hicho".

"Kwa hivyo zaidi ya msichana huyu maisha ya Kiki hapa mjini hayaeleweki".

"Ndiyo, Kiki hakuwa na rafiki mwingine zaidi ya Zabaibu, lakini muda mwingi alikuwa kwa Zabibu. Tumejaribu sana kupata habari nyingine zozote juu yake lakini tunashindwa. Huenda Zabibu anaweza kujua".

"Okejamani nafikiri nyinyi mnaweza kurudi matotelini kwenu. Ila mjihadhari sana maana hali ya sasa ni ya hatari, nitakuja kuwaona baadaye msitoke mpaka nimekuja. Eddy atawapeleka mkapumzike. Mimi nitakwenda kumwona Zabibu sasa hivi, nafikiri atakuwa ametoka kazini", niliwaeleza.

"Nafikiri atakuwa amerudi maana anatoka kazini saa kumi kamili", Eddy alinieleza.

"Twende wote", Veronika alinieleza huku akiniangalia kwa macho ya wizi.

"Hapana wewe nenda ukapumzike, kazi uliyofanya mpaka sasa inatosha. Usiwe na wasiwasi nitajiangalia".

Veronika alikuwa haamini kwenda kuonana na msichana mrembo namna hiyo peke yangu. Hiyo ndiyo ya kazi na dawa.

Waliondoka wakaniacha mimi nikienda maliwatoni. Baada ya kukoga na kubadili nguo, niliangalia saa yangu nikaona ni saa kumi na moja na nusu. Nilichukua bastola yangu nikaiweka ndani ya jaketi nililovaa, nikajiona nilikuwa tayari kupita kiasi kuonana na Binti Tanzania. Nilitoka nje nikafungua mlango, nikaenda mpaka Palm Beach ambako nilichukua teksu kunipeleka kwa Binti Tanzania.

SURA YA KUMI

ILIKUWA yapata saa kumi na mbili wakati dereva wa teksi aliponishusha hatua chache kabla ya kufika kwenye mzunguko wa Mtaa wa Jamhuri na Zanaki.

"Hapo hapo pananitosha", nilimweleza huku nikimpa shilingi ishirini kisha nikatelemka. Niliangalia kwenye maegesho ya mtaa huu wa Jamhuri nikaiona gari ya Zabibu. Ilikuwa gari ya rangi ya kijani ambayo haikuiva sana, na ilikuwa ni aina ya Ford Mustang muundo wa kisasa. Kama umeshaiona Ford Mustang zilizoundwa vizuri basi hii ilikuwa mojawapo. Hata mimi niliipenda kwa umbo lake maana ilikuwa na milango miwili. Yaani 'Ford Mustang Sports Car', kama wanavyoiita wenyewe walioitengeneza.

Kule kuona gari hii kulinihakikishia kuwa Zabibu alikuwepo nyumbani, niliangalia jengo, nikaangaza huku na huku kuona kama kuna mtu ananifuata, nikaona hakuna. Kila mtu alionekana kuwa na hamsini zake. Basi mimi Willy nilijipenyeza kwenye lango linaloelekea kwenye ngazi za jengo hili. Nilipofikia ngazi nilianza kupanda taratibu kama mtu anayejua anapokwenda. Nilipanda mpaka orofa ya tatu, na nyumba iliyokuwa inatazamana na ngazi hizi ilikuwa namba 1a na nikajua 7a itakuwa mkono wa kulia hivyo nikafuatia taratibu.

Kwa sababu giza lilikuwa linaingia nyumba zingine zilikuwa zimewasha taa na zingine zikiwa giza kuonyesha wenye nyumba walikuwa bado hawajafika. Nyumba namba 5a na 6a zilikuwa giza ila 7a ilikuwa inawaka taa sebuleni. Nilitembea taratibu bila kupiga kelele mpaka kwenye mwisho wa namba 6a, niliposikia sauti ya msichana inapiga kelele ndani ya namba 7a. Harafu nikasikia sauti ya mwanaume.

"Mimi nisingependa kukuua Zabibu maana mimi nafurahia uumbaji wa Mungu mzuri aliokuumba lakini mimi nimeamriwa nikuue hivyo sina njia. Nisipokuua wewe, mimi nitauawa. Hivyo huna haja ya kupiga kelele, kufa hakika utakufa".

"Kwani mimi nimekosa nini masikini?", msichana aliuliza.

"Hata mimi sijui, haya kwa..."

Mimi nilikuwa nimejivuta na kuwa sawasawa na mlango wa hii nyumba, hivyo nilisikia mazungumzo haya. Niliona nikichelewa msichana huyu anaweza kuuawa. Basi nilitudi nyuma, bastola mkononi, niliurukia ule mlango na kuupiga teke

ukafunguka. Hapo hapo mimi nikatumbukia ndani nikitanguliza kichwa chini lakini nikafyatua bastola na kumpata yule kijana niliyemuona ameshika kisu chenye mpini mwekundu. Ile risasi ilikuwa haikumpata vizuri hivi alisimama wakati na mimi nimeshasimama yakaanza masumbwi. Alitupa konde moja likanikosa mimi nikampa shoto langu lililompata shingoni akaenda chini na hakusimama tena.

Mambo haya yalitokea kwa muda mfupi sana. Zabibu alikuwa amepigwa na butwaa kiasi cha kwamba yule mtu alipoanguka chini na yeye akaanguka juu ya kochi na kuzirai. Nilienda kumwangalia yule mtu pale chini, sikuwa na haja hata ya kumgusa ili nijue kama amekufa. Niliona kulikuwa na barafu pale sebuleni, nikaifungua nikatoa chupa ya maji baridi nikammiminia Zabibu naye akashituka.

"Kweli huyu Zabibu alikuwa ndiye Binti Tanzania. Mimi nimeona warembo katika nchi hii, lakini huyu alikuwa ni zaidi. Ukiwa unaamini kuwa kuna binadamu wengine hushushwa moja kwa moja toka mbinguni, basi Zabibu alikuwa mmoja wao, kwani mpaka sasa siamini kama msichana huyu alizaliwa na binadamu. Ingawaje haiwezekani kuamini kuwa mtu anaweza kutelemshwa toka mbinguni, lakini ukimwona Zabibu wewe mwenyewe utaona uwezekano. Maana hata mimi niliona inawezekana kwa huyu kiumbe wa binadamu alikuwa ameumbwa bila kasoro. Palipo ukweli lazima tuseme; mwenzetu alikuwa na uzuri sio kifani. Mcho yake manene ya mviringo yaliyozungukwa na nyusi zenye rutuba yalifunguka na kuniangalia mimi.

"Umetoka wapi?", aliuliza kwa sauti nyororo iliyotoboa rohoni mwangu kama miali ya moto.

"Nimekuja kukuokoa".

"Kama wewe si mmoja wao umejuaje kuwa amekuja kuniua?"

"Kama mimi ni mmoja wao kwa nini nimwue wakati anataka kukuua?"

"Ndicho kinachonishangaza".

"Basi mimi si mmoja wao, mimi ni rafiki yako. Kama una akili timamu tuondoke hapa chumbani kwako maana kinanuka mauti".

"Sijui kwa nini naona kama ninakuamini".

"Kwa sababu ndio jambo la busara".

"Haya nichukue, nitoe hapa, yule mtu kweli angeniua. Huenda lazima nikushukuru, asante sana?".

"Bila asante, msichana kama wewe una haki ya kuokolewa, huna haja ya kushukuru, hiyo ni haki yako".

"Na huyu mtu tutamwacha humu?".

"Nitafanya mipango aondolewe, simu iko wapi?".

"Chumbani".

Aliniongoza chumbani, nikapigaa simu ofisini nikamkuta Eddy nikamweleza kwa kifupi, kisha nikamwambia afanye mpango mtu huyu aondolewe hapa. Eddy akasema atatekeleza.

"Wewe ni polisi?", Zabibu aliuliza.

"Hapana".

'Sasa wewe ni nani?'.

"Mimi ni mtu ninayesaidia warembo kama wewe".

Nilimjengea tabasamu babu kubwa kisha nilimshika mkono tukazima taa, nakurudisha mlango, halafu tukaondoka. Nilipata tekisi pale chini, tukapanda na kumwelekeza dereva nyumbani kwangu.

"Tunakwenda wapi?", Zabibu aliuliza.

"Nyumbani kwangu, unaonaje?".

"Nakuona wewe ni mtu wa ajabu ajabu tu, usingekuwa umeniokoa nisingekuamini hata chembe!.

Nilikuwa nimeingia na mashaka makubwa kwenda moja kwa moja nyumbani kwangu. Nilikuwa sijui kwa nini, hivyo nikabadili mawazo na kumwelekeza tekisi dereva twende Ocean Road ambako ndiko Eddy alikuwa akikaa. Nilikuwa nina ufunguo mmoja wa nyumba yake kwa ajili ya nyakati kama hizi.

Tulikwenda moja kwa moja mpaka nyumbani kwa Eddy baada ya kumwelekeza dereva nyumba. Nilimlipa dereva tekisi pesa zake, halafu tukatelemka. Nilifungua mlango kisha nikawasha taa.

"Karibu ndani bibie".

Asante sana".

Nilikwenda kwenye barafu nikaifungua.

"Sijui utakunywa nini?"

"Baada ya vituko vilivyotokea nafikiri whisky na soda kali vitanifaa".

Nilichukua chupa ya whisky na soda kali halafu nikaendea glasi na kumimina kwenye glasi mbili ya Zabibu na ya kwangu halafu tukainua glasi zetu.

"Na tunywe kwa maisha yako marefu mrembo", nilisema.

"Na tunywe", alijibu kisha akanywa whisky ile haraka haraka.

Mimi nilikwenda kwenye simu nikapiga tena ofisini nikampata Eddy. Nilimpasha habari kuwa mimi na huyu mrembo Zabibu tulikuwa nyumbani kwake. Na yeye vile vile akanieleza juu ya kazi niliyokuwa nimemuagiza; vijana walikuwa wamempigia simu kuwa tayari walikuwa wameshaifanya. Nilimpongeza kwa jinsi kazi yake alivyokuwa anaifanya haraka kwa juhudi na maarifa.

"Nafikiri kwanza itabidi tufahamiane", nilimweleza Zabibu.

"Hasa ndilo litakuwa jambo la maana", alijibu.

"Mimi naitwa Willya Gamba, sijui wewe mwenzangu unaitwa nani?"

"Mimi naitwa Zabibu Abeid".

"Lo kweli aliyekuwa jina la Zabibu alijua kweli, kwani mimi naamini umtamu kama Zabibu".

"Ndio unataka kusemaje?"

"Nataka kusema wewe ni msichana mrembo ambaye sijawahi kumwona, na bila shaka aliyekuwa jina la Zabibu alijua utakuwa mtamu kama Zabibu".

"Usinivike kilemba cha ukoka. Kijana nadhifu mwenye sura nzuri na vituko vingi namna hii, haiwezekani kuwa haujamwona msichana mrembo kunizidi".

"Amini usiamini".

"Asante, lakini hata mimi leo nimemwona mvulana wa kipimo changu, sijui ulikuwa umejificha wapi mji huu hata nisikuone?"

"Mimi nilikuwepo nimejaa tele hapa mjini, lakini najua ingekuwa vigumu kuniona maana George Kiki alikuwa amekuganda kama kupe".

Pale pale sura yake iligeuka akainua macho yake marembo kunitazama machoni. Mimi nikamjengea tabasamu la sheria yake, Zabibu alionekana alikuwa amechanganyikiwa mawazo.

"Unajua nini juu ya George?"

"Hakuna haja ya kuzungushana sana, nafikiri inabidi sasa tuelezane ukweli. Na kabla hatujaendelea mbali ningependa kukuuliza lini umeonana na Kiki kwa mara ya mwisho".

Kwa kutokana na uzito wa sura yangu, Zabibu alilegeza sura yake kisha akajibu kwa sauti nyororo.

"Siku nne zilizopita, alisema atakwenda safari Botswana na atarudi baada ya wiki tatu".

"Na hauna habari nyingine yoyote kuhusu yeye?"

"Sina, kwani kumetokea nini?"

"Kwani yule mtu aliyetaka kukuuu alikuwa amekueleza nini?"

"Hata, alinielea tu kuwa alikuwa ametumwa kuja kuniua ingawaje yeye hakutaka lakini alikuwa amelazimishwa. Hakunielea kabisa sababu.

"Nakuomba uwe na roho ngumu, rafiki yako George Kiki ameuawa jana. Maiti yake ilikutwa chumbani mwake ikiwa imechomwa kisu chenye mpini mwekundu".

Nilitoa kisu nilichokuwa nimekiokota nyumbani kwa Zabibu kabla hatujaondoka.

"Na watu wale wale waliomwua ndio walikuwa wanakuja kukumalizia wewe".

Zabibu alibubujikwa machozi na kidogo azirai tena.

"Lazima ujitulize kwa sababu mimi niko hapa kupeleleza mauaji ya mpenzi wako".

"Mimi nilijua tu wewe ni Polisi. Sura yako na namna ulivyoingia chumbani kwangu sijapata kuona kwa macho ila ndani ya sinema tu. Zile sinema za kijasusi".

"Mimi si polisi bali ni mpelelezi. Huenda polisi nao wakaja kufanya upelelezi wao, lakini mimi bahati nimewahi na kukuokoa huenda wao wangepika wakati wewe umekwisha kuwa maiti".

"Una maana gani kusema wewe ni mpelelezi wala si polisi?"

"Mimi ni mpelelezi wa siri kama umewahi kusikia watu kama hao".

Macho ya Zabibu yakapanuka.

"Usije ukawa wewe ndiye mtu ambaye huwa tunasoma habari zake kwenye magazeti akipambana na majasusi mbali mbali wanaofanya maovu dhidi ya Afrika".

"Ndio mimi".

Zabibu aliruka pale alipokaa akaja katibu na mimi.

"Ooh! Mungu ni bahati gani kuonana na mtu kama wewe maana mimi nilikuwa nafikiri ni maneno ya uzushi tu ya magazeti maana walikuwa hata hawatoi jina. Kila mara ukisoma unaona tu vijana wa Afrika wakiongozwa na mpelelezi mashuhuri kutoka Tanzania wamefaulu katika kuwateketeza majasusi ya mabeberu yaliyokuwa yanatenda mambo maovu dhidi ya Afrika. Nitawaeleza rafiki zangu kuwa ni kweli huyu mtu yupo na mimi nimeonana naye".

"Halitakuwa jambo la busara, tafadhali fanya hii iwe siri kati yangu na wewe, nimekueleza tu kwa sababu unaweza kunisaidia katika upelelezi wangu juu ya tukio la kutisha lililotokea hapa mjini siku chache zilizopita".

"Ahaa nimeelewa tumesikia kwenye maredio ya nchi za nje, kuwa silaha kali za wapigania uhuru zimeibiwa kwenye bandari ya Dar es Salaam".

"Basi umebashiri sawa".

"Sasa George ana uhusiano gani na tukio hili?".

"Ndio sababu tumekuja kukuona, huenda ukajibu maswali yangu nitaweza kuambulia jambo lolote linalomwunganisha Kiki na tukio hili".

"Niko tayari kukusadia, kwanza kwa sababu umeniokoa, pili kwa sababu unapeleleza kifo cha mpenzi wangu na tatu nafikiri wewe ni kijana mwenye kupendeka".

"Asante, swali langu la kwanza nilitaka kujua kama ulikuwa unajua Kiki ni mtu wa Afrika Kusini?".

"Nilikuwa najua".

"Alikwambia alikuwa akifanya kazi gani?".

"Alisema yeye ni mwakilishi wa chama cha SANP katika Kamati ya Ukombozi ya OAU".

Nilishangazwa na jibu hili lakini sikuonyesha.

"Kwa hiyo mara nyingi alipokuwa anakuja kwako alikuwa akiandamana na wanachama wenzake wa SANP?".

"Hapana, George alikuwa mtu wa pekee, huenda ndio sababu nilimpenda. Alikuwa kila siku ananiambia kama ninataka kuepukana na matatizo nisizoeane na watu wengi. Na yeye kweli alikuwa hakuzoeana na watu. Ila alikuwa na marafiki wawili tu. Ndugu Ray Sikazwe, rais wa SANP na Patlako Shuta ambaye ni ofisa mkubwa katika SANP. Sikumwona na mtu mwingine. Oh, kidogo nisahau, vile vile walikuwa na rafikio yao mwingine Mzungu ambaye George alifahamishwa kwake na Sembuche na mwenzake Shuta. Na hata gari nililo nalo, George aliuziwa na Mzungu huyu. Kwa vile yeye alikuwa hapendelei gari kwani alikuwa anatumia gari la ofisini alinipa mimi".

Kwa mara ya kwanza niliona mwanga kwa mbali, na nikajua kwa nini msichana huyu alitakiwa auawe. Nilijivunia bahati yangu kuwahi kabla hajauawa.

"Unaweza kujua Mzungu huyu anafanya kazi gani?".

"Lo! hawa ndio wenye lile kampuni kubwa lililo na makampuni kadha wa kadha katika nchi nyingi za kifaraka yaani EUROAFRO Limited. Na huyu Mzungu ndiye mwakilishi wa kampuni hilo hapa akiangalia akiangalia makampuni yake madogomadogo yaliyoko hapa".

Kampuni hili EUROAFRO Limited lilikuwa kampuni kubwa la kibepari lililokuwa na hisa nyingi katika makampuni katika nchi nyingi za Afrika. Kirefu chake kilikuwa EUROPE - AFRIKA COMPANY. Uhusiano huu kati ya wanachama wa chahama cha wapigania uhuru na kampuni ya kibepari ulinishinda kuelewa.

"Kwa hiyo unasema huyu Sikazwe na Shuta walikuwa marafiki wa karibu sana wa Kiki

"Ndiyo, hao ndio alikuwa anatembea nao mara kwa mara na vile vile walikuwa wanajua kumwona au kumchukua pale kwangu mara kwa mara. Lakini zaidi ya watu hawa wawili na yule Mzungu, George hakuwa na rafiki mwingine".

"Huyu Mzungu unaweza kumkumbuka jina?".

"Ndiyo anaitwa Tony Harrison".

"Hawa marafiki wa Kiki uliweza kuzoeana nao?".

"Kusema kweli, Shuta na yule Mzungu walikuwa wananiheshimu kiasi cha kutosha lakini Sikazwe alikuwa wa ovyo sana. Amewahi kunitongoza mara nyingi na kunitaka nimwache George. Kwanza alikuwa anajivuna kuwa yeye ni Rais wa Chama na George alikuwa mtu mdogo tu, na kwamba msichana kama mimi sikufaa kutembea na George ila mtu kama yeye. Mimi nilimponda na kumwambia cheo na pesa havileti mapenzi, ila mtu anampenda mtu kwa vile alivyo, maana mtu na mtu ndio wanapendana".

Lakini nakwambia uso wa msichana huyu unapoonyesha sura ya haya ndipo uzuri wake unapozidi. Ingekuwa wewe usingevumilia lakini mie nilipiga moyo konde na kuendelea na kazi. Nilifikiria swali jingine nikaona nimepata maelezo ya kutosha ila nikaamua nimweke zabibu chini ya ulinzi wangu mpaka hapo baadaye.

Nilikuwa bado nafikiri hivi wakati tuliposikia gari linapiga breki mbele ya nyumba. Nilitoa bastola yangu tayari. Mlango ulipofunguliwa na Eddy akakingia.

"Bosi, twende haraka Veronika amenipigia simu anasema yuko katika matatizo. Nimekuja sababu nilijua huna gari", Eddy alisema huku akitweta.

"Oke Zabibu, subiri hapa tutarudi sasa hivi".

Nilifungua mlango kabla Zabibu hajasema neno lolote.

SURA YA KUMI NA MOJA

USIKU WA HEKAHEKA

Tulipofika Kilimanjaro Hoteli ilikuwa yapata saa tatu kamili. Tulipokuwa njiani kuelekea Kilimanjaro nilimweleza Eddy mambo yote niliyokuwa nimepata toka kwa Zabibu, mambo ambayo hata yeye alisema yalionyesha ufumbuzi wa jambo hili kwa mtu mwenye kufikiri. Tuliingia hotelini tukapanda lifti iliyotushusha orofa ya pili. Tulipotoka ndani ya lifti mara ile hali ya tahadhari ilituingia. Mimi nilitoa bastola yangu nikaiweka tayari na Eddy akafanya vile vile.

Tulipofika mlango wa chumba namba 206 tulikuta umefungwa, niligonga nikiwa nimesimama upande kabisa. Niligonga mlango mara mbili haraka haraka, halafu nikatulia kidogo kisha nikagonga tena, kwani hivi ndivyo Veronika alikuwa amenielekeza namna ya kujitambulisha lakini sikusikia kitu. Nilimonyesha ishara Eddy abane ukutani wakati mimi nafungua.

Nilifungua mlango ghafla. Tishio nililolikuta sijawahi kulipata tena, kwani Veronika alikuwa amelala kwenye sofa na kisu chenye mpini mwekundu kikiwa kimemwingia juu kidogo ya titi la kushoto. Kidogo ningezimia lakini nilijikaza nikakimbia pale kwenye sofa huku nikikanyaga maiti za watu wengine hapo chumbani.

Veronika alikuwa bado ameshikilia mkono wa simu mikononi mwake. Nilipomfikia nilimkuta bado yuko hai. Wakati huo Eddy nae alikuwa ameingia akanipa glasi ya whisky.

"Bosi jikaze, mnyweshe hii whisky mimi naita gari la hospitali"

Nilimnywesha Veronika kisha nikamtingisha akafunua macho akapata fahamu kidogo.

"Vero, Willy hapa, niambie nani amefanya hivi".

"Walikuja.... watatu... nikapam...bana ...nikawaua nikakupigia simu.... ku...ku...kumbe walikuwepo... wengine ...wawili ... mmoja ... akamwita ... Shu... Shu...Shuta muue.... mimi kugeuka ... akanichoma... ki... kisu... nikawahi ...kumpiga yule mwingine ...kwa... akafa... Shuta... akakimbia ...nika...

Hakuweza kusema tena. Nikamwongeza whisky na kumtingisha.

"Oh Vero, nimeita gari la wagonjwa na mganga anakuja sasa hivi utapona tu.

"Si...siwezi...nitakufa...nimekufa...ame...moyo...Willy na...nakufa...na...ku...penda ...hakuna tena... mwanamume... niliye... mpenda...kama wewe.

Ni...nimefurahi...kukuona ...ma...mara... ya...mwisho...nikifa ...kwa ajili ya Afrika... siogopi...kufa...kwani nimekufa ...kwa sa...sabab...bu...nzuri. Ende...le..za ...ma...pa...mba...no... Willy ...Mungu...a...ku...sai...die...uni...ku...pi...zie...kisasi Afrika. Ni...busu...na... ku...

SURA YA KUMI NA MBILI

NILIJUA Veronika hawezi kuchukua dakika moja zaidi, niliweka midomo yangu kwenye midomo yake na kulamba damu yake ambayo sasa ilikuwa inatoka mdomoni. Alitabasamu na macho yake yakang'ara kiasi ambacho sikuwahi kuyaona yanang'ara vile halafu akayapepesa akafariki. Alikufa huku akitabasamu.

Sikuwahi kulia na kupata uchungu kama wakati wa kifo cha Veronika. Nilijilaumu. Kama ningekwenda nae kwa Zabibu asingekufa.

Eddy alinikuta nabubujika machozi kama mama anayemlilia mtoto wake wa pekee.

"Bosi jikaze", Eddy alinishauri.

"Washenzi hawa, nduli hawa, watanitambua. Kwanini Mungu anaruhusu mtu kama Veronika kufa mikononi mwangu?. Eee Mungu nisaidie nilipize kisasi kwa ajili ya mwanamapinduzi huyu wa Afrika nzima", niliomba kwa sauti huku machozi yananitoka. Vero alikuwa amekufa kishujaa. Alikuwa amewaua maadui wanne pale pale chumbani.

Niling'oa kile kisu nikasafisha damu yake kwenye nguo zake.

"Kisu hiki hiki kitawauwa kama walivyomwua Veronika", nilisema.

"Bosi ninataka toka sasa tuwe pamoja".

"Hapana sasa hivi, fanya mpango wa kuondoa maiti hizi humu ndani. Na umwarifu Chifu, polisi wala wakuu wa hoteli wasiingilie. Na halafu kampashe Sherriff habari hizi za huzuni. Muushughulikie mwili wa Veronika uweze kupelekwa kwao. Mwambie Sherriff ashughulike na habari hiyo tu mambo mengine aniachie. Mwambie Chifu mambo yote yalivyo mpaka sasa mimi namfuata Shuta lazima aliye. Fanya hayo kwanza halafu nitakapokuhitaji nitakujulisha".

Niliondoka na kumwacha Eddy mle ndani ya chumba nikakimbia kwenye lifti iliyonitelemsha chini. Nilipita pale mapokezi huku nikikimbia kiasi cha watu wote kunishangaa.

Niliingia ndani ya gari Eddy alilokuwa amekodi na kuliacha Kilimanjaro Hoteli nikaondoka kwenda kumtafuta Shuta.

Niliondoka na kuelekea nyumbani kwa Eddy nilikomwacha Zabibu. Njiani nilifikiria uhusiano wangu na Veronika tokea siku tuliyoona mwenye ndege mpaka kifo chake kilipotokea mikononi mwangu dakika chache zilizopita. Nilisikia uchungu usio kifani. Hasira na chuki yangu kwa makaburu, mabeberu na vibaraka wao ilizidi kiwango chake cha kila siku.

"Kifo peke yake ndicho kitaniachisha kuwawinda hawa wadhalimu maishani mwangu", niliapa.

Nilipofika nyumbani kwa Eddy nilimkuta Zabibu amekaa kwenye sofa pale tulipomwacha.

"Kumetokea nini, mbona ulikuwa unalia?", Zabibu aliniuliza baada ya kuniangalia kwa muda mfupi.

Nilimweleza yaliyompata Veronika, na jinsi urafiki wetu na Veronika ulivyokuwa umekomaa tangu kuonana mwenye ndege wakati tukielekea Freetown. Hakika nilijuta kumfahamu Veronika afadhali nisingeonana nae.

"Usisikitike sana, sasa tunakuwa watu wawili tuliopoteza marafiki zetu. Lililopo sasa ni sisi kutiana moyo na kusaidiana kuwatafuta hawa waliofanya matendo haya.

Nilijisikia vizuri kidogo Zabibu kuwa pamoja nami.

"Unajua Shuta anapokaa?", niliuliza.

"Ndio, ankaa Oysterbay, Kaunda Drive No. 11230".

"Basi, sasa wewe tulia hapa mimi nitarudi muda si mrefu".

"Twende sote".

"Hapana. Kazi hii huijui niachie mimi, wewe pumzika hapa. Ukiona usingizi chumba hicho hapo kalale. Tutaonana baadaye".

"Lakini jihadhari inaonekana watu hawa ni hatari kabisa, sitapenda kusikia umeuawa, nikisikia tu na mimi nitajiua", aliniambia Zabibu akionyesha hali ya mapenzi kama kwamba tumekuwa marafiki siku nyingi.

Mimi huwa sielewi kwa nini binadamu hawa hutokea kunipenda mara tu nionyeshapo uso wangu. Niliondoka na kuelekea Oysterbay. Niliingia Kaunda Drive na kuanza kuangalia namba za nyumba. Niliendesha polepole mpaka nikaona nyumba. Nilipokuwa napita mbele ya lango la nyumba hiyo mlango wa

mbele ulifunguliwa mimi nikaendelea mbele kidogo nikaegesha gari langu, halafu nikarudi kwa miguu.

Nilipofika kwenye ua wa jengo hili nikabana, maana watu wanne walikuwa wanazungumza hapo nje na kulikuwa na magari mawili.

Niliposogea nilisikia mtu mmoja anazungumza.

"Hay Shuta, zungumza na mzee halafu utatukuta Sliver Sands marquuis Du Zaire wanapiga huko mpaka saa kumi. Baada ya kazi ngumi namna hii mtu inambidi astarehe kidogo".

"Sawa Mlambo, ngoja nizungumze na mzee nimpe taarifa yote ilivyo halafu nitampitia msichana wangu na mnamo saa tano hivi nitakuwa huko", alijibu Shuta.

"Oke tutaonana", alijibu Mlambo.

Kisha Mlambo na wenzake wakaingia ndani ya gari aina ya Peugeot 504 na walipotokeza kwenye mlango nikaona namba zao TZ 66500. Shuta alirudi na kuingia nyumbani. Mimi niliruka kama paka nikatua ndani ya ua. Baada ya kutua nikasikia viatu vinatembea kwa nje. nikarudi haraka haraka nikabana ndani ya ua wa michongoma. Nilipoangalia nikaona alikuwa ni askari wa usiku aliyekuwa analinda ile nyumba. Bila kuniona alizunguka kunipita kwenye upande huu wa kulia wa nyumba. Nyumba yenyewe iliwa kushoto mwa barabara kama unatoka mjini.

Alipotangulia tu mimi nilimnyemelea bila yeye kunisikia. Nilipokuwa karibu nae nilimrukia na kumtia kabali, taratibu na bila kupiga kelele nilimnyonga na kuhakikisha amekufa kisha nilimsogeza pembeni kwenye giza la michongoma. Kisha nilizunguka nyumba kuangalia hali ilivyo. Nyumba yenyewe ilikuwa na vyumba vitatu vya kulala. Kulikuwa na chumba kimoja kikubwa nikajua hiki ndicho mwenye nyumba alikuwa akilala. Madirisha yalikuwa yamefungwa. Nikatoa pete yangu yenye jiwe la almasi, nikakata tundu katika kioo kisha nikaingia mkono karibu na mahali pa kufungulia dirisha. Baada ya kufungua dirisha la kioo, kulikuwa na dirisha jingine la wavu wa kuzuia mbu. Nilichukua mkasi nikakata sehemu kiasi cha kupitisha mkono karibu na mahali pa kufungulia nikalifungua.

Nilipanda na kutumbukia ndani ya chumba cha kulala kilichokuwa na bafu ndani yake. Nilifunga madirisha vizuri nikaacha mapazia kama yalivyokuwa

yamekunjwa. Nilinyata mpaka kwenye mlango nikasikia mtu anasema kwenye simu.

"Halo naomba mzee. nimepiga karibu dakika tano nzima sipati namba hiyo. Mimi Shuta hapa.

Nilisubiri pale kwenye mlango wa kutokea sebuleni.

"Halo, Shuta hapa".

Mambo hayakwenda vizuri sana yule msichana ni mpiganaji wa karate na judo sijawahi kuona. Ameua vijana wetu wanne, watatu aliwaua kabla ya kuchomwa kisu, lakini hata wakati amekwisha kuchomwa kisu alimwua Shilonda kwa kumvunja shingo. Lakini hata hivyo nimemwua.

"Nina uhakika kabisa amekufa palepale maana nilimchoma kisu kwenye moyo hasa".

"Ndio sasa tumebakiza wawili ndipo tunaweza kuanza kupakia".

"Haya asante mzee".

Kisha nilisikia anapiga simu tena. "Halo Sakina yupo. Shuta hapa".

"Aha kisura jitayarishe nakuja kukupitia twende kamanyola nasikia siku hizi wana mtindo mpya wa 79 Scania LBT III... tutakwenda ukauone".

"Dakika kumi na tano nitakuwa hapo".

"Haya kwaheri".

Akarudisha simu.

Nilijua atakuja chumbani hivyo mimi nilijibanza kwenye ukuta karibu na mlango nikamsubiri maana nilisikia viatu vinakuja. Mkono wa kushoto nilishika bastola na mkono wa kulia kisu kile kilichomwua Veronika.

Alifungua mlango akawasha taa huku akipiga mluzi kisha alifululiza kwenda kwenye kabati la nguo bila hata kuniona. Mimi nilirudisha mlango kwa mguu, ndipo akageuka kuniona. Sijaona mtu anastuka namna hii maana palepale jasho lilimtoka, akataka kukaa chini akashindwa, akaanza kugwaya. Nilifikiri atazirai.

"Kumbe wewe unaona kuuwa wenzako ni rahisi na kumbe wewe mwenyewe unaogopa kifo namna hii".

"Niche niache, mimi ninakujua wewe ni nani, nisamehe".

Kuomba kwake msamaha kulinifanya mimi nikasirike zaidi.

"Kabla sijafikiria kukusamehe nataka kujua kiongozi wenu ni nani?".

"Mimi simjui; mimi ni mtu mdogo tu".

"Si unasema mimi unanijua?".

"Ndiyo nakujua wewe ni Willy Gamba, mpelelezi mkuu wa Afrika. Mimi niliwaambia waaache kama wewe wamekuuingiza katika upelelezi lakini walikataa".

"Wakina nani?".

"Akina Mlambo".

"Mlambo ndiye nani?".

"Ndiye mkuu wetu sisi kwa upande wa kuua wapinzani".

"Na yeye ni mwanachama wa SANP?".

Alitoa macho na kushitushwa sana na swali langu hili, kisha nikaona anaanza kutokuwa na mshituko.

"Sitasema maneno zaidi nifanye unavyotaka".

"Ahaa, mimi huwa napenda watu shujaa kama wewe".

Niliweka bastola yangu ndani ya mkoba wake nikaweka kisu vizuri kwenye mkanda nikamfuata. Aliponiona sina silaha akaona ajaribu bahati yake. Palepale aligeuka mbogo na kuanza kunishambulia kwa makonde. Alitupa konde la kwanza nikaliona. Akatupa la pili nikaliona. Akatupa la tatu nikashika mkono wake nikamchukua judo na kumtupa upande mwingine wa chumba akaanguka kama papai bovu. Haraka haraka nikamfuata pale chini nikampiga teke la mbavuni na lingine la tumboni akalainika. Kisha nikamkunja vizuri sana. Nikatoa kisu nikachana shati lake akabaki tumbo wazi.

"Sasa utanieleza. Usiponieleza nitakutumbua matumbo na Sakina hutamwona tena. Niambie nani mkubwa wenu?".

Macho ya kutisha yalimtoka kwa kukiangalia kisu na kuona kuwa nilikuwa sitanii.

"Niache, niache nitakwambia mkubwa wetu ni...

Kabla hajamaliza kusema mlango ulipigwa teke na mtu mmoja akaingia ndani na kabla hajafyatua risasi pale tulipokuwa nilijirusha upande mwingine risasi zake zikanikosa ila zikamwingia Shuta tumboni, na mimi wakati ule ule nikamtupia kisu kilichompata katikati ya koo akaanguka chini huku risasi zinatoka ovyo.

Nilisikia vurumai nyingine sebuleni nikajua wako wengi. Kama umeme nilitoa bastola yangu tayari kukabiliana na matatizo.

"Mashuka umempata?", nilisikia sauti inauliza kwa woga.

"Ndiyo", nilijibu kwa sauti ya chini.

Kabla sijampa nafasi nilijirusha na kujiviringisha ndani ya sebule ambamo nilikuta watu wawili mmoja akiwa na bastola. Na kwa vile hakutegemea hatua kama ile alishikwa na bumbuwazi palepale nikapata nafasi ya kumpiga risasi ya katikati ya paji la uso akaanguka chini. Kabla sijawahi kusimama yule mwingine alipiga teke bastola yangu ikaanguka chini, palepale akanipa teke la tumboni nikaanguka chini. Wakati ule ule nikaona anaangalia kule bastola ya yule mwenzake niliyempiga risasi ilikoangukia na akaruka kuichukua. Mimi nikitumia ujuzi wangu wa miaka mingi nilimwahi wakati ndipo anafikisha vidole vyake kwenye bastola nikampiga kichwa kimoja cha sisimizi akaona nyota na kujiviringisha mbali na bastola. Kwa vile alikuwa tayari amenitia mori nilimfuata wakati naye anasimama. Nikaona anajikunja tayari kupigana karate, mimi nikaona ndipo ananipeleka nyumbani.

"Aisee mlambo-iiiiji mjukuu wa Chaka mwana Zulu fanya kazi yako", alijitia mori.

"Ungekuwa mjukuu wa Chaka ufanye jambo la aibu kama kuwa kibaraka wa Makaburu - tazama Mwafrika asiye na aibu".

Aliruka na kutupa karate nikaikinga kwa mikono. Akatupa tena nami nikaizuia, halafu akageuza mara moja, akanipata, kisha akanipata tena, nikajua huyu alikuwa na ujuzi wa kutosha hivyo mimi ilinibidi nibadili na kujaribu Kung-fu. Na hapo hapo nikasikia mwili mzima unasisimka nikamwingia. Kwa sababu ya hasira na baada ya kukumbuka mauaji ya Veronika chuki kubwa iliniingia hivyo nilitupa wimbi la kwanza nikatupa la pili likampata

la tatu nilipopeleka kiganja changu kikamtoboa chini kidogo ya kifua na kutoka na vipande vya matumbo na vitu vingine vya ndani. Alipiga kelele

"Eeeeeeeeeeeeeenakufa, eeeeeeee.

Akaanguka chini akafa.

Nilirudi chumbani nikamkuta Shuta yu hai, anajaribu kusimama lakini anashindwa sababu ya risasi zilizomwingia tumboni. Nilichomoa kisu kutoka kwenye maiti ya yule mtu niliyekuwa nimemchoma kooni nikamfuata.

"Kama ulivyomwua Veronika na mimi nakuua hivyo hivyo, maana nilimwahidi aliponiomba nimlipizie kisasi"

"Nisamehe, nipeleke hospitali".

Kusikia hivi roho ilinichemka, nikamchoma kisu katikati ya moyo huku analia hovy.

"Kwa heri Shuta, mtaonana sasa hivi na Veronika mbele ya Mungu, ukajibu vizuri kwanini umemwua".

Niligeuka na kumwacha anakufa.

Nilipofika sebuleni tu nikasikia gari linapiga breki pale nje. Niliruka nikachukua bastola yangu na kuokota nyingine hapo sebuleni nikabana karibu na mlango wa kutokea nje nikasubiri.

Mlango ulipigwa teke na hapo hapo wakaingia watu wawili kama risasi, bastola mkononi, wakajiviringisha mmoja akiwa tayari kupambana na kitu chochote mbele yake na mwingine akajiviringisha na kugeka nyuma. Mimi nilikuwa tayari kwa lolote.

"Ni mimi usiftatue", nilipiga kelele.

Kumbe hawa walikuwa ni Eddy na Sherriff.

Oh Bosi, samahani", Eddy alisema huku akiruka.

"Siku nyingine kutatokea ajali namna hii", nilimwambia.

"Tunaomba isitokee", Sherriff alijibu naye akisimama.

"Umefanya kazi kubwa sana Bosi", Eddy alinipongeza baada ya wao kuangalia maiti zote ndani ya nyumba hii.

"Ninastahili kazi kama hii", nilijibu.

"Sisi tulipongojea kwa muda mrefu tukaona tukufuate baada ya kujua kutoka kwa Zabibu kuwa umekuja huku. Tulihisi kuwa kuchelewa kwako unaweza ukawa katika matatizo. Tulipokuja tulikuta gari lako na gari jingine hapo mbele

yameegeshwa. gari lako lilikuwa limetolewa upepo ndani ya tairi zote, hivyo hii ilituhakikishia kuwa uko msambweni", alieleza Eddy huku tukielekea kwenye gari lao. Ndani ya gari nilimkuta Zabibu.

"Oh Willy mpenzi uko salama?".

Alifungua mlango na kunirukia akiweka mikono shingoni mwangu na kunibusu.

"Na wewe umefuata nini?", nilimwuliza.

Nilimkarisha ndani ya gari kwenye viti vya nyuma mimi nikakaa huku Sherriff na Eddy wakaingia mbele, Eddy akatia gari gea tukaondoka.

"Nilikuja nikuone kama ni kufa tufe wote. Maana sijui nini kimeniingia nakuona wewe ndiye mwenzangu sasa. Nikiwa karibu na wewe nasahau yote yaliyopita".

"Usizoe kutembea na sisi mtoto kama wewe, hufai hata kujeruhiwa kidogo. tuachie sisi hatari ndiyo kazi yetu. Sitaki kupatwa mkasa kama niliopatwa nao kwa Veronika".

Kisha nikamweleza toka mwanzo mpaka mwisho wa mapambano yangu nyumbani kwa Shuta.

"Naona huyu Mlambo na wenzake walitia shaka walipoona gari langu. Hivyo walirudi kuhakikisha. Lazima niseme Mlambo alikuwa na mafunzo ya hali ya juu ya jeshi hata mimi alinitoa jasho".

Tulielekea nyumbani kwa Eddy.

Tulipofika nyumbani kwa Eddy ilikuwa saa tano za usiku. Tuliingia tukaa kwenye viti. Eddy akaleta vinywaji.

"Kifo cha Veronika kimeniuma sana, tokea sasa mimi nimeahidi nitakuwa bega kwa bega na wewe mpaka nione mwisho wa mambo haya", Sherriff aliniambia huku machozi yakimtoka.

"Sijui nikwambie nini Sherriff, maana hali niliyonayo mimi siwezi kuieleza. Afadhali tuiachie hapo hapo".

"Basi, mambo yote tumetengeneza. Chifu amesema mwili wa Veronika hauwezi kusafirishwa mpaka mwisho wa mambo yote ili aweze kupewa heshima zote za kijeshi. Hivyo mwili wake umetunzwa huko kwenye chumba cha maiti katika hospitali ya Muhimbili mpaka hapo tutakapojua mwisho wa mambo haya. Mwili

wake utapewa uangalizi wa pekee hivyo hata tukichukua mwezi mzima utakuwa katika hali safi tu", Eddy alieleza.

"Jambo hili haliwezi kuchukua siku mbili zaidi. Nimeshapata mwanga mkubwa wa kutosha. Kuna kitu kidogo tu ambacho bado kinakosekana lakini naamini kesho haiishi bila kukupata kitu hicho", niliwaeleza. Kisha nikawaeleza jinsi nilivyokuwa ninafikiria mambo yalivyo toka mwanzo mpaka mwisho.

"Sasa ninachotafuta ni yale magari waliyapata wapi?.Nguo ni rahisi pamoja na vyeo kama nilivyowaeleza. nikishajua hilo basi jambo hili tutakuwa tumelitatua. Itabaki sasa kufanya shughuli ya mwisho ambayo ni kuzikamata hizi silaha na kuwakamata vibaraka hawa".

Wote walitingisha vichwa kuonyesha wamenielewa.

"Ray Sikazwe anakaa wapi?", nilimwuliza Zabibu.

"Anakaa Oysterbay, Kenyatta Drive nyumba Nambari 1000/D.

"Oke, Eddy tokea sasa hivi weka vijana wa kumfuata Ray Sikazwe kila mahali anapokwenda. Ifikapo asubuhi nataka nataka nijue nyendo zake zote na sisi tutawasaidia tokea hapo. Tukiweza kufanya hivyo kazi itakuwa rahisi. Baada ya mambo yote yaliyotokea leo lazima akipata habari atakuwa na wasiwasi, hivyo lazima tu atafanya kitu cha kujinasa. Wote tutalala hapa maana ndiko mahali hapafahamiki.

"Tutaonana asubuhi", niliwaaga.

Nyumba ya Eddy ilikuwa na vyumba vitatu vya kulala. Kwa vile Zabibu alikuwa na huzuni nyingi na kwa vile mimi pia nilikuwa na huzuni tulionelea afadhali tukalala pamoja ili tuweze kuliwazana mioyo.

SURA YA KUMI NA TATU

MAPAMBANO NA VIBARAKA

Ilikuwa saa kumi na mbili na nusu za asubuhi wakati nilipokuwa nakaribia kumaliza kunyoa ndevu. Nilikiangakia kidevu changu kwenye kioo nikaona nilikuwa sijajinyoa vizuri. Kila wakati nilipokuwa na mawazo mengi kitu kama hiki kilikuwa kinanitokea . Lakini hata hivyo nia yangu nionekane nadhifu hivyo nilichukua tena mashine ya ndevu na kuanza kujinyoa. Nilipoona mambo yanakuwa mazuri kwenye kidevu changu, nikaanza kuoga.

Nilitoka maliwatoni na kurudi chumbani nilikokuwa nimelala. Zabibu bado alikuwa hajaamka, hivyo nilivaa taratibu ili nisije nikamshtua toka usingizini. Alikuwa na sura ya mtoto mchanga isiyokuwa na maneno. Nilimwangalia huku nikivaa. Nilipomaliza kuvaa na kuweka kila kitu changu tayari, nilikwenda nikambusu Zabibu usingizini nikaondoka ndani ya chumba na kufunga mlango taratibu.

Niliwakuta Sherrieff na Eddy wamekaa sebuleni wanakunywa kahawa.

"Karibu bos, habari za kuamka?".

"Nzuri", nilijibu, nikaa kwenye kiti cha meza ya kulia nikavuta kikombe cha chai na kujiwekea kahawa ya kutosha.

"Lazima iwe nzuri", Sherrieff alijibu huku akitabasamu nikajua alikuwa na maana gani kusema hivyo.

"Usinionee wivu".

"Lazima tukuonee wivu, maana chuma kama hicho si cha kawaida.

"Bosi, vijana wameleta habari kama ulivyoomba", Eddy alisema huku akibadilisha mazungumzo.

"Ndio, wamesemaje.

"Wamesema hawakuweza kumwona Sikazwe mpaka saa tisa za usiku. Walimpata akitokea kwenye barabara ya Bagamaoyo na akielekea nyumbani kwake. Hawakuweza kujua alikuwa anatokea wapi. Na mpaka sasa hivi bado yuko

nyumbani amelala. Wamenieleza kuwa ofisi za SANP hazifanyi kazi siku za Jumamosi. Na kama unavyojua leo ni Jumamosi".

"Basi waambie waendelea na wahakikishe kuwa hawapotezi hata dakika moja. Atakapoondoka nyumbani nataka kujua anaelekea wapi. Sawa?".

"Hamna taabu".

"Sasa hivi mimi ninakwenda kumwona Chifu maana nilipata habari kuwa anataka ripoti toka kwangu, maana anasumbuliwa sana na Serikali".

"Nafikiri Sherriff anaweza kuendelea kupumzika hapa, mimi nitakujulisha wakati nitakapokuhitaji".

"Sawa", alijibu Sherriff kwa mkato.

"Naomba unipatie 'machine gun' inayoweza kuchukua risasi zaidi ya mia. Niliwahi kuzitumia nilipokuwa jeshini.

"Aina gani".

"Zilizotengenezwa Urusi".

"Zipo".

"Oke niletee moja ya aina hiyo. Ikiwezekana tuma mtu aniletee mapema kusudi niishughulikie".

"Hamna taabu, utapata.

Baada ya kuzungumza na hawa vijana tuliagana kisha nikaondoka. Nilitembea kwa mguu mpaka nyumbani kwangu, ili nikabadilishe nguo. Nilifika nikafungua mlango, nikaangalia saa yangu nikaona ilikuwa yapata saa mbili kasoro robo. Nilipoingia tu ndani, roho yangu ikashtuka lakini nilikuwa nimechelewa, nilipigwa na mfuko wa mchanga kisogoni nikaanguka.

Nilisikia sauti ikisema ni saa tisa sasa. Sauti hiyo ndiyo ilikuwa imenizindua. Nilijikuta nimelazwa kwenye kitanda cha chuma bila godoro, na nilijikuta nimefungwa kwenye kitanda mikono na miguu. Kichwa kilikuwa kinaniuma sana, na kwa chati nilifunua nilikuta nimo kwenye chumba kidogo cha giza tupu.

Nikatuliza mawazo nikaanza kufikiri nini kimetokea. Ndipo nikatambua kuwa nilipokuwa nakwenda nyumbani kwangu saa mbili kasorobo nilipigwa na kitu nilichohisi ni mfuko wa mchanga nikaanguka chini. Tokea hapo mpaka sasa

sikujua chochote. Hii ina maana kuwa nilizimia. Nikakumbuka yule mtu alisema ilikuwa saa tisa, hii ina maana nilikuwa nimezimia kwa zaidi ya masaa sita.

Nilifikiri jinsi akina Eddy, Sherriff, zabibu na Chifu walivyokuwa wamehangaika huu kujaribu kunitafuta. Hata mimi mwenyewe nilikuwa sijui hapa ni wapi. Ila nilikuwa nasikia kelele nyingi nje ya chumba hiki. Hivyo nilifikiri kuwa huenda ikawa ni sehemu ya viwanda. Sikujua ile sauti iliyosema sasa ni saa tisa ilitokea wapi, maana kulionekana kana kwamba hakukuwa na mtu ndani ya chumba hiki.

"Zaidi ya saa tisa sasa lazima waje kutupokea sisi twende tukapate chochote", nilisikia tena mtu anazungumza.

"Washa taa", sauti nyingine ikajibu.

Hivyo nikajua kuwa nilikuwa nalindwa na watu wawili ila sikuweza kuwaona kwa sababu ya giza. Taa ilipowashwa mimi nikajifanya kana kwamba bado nimezimia kabisa.

"Bado kazimia kabisa", alisema mmoja wao.

"Daktari alisema hawezi kuamka mpaka saa kumi na mbili au baada ya hapo", alijibu mwingine.

"Kama ni hivyo basi twende tukawaambie watupokee njaa inauma sana".

"Oke twende, zima taa".

Walifungua mlango na kuzima taa halafu wakafunga mlango na funguo wakaondoka. Mimi nilijinyanyua ili nione nimefungwa kiasi gani. Nilikuta ni mikono na miguu tu iliyofungwa kwenye kitanda cha chuma kipatacho futi tatu upana. Miguu ilifungwa kwa ustadi sana kiasi kuwa nilisikia kama damu haipiti na sehemu za nyayo zimekufa ganzi. Kwa upande wa mikono, mkono wa upande wa ukutani nilipoujaribu nikaona haukufungwa kwa ustadi sana, ule wa upande mwingine ndio ulifungwa kwa ustadi sana.

Nilinyanyua kichwa changu nikasikia kinauma sana, nikakirudisha chini. nilianza kufikiri namna gani nitajiokoa. Baada ya kufikiri sana nikaona njia pekee ni kujaribu kufungua hizi kamba kabla walinzi hawa hawajarudi. Hivyo nilionelea nijikaze. Ingawaje kichwani nilisikia maumivu makali. Kwa vile sehemu zote tokea tumbo, kifua na kichwa zilikuwa hazikufungwa, na kitanda kilikuwa cha futi tatu nilijikunja ili mdomo wangu ufikie kamba za mkono wa upande wa ukutani ambao haukuwa umefungwa sana.

Nilitulia tena nikamwomba Mungu. Niliupeleka mdomo wangu kwenye fundo la kamba walilokuwa wamenifungia. Kwa bahati mdomo wangu ulifika nikaanza kupitisha meno yangu kwenye kamba ili niweze kujua wamefungaje. Katika hii tafuta tafuta huku maumivu karibu yananitoa fahamu, niliuma ncha moja ya kamba, nikaivuta na fundo lote la kamba likafunguka na mkono wangu wa kulia ukawa huru.

Ilibidi nirudishe kichwa changu kipumzike maana maumivu yangu yangeweza kunifanya nizimie.

Nikiwa na mkono mmoja huru, nilipata tumaini na nguvu mpya. Nilichoomba sasa ni watu hawa wasije upesi. Kwa vile walikuwa wamesema daktari aliwaambia siwezi kuamka kabla ya saa kumi na mbili nilijua watadharau kuja ndani ya chumba hiki cha joto la kuweza kuua kabla haijakaribia saa kumi na mbili wakati wananitegemea kuamka. Nguvu mpya zilizoletwa na mawazo kuwa nimechelewa mambo mengi zilinifanya nisahau kabisa maumivu yangu.

Niliutumia mkono wangu wa kulia kufungua mkono wa kushoto. Nikiwa sasa nimeweza kufikia hatua hii niliingiwa na furaha nikaanza kushambulia kamba nilizofungwa miguuni. Kwa mtu mwenye ujuzi kama wangu hii haikunipa taabu na mara nikawa huru tayari kupambana na wadhalimu hawa.

Nilirudi nikajilaza nikaziweka kamba kijanja kana kwamba bado hazijafunguliwa. Nikawa katika hali ya kusubiri. Nilivyokuwa na bahati haikupita muda mrefu nikasikia funguo zinaingia ndani ya kufuri la mlango. Mara mlango ukafunguliwa na taa zikawashwa. Mimi nilijilaza vile vile na kujifanya bado nimezirai.

"Bado sana huyu, niliwaambia daktari alisema saa kumi na mbili. Angekuwa mtu wa hivi hivi asiye na mazoezi pigo lile lingemuua pale pale", nilisikia sauti ikisema.

"Sawa. Akiamka saa kumi na mbili itakuwa vizuri maana ndipo wakati wazee watakapomhitaji", sauti nyingine ilijibu.

"Haya shika funguo, mwangalie kwa makini akionyesha dalili ya kupata fahamu tupashe habari mara moja. Sisi tuko chumba kingine tukisubiri maelekezo zaidi kutoka kwa wazee.

"Haya asante, lakini naomba asiamke wakati nikiwa peke yangu. Nasikia mtu huyu ni hatari kubwa kabisa'.

"Wewe mwoga sana. Mtu aliyefungwa kiasi hiki unafikiri atafanya nini hata akiamka, labda awe na nguvu za kishetani".

"Huenda anazo".

"Kama anazo basi pole, yatakuwa matatizo yako".

Nikiwa katika kusikiliza mazungumza haya kidogo nicheke. Yule mtu mwingine alitoka, akabaki mlinzi mmoja ambaye alifunga mlango na kuzima taa, halafu akakaa kwenye kiti. Nilisubiri kama dakika kumi hivi nikaanza kukoroma. Yule mlinzi aliinuka na kuwasha taa na kunisogelea kitandani wakati mimi bado nimefumba mamcho. Kule kuhema kwake ndiko kulinifanya nijue yuko karibu.

"Wewe umeamka", aliuliza kwa wasiwasi, nilifungua macho yangu kwa chati nikaona alikuwa ameshika bastola akiwa amelenga kifuani pangu. Nilifanya mahesabu ya namna ya kumwingia mtu huyu nikapata.

"Ndiyo", nilijibu kwa unyonge.

Niliona macho yanamtoka, nikaona mtu huyu ameingiwa na woga na anaweza kunipiga risasi shauri ya woga nisipomwahi. Hivyo kama chui nilimrukia na wakati ule ule nikawa nimepiga bastola yake ikaanguka upande mwingine na nikampiga pigo la mkono la karate katikati ya kichwa akafa bila kujua nini kimemwua. Niliindea bastola yake, nikamvua joho lake jekundu, nikalivaa, kisha nilifungua bastola nikakuta funguo na risasi za bastola hii. Nilifungua bastola nikakuta ina risasi tatu tu nayo ina uwezo wa kubeba kumi. Hivyo niliijaza risasi, kisha nikachemsha kidogo viungo vyangu tayari kwa kupambana na watu walioko chumba kingine. Kichwa kilikuwa bado kinaniuma lakini hakikuwa tishio kubwa.

Nilizima taa, nikajaribu kufikiri nilipo lakini nikaona bila kwenda nje haingenisaidia. chumba hiki kilionekana kilikuwa ni stoo ya vitu, hivyo nilihisi hapo nje kuna ofisi na nilifikiri kuwa ndicho chumba cha pili alichokuwa amezungumzia yule mlinzi wa pili. Nilifungua mlango taratibu, niliangalia hali mara moja nikajua hizi zilikuwa sehemu za nyuma za bohari, au ofisi. Maana kulikuwa na chumba kinatazamana na stoo hii, halafu kulikuwa na vyumba vitatu mbele tena kwa upande wa kulia. Upande wa kushoto kulikuwa na mlango wa kutokea uwani.

Nilisikia watu wanazungumza kwenye chumba kilichokuwa kinaangaliana na mahabusu yangu. Nikajua ni hiki chumba alichozungumza yule mlinzi. Nilijiweka

tayari kisha nikagonga. Mimi niliamini watajua ni mwenzao hivyo wangekuja bila tahadari kufungua mlango.

"Ngwishe", nilisikia sauti ikiita.

"Ndiyo", nilijibu kwa sauti nzito.

"Ameamka?".

"Bado".

"Funguo tu mlango haukufungwa", nilijibiwa.

Basi bastola yangu ikiwa tayari mkononi, nilifungua mlango na kuingia ndani. Kweli watu wote sita walikuwa wamwezunguka meza wanakula. Waliponiangalia na kunitambua mimi ni nani wengine chakula kiliwadondoka toka midomoni.

"Endeleeni kula, mbona mnaacha", niliwatania.

Mmoja wao alimkonyeza mwenziwe wakifikiri mimi sikuona kumbe hawakujua macho ya Willy yamefundishwa kuangalia kila mahali kwa wakati mmoja utafikiri kinyonga. Yule aliyekonyezwa alitoa bastola haraka sana lakini mimi nilijua anataka kufanya nini na kabla hata sijamtahadhalisha alikuwa tayari kufyatua, lakini mimi nilikuwa mwepesi zaidi nikampata. Wakati yeye alipofyatua risasi alimpiga mwenzake na kumwua. wawili tayari walikuwa wamekufa.

Pale pale wengine wote walisimama kila mtu akitoa bastola. Lakini niliwawahi watatu halafu nikaona yule wa nne macho yake yanaangalia mlango. Mara moja nikaanguka chini na risasi ikanikosa kwa nyuma ikapita na kumpiga yule wa nne na kummaliza, mimi pale pale nikajiviringisha na kumwahi yule wa nje. Lo nilikuwa nimeponea chupu chupu, maana kama nisingewahi kulala chini, vile vile ningekwenda kuonana na Veronika mpenzi wangu kama kweli watu huwa wanaonana tena huko ahera.

Nilitoka ndani ya jengo hili upesi upesi. Nilipofika nje nikaona niko kwenye mabohari ya Chang'ombe. Bohari hii ilikuwa imezungukwa na ua wa matofali. Nilivua joho jekundu nikapanda ua nikatokea katika uchochoro nikaanza kukimbia. Nilikadilia kuwa ilikuwa yapata saa kumi na moja. Nilipofika mbele ya bohari nilikuta ni mali ya Kampuni moja ya matairi ya magari iitwayo "Trans World Tyres", kwa sababu sikutaka kufanya uchunguzi zaidi kutokana na hali niliyokuwemo niliona teksu nikaipungia ikasimama na kumwamuru dereva anipeleke Independence Avenue haraka.

"Ohuu. Bosi umetokea wapi?". Linda aliuliza huku akitoa pumzi ndefu ya kuonyesha wasi wasi aliokuwa nao umemtoka.

"Nimetoka mahabusu".

"Pole sana bosi".

"Usinipe pole sasa hivi, mapambano bado kabisa yanaendelea, utanipa pole nikiweza kumaliza mapambano haya kwa usalama. Eddy yuko wapi?".

"Yuko katika shughuli za kujaribu kukutafuta apate kujua uliko. Lakini kila baada ya muda mchache anauliza hapa".

"Akipiga tena simu mwambie arudi haraka. Je Sherriff yuko wapi?".

"Wote wako pamoja".

"Haya kaniletee Sandwich za nyama ya kuku na niwekee glasi ya whisky ofisini kwangu. ninakwenda kunawa kidogo".

Baada ya kumaliza kunawa niliingia ofisini kwangu na kuanza kunywa whisky na Sandwich alizokuwa ameleta Linda.

"Chifu yuko?", niliuliza.

"Amesema muonane saa moja bila kukosa", Linda alijibu.

Mara simu ililia ofisini kwa Linda. Linda akashika simu yangu iliyokuwa imeunganishwa na yake. Alibonyeza kidude kimoja baada ya kuinua mkono wa simu.

"Hello nani hapo?", Linda aliuliza".

"Oh Eddy, rudi hapa haraka Bosi yuko hapa. Yuko hai kabisa ameketi kwenye kiti chake anakunywa whisky"....

"Haya asanhte", Linda aliweka simu huku akicheka.

"Nakwambia bosi ungesikia sauti ya Eddy niliposema uko hapa. utafikiri mtu aliyekwamwa na mwiba wa samaki".

Simu iliita tena ofisini kwa Linda na Linda akachukua simu.

"Hello nani hapo?", Linda aliuliza. "Ehe Unasemaje Issack... Eddy bado hajafika hapa, lakini atafika muda si mrefu, na kama una habari muhimu Bosi yuko hapa".

"Oke, njoo haraka sana", Linda alijibu na kukata simu.

"Vijana wa Eddy aliokuwa amewasambaza, huyu Issack na mwenziwe ndio walikuwa na jukumu la kuangalia mienendo ya Sikazwe", alisema Linda.

"Ghafla mlango wa ofisi yangu ulifunguliwa, Sherriff, Eddy na Zabibu wakaingia ndani.

"Pole sana Bosi, sisi tulijua kwa uhakika kuwa utakuwa msambweni", Eddy alitoa pole.

Linda na Zabibu waliangaliana kwa jicho baya. Inaonekana Linda hakunda Zabibu kuja ofisini kwa bosi wake.

"Huyu anakuja kufanya nini, si afadhali angalikaa nyumbani, akawaachia wanaume hawa kazi hii. Mara nyingine kutembea na wanawake katika mapambano kama haya kunaweza kuleta mkosi".

"Mimi sina mkosi. Pilipili usiyokuwa inakuwashia nini?. Shughulika na mambo yako dada na mimi nitashughulika na yangu, usinijue kabisa", alijibu Zabibu kwa hasira.

"Haya basi yaacheni hayo mambo ya kitoto hapa tuko kazini. Sitaki kusikia uchafu mwingine wowote", niliwaonya.

Nilianza kuwaeleza yaliyonipata toka mwanzo mpaka mwisho. Nilipomaliza kuzungumza tu Issack akaingia.

"Ehe tupe maelezo", Eddy alimdai.

"Nitaanza toka jana usiku kwa faida ya wale ambao hawakupata habari hizo toka mwanzo. Sikazwe tulianza kumwona mnamo saa tisa za usiku akitokea barabara ya Bagamoyo. Alielekea moja kwa moja nyumbani kwake na hakutoka tena mpaka saa sita za mchana. Mnamo saa sita hivi aliondoka akaenda kula chakula cha mchana. Aliporudi mnamo saa saba hivi alikuja na lori dogo tani tatu likimfuata nyuma. Alifungua mlango na kuanza kutoa mizigo iliyofungwa kama mtu anayehama. Baada ya kujaza gari hili, liliondoka na nikamwambia Ismail alifuate. Ismail aliporudi alisema mizigo hiyo imetelemshwa kwenye bandari ndogo yaani pale ngalawa na meli ndogo ndogo zinapopakia mizigo yao.

"Yaani mizigo hiyo ilikuwa imefungwa kisafari?".

"Ndio".

"Haya endelea".

"Kiasi cha saa tisa hivi walikuja watu wawili ndani ya gari, mmoja Mzungu mwingine mwafrika. Walikaa kama dakika tano tu wakaondoka. Nilimwambia Ismail awafuate. Walielekea barabara ya Bagamoyo, Ismail aliporudi alisema watu hawa waliingia barabara ya Kilimani na kuingia nyumba moja inayotazamana na Hosteli ya Tazara. Sikazwe hakutoka. Mnamo saa kumi na moja hivi alikuja mtu mwingine na gari akazungumza nae mlangoni. Maneno aliyosema yalionyesha kumkasirisha Sikazwe maana alimsukuma, na yule mtu haraka haraka akaingia ndani ya gari na kuondoka....

"Ismail alimfuata huyu mtu lakini mtu huyu aliingia Estiennes Hoteli na kuanza kunywa pombe, hivyo akamwacha akarudi. Wakati natoka Sikazwe alikuwa bado yuko ndani lakini nafikiri atatoka maana alichukua debe la mafuta ya petrol akajaza gari lake".

"Kazi nzuri umefanya".

"Asante", alijibu kwa furaha sana.

"Eddy nitayarishie gari, hapana Issack nitatumia gari lako mimi na wewe tutakwenda kumfuata Sikazwe, popote atakapokwenda. Sherriff Eddy na wengine mnisubiri hapa hapa nitarudi ila mjitayarishe kwa usiku wa kazi", niliwaeleza lakini niliona wanashangaa.

Kabla hawajaanza kusema mengi nilimwambia Linda. "Mwambie Chifu anisubiri kidogo nikichelewa kufika saa moja".

Nikatoka nje pamoja na Issack nikawaacha wamepigwa na butaa.

Niliangalia saa yangu ilikuwa saa kumi na mbili na dakika tano na kwa majira ya wakati huu ya Dar es Salaam giza lilikuwa limeingia. Tulipofika kwa Sikazwe tu tulimwona naye anafungua mlango wa gari akaweka mkoba wake ndani, kisha akaingia na kuwasha gari moto. Sisi tuliegesha gari letu kama watu wanaopunga hewa pwani saa za jioni kwani vile vile kulikuwa na magari mengine. Alipoondoka tu Sikazwe sisi taratibu tulimfuata.

Mimi ninapomfuata mtu hata awe na ujuzi wa namna gani hawezi kunitambua. Sikazwe alituongoza mpaka kwenye nyumba hii ambayo Issack alisema ilikuwa karibu na Hosteli ya tazara. Alipiga honi mbele ya lango kubwa. Tukaona askari anakuja kumfungulia akaingia ndani. Majibwa mawili makubwa yaliandamana na askari huyu. Sisi tulienda na kuegesha gari letu mbele ya baa ya Hosteli ya Tazara. Mtu yeyote angedhani tuko humo katika baa, tunakunywa.

"Unayo bastola yenye seilensa?", nilimwuliza Issack.

"Ndiyo".

"Nipe. Wewe ningoje hapa lakini uwe katika tahadhari kitu chochote kikitokea njoo haraka, umenielewa.

"Hamna wasiwasi bosi".

"Kazi ninayokwenda kuifanya ni ndogo ila majibu ndio yananipa wasiwasi".

"Nakutakia kheri, bosi".

"Nafikiri nitaihitaji".

Niliondoka na kwenda kwenye nyumba ile. Mbwa walikuwa wanabweka kila gari linapopita mbele ya ile nyumba. Niliona hii itanisaidia maana hata wakibweka halitakuwa jambo la ajabu. Niliangalia wapi upepe unatoka nikaona ulikuwa unatoka Mashariki kwenda magharibi, hivi nikaamua kuingia nyumba hii kutoka magharibi kuzuia mbwa wasije wakaninusa. Nyumba ilikuwa imezungushiwa ua wenye seng'eng'e zenye miba upatao urefu wa futi sita kwenda juu. Kati ya mafunzo yangu makubwa kuruka ilikuwa mojawapo. Nilikuwa naweza kuruka futi saba wakati mwingine nane. Hivyo nilirudi nyuma nikaruka juu ya seng'eng'e na kutumbukia ndani ya ua bila kishindo maana nilitanguliza mabega.

Nilikumbuka kuwa kibao nje la lango kubwa kilikuwa kimeandikwa jina la Tony Harrison, hivi nilijua huyu ndiye mwakilishi wa Euro-Afro. Zabibu aliwahi kunieleza habari hizi. Walivyokuwa wanahusiana na Sikazwe ndicho nilikuwa nimekuja kutafuta. Kwanza ilinibidi nitoe kikwazo kimoja yaani askari mlinzi na mbwa. Nilisikia mbwa wanabweka mbele ya nyumba, hivyo nilijibanza kwenye ukuta wa upande huu wa magharibi halafu nikanyata pole pole mpaka kwenye kona ya ukuta na mbele. Nilichungulia nikaona askari mlinzi pamoja na mbwa wake wawili. Nilikohoa yule askari akastuka akaangaza huku na huko asione kitu maana mimi nilikuwa nimeganda kama kupe kwenye ukuta. Ili kuridhisha mashaka yake alikuja upande niliokuwa akifuatana na mbwa. Alikuwa na bunduki mkononi, kwa umbo lake nikajua ni 'SAR'.

Alipofika karibu kabisa na mimi niliona mbwa wanainua mikia nikajua tayari wameninusa. Nililenga bastola yangu nikawaua wale mbwa kwa kuwapiga katikati ya vichwa kwa upesi sana kwamba yule askari alishangaa kuona mbwa wanaanguka hata bila kubweka. Alipogeuka na kuniona tayari alikuwa amechelewa, nilimrukia nikamkaba kabali taratibu mpaka alipokufa bila kutoa

sauti. Nilivuta mizoga ya majibwa haya na maiti ya yule askari na kuyaweka kando ya ua upande wa magharibi kwenye seng'eng'e. Nikiwa nimeridhika na hatua yangu ya kwanza. Sasa nilichukua hatua ya pili.

Nilianza kuzunguka nyumba kwa nyuma nikielekea Mashariki. Sikwenda mwendo mrefu kabla sijafika mahali nilipokuwa ninapahitaji. Nilikuwa nimefika nje ya sebule na dirisha la nyumba lilikuwa wazi, na nikasikia mazungumzo ya huko ndani kama nami niko pale pale. Hivyo nilibana tena kwenye ukuta nikaanza kusikiliza mazungumzo.

"Lakini Tonny, mimi nimrjitshidi sana lakini huyu mdudu Gamba na kundi lake amewaua watu wangu wengi sana. Fikiria Shuta na Mlambo wameuawa. Nadhani nisingejitahidi zaidi ya hapo. Lakini hata hivyo bado nina watu wa kutosha kutekeleza kazi hii. Usiku huu huu itakwisha, usiwe na shaka.

Hii ilikuwa sauti ya Sikazwe.

"Sawa Ray, lakini naona ungejitahidi zaidi ya hapo maana lazima ile meli ndogo iondoke saa tisa za usiku ili kuwahi meli yetu ya Euro-Afro Mtwara usiku wa kesho. Tayari rubani wa meli hiyo ana habari na mpango wa kutoa mizigo ndani ya meli ndogo (scooner) na kuingiza katika meli hiyo huko Mtwara haina uangalizi sana kama bandari ya Dar es Salaam", Tonny alisema.

"Vizuri mimi nitajitahidi, tayari mizigo yote imefungwa vizuri, imebaki kusafirisha tu kwenda kwenye bandari ya meli ndogo".

"Nimepata habari kuwa unangojewa kwa shangwe na wakuu wa serikali ya Afrika Kusini. Nimewaeleza mipango yote, na wao wako tayari kuzungumza na chama chako ili damu isimwagike Nchini. Wamefurahi sana kwa kazi yetu ya kuweza kuziiba silaha za hatari ambazo zingewa wananchi wa Afrika Kusini bure, kumbe mnaweza kufikia maafikiano ya kubadilisha siasa ya Serikali ya Afrika Kusini kwa mazungumzo", Tonny Harrison alieleza.

"Na mimi nimeona ni wenda wazimu kuendeleza vita dhidi ya Afrika Kusini kwa njia ya mapambano. Lakini bado chama cha PLF kitaendeleza mapambano. Chimalamo ni mtu mwenye nia ya kuuza ubaguzi wa rangi kwa mapambano na mtutu". Sikazwe alionya.

"Si wewe unajua vitu vyao vyote na namba ya askari wao na mafunzo waliyopata askari wao pamoja na silaha walizonazo.

"Ndiyo, najua kila mbinu ya jeshi lake maana mwaka jana Kamati ya Ukombozi ya OAU ilitaka kutuunganisha. Hivyo tulipewa fursa ya kuelezana kikamilifu hali ya mali ya kila Chama kwa mwenzake. Tulikuwa wote tumekubali kuungana tukaeleza siri zote za vyama vyetu. Ni wakati tu tulipokuja na maoni ya namna ya kuweza kufikia hali ya kubadili siasa ya ubaguzi bila kumwaga damu, ndipo nilipokataa tena mpango huo wa kuunganisha vyama. Nilidai kuwa siasa ya Chama cha PLF na chama changu zilikuwa na tofauti za kimsingi ambazo hatukuweza kukubaliana. Huu ulikuwa uongo lakini ulikubalika ikaonekana tuendelee hivi tulivyo ili mradi wote tuna nia moja kwa hivyo siri zote za PLF ninazo.

"Kwa hiyo siri zote za PLF unazijua na kwa sababu wewe umejiunga na serikali ya Afrika Kusini itakuwa rahisi sana kuwateketeza wapigania uhuru wa PLF wasijaribu tena. Yaani litakuwa pigo kubwa kiasi kuwa kuweza kuimarisha chama chao kianze mapambano tena, lazima itawachukua muda mrefu, na wakati huo Ray utakuwa uanatawala pamoja na wazungu huko Afrika Kusini". Sikazwe alitoa kicheko.

"Msiwe na wasiwasi mimi nitakuwa nao bega kwa bega kuleta hali nzuri katika Afrika Kusini na nitakuwa mstari wa mbele kupinga harakati za ukombozi ambazo wakati huo zitakuwa hazina maana".

"Kesho ndiyo siku kubwa kwako utakapoingia Pretoria na kuwekewa zulia jekundu", Tonny alisema kwa sauti ya kejeli.

Bila kutambua ile kejeli Sikazwe alijibu. "Ninaisubiri kwa hamu sana. Magari yale yaliyofanya kazi tayari yamebadilishwa rangi za jeshi la Tanzania. Kwa hiyo saa nne inaweza kupitia Intercontinental Motors na kuyachukua ili kubeba ile mizigo toka bohari mpaka bandari ndogo".

"Tayari Max ameisha waarifu, au siyo ?", Tonny aliuliza.

Niliinuka taratibu kumwalia huyu Max nikamtambua; ni yule aliyetukimbia kule kwenye uwanja wa Saba Saba.

"Mara hii nitakupata", nilijisemea moyoni maana mara moja alinikumbusha Veronika.

"Ndiyo, gari ziko tayari", Max alijibu.

"Oke mimi ninakwenda kijitayarisha saa tatu unusu ndipo nitatoka nyumbani kwangu kuelekea kwenye shughuli.

"Je kuna wasiwasi wowote?", aliuliza Tonny.

"Hamna taabu, tayari watu wa Forodha wanajua tunapeleka spea za magari Mtwara na tumeishazungumza nao vizuri hamna taabu".

"Lakini usimsahau Gamba na wenzake", Tonny alikumbusha.

"Usiwe na wasiwasi nina askari zaidi ya mia ambao wamefundishwa mafunzo ya juu hapa hapa Tanzania. Kama Gamba na wenzake wanataka kifo vema, na waje watuingilie watakiona kilichomtoa kanga manyoya shingoni".

"Oke nakutakia upakuzi mwema".

"Max, kwa sababu wewe ndiye kiongozi wa meli hii ndogo uwe macho kusije kukatokea kosa", Tonny alimwonya.

"Wewe unanijua sifanyi kosa mara mbili", alijigamba Max.

"Haya Sikazwe nafikiri saa tisa na nusu tutaonana hapa sitalala nitakusubiri".

"Usiwe na shaka", alijibu Sikazwe huku akisimama.

"Lo, nipe tiketi yangu ya ndege kabisa".

"Chukua hii hapa imelipiwa na serikali yako unakokwenda kuwa kati ya watu wakubwa watakaoongoza nchi yenye nguvu kuzidi zote katika Afrika".

SURA YA KUMI NA NNE

SIKAZWE na Max walimwaga wakafungua mlango wakatoka nje. Tonny Harrison alibaki ameketi kwenye kiti. Kwa vile nilikuwa na wasiwasi kuwa wangeshangaa kutomwona askari mlinzi na mbwa wake, nilitoka pale dirishani nikazunguka mbele. Kwa bahati nzuri hawakushughulika kumwita askari, ila Max alikwenda akafungua mlango, Sikazwe akapitisha gari langoni, halafu Max akarudisha mlango na kuingia ndani ya gari wakaondoka.

Mimi nikaona nimepata wakati mzuri wa kuzungumza na Tonny Harrison. Nilipoangalia saa yangu nikaona ni saa moja na nusu. Saa mbili zilikuwa zinatoshia kumaliza shughuli zangu na Tonny Harrison kabla sijamfuata Sikazwe hapo saa tatu na nusu. Nilifungua mlango taratibu maana ulikuwa umerudishiwa tu bila kufungwa kwa ufunguo. Nikiwa na bastola mkononi niliingia sebuleni na kumkuta Tonny Harrison ameinamia meza anasoma faili.

"Habari za kazi Tonny Harrison?".

Harrison aligeuka na kujikuta anaangalia katikati ya mdomo wa mtutu wa bastola. Pale pale aligeuka sura. Kwanza ikawa ya manjano kisha ikageuka ikawa nyekundu kama mtu aliyechapwa kofi usoni. Unajua hawa wenzetu weupe akichapwa kofi muruwa uso hugeuka na kuwa mwekundu. Alitaka kutamka neno akashindwa. Niliona alikuwa hategemei kabisa maisha mwake kukutana na wakati kama huu ambao alijikuta anatazama mdomo wa kifo.

"Habari gani?. Au umekuwa bubu?".

Nilisogea taratibu huku bastola yangu ikiwa imemlenga katikati ya uso wake. Kwa kigugumizi alijibu. "Nzuri....".

"Telemka hapo kwenye meza njoo tukae hapa kwenye makochi nina mazungumzo ya maana na wewe kabla sijaondoka".

Bila kusita aliinuka kwenye kiti na kwenda kukaa kwenye kochi. Wakati wote huu mdomo wa bastola haukumwachia hata chembe ya nafasi. Nilikwenda pale mezani alipokuwa ameacha faili nikalichukua. Nilikaa upande mwingine wa makochi tukawa tunaangaliana ana kwa ana.

"Bwana Harrison natumaini tumewahi kuonana?".

"Ndiyo, nafikiri tulionana kwenye tafrija iliyoandaliwa na Lion Club Hotelini Kilimanjaro".

Nikaweka bastola yangu kwenye paja huku macho yangu yakiwa yanamwalia kwa makini.

"Na si mara moja au mbili?".

"Nafikiri ni mara nyingi".

"Nasikitika kusema kwamba leo sikuja kwenye tafrija ila nimekuja kuzungumza nawe kwa ajili ya suala la hatari ambalo wewe unalijua vizuri zaidi.

Faili niliyoichukua kwenye meza ilikuwa imeandikwa "SIRI" halafu kichwa cha faili kiliitwa "OPERESHENI HUJUMA". Mara moja nikajua katika faili hili ndimo kulikuwa na maelezo yote ya jinsi tukio hili lilivyofanywa na hawa majahiri. Ule ulikuwa ni ushindi thabiti hivyo niliweka faili kwenye mapaja yangu.

"Sina haja ya kujitambulisha kwako kuwa sasa hivi nimekuja kukuona kama nani, kwa sababu natambua unaelewa, au sivyo".

Ndiyo".

"Bila kupoteza muda ningependa kujua, bwana Harrison, wazo la kuziiba silaha za wapigania uhuru mkiwatumia wapigania uhuru wenyewe limetoka kwa Makaburu au kwa mataifa ya Magharibi?".

"Kwanza kabla sijajibu swali lako nataka kutoa mshangao wangu kwako jinsi ambavyo umeweza kupeleleza na kugundua jambo hili ambalo lilitayarishwa kwa mbinu za hali ya juu. Mimi ningependa unieleze kwanza jinsi ulivyoweza kupeleleza mpaka kunifikia mimi kitu ambacho sikutegemea kabisa. Nafikiri baada ya hapo unaweza kunifanya unavyotaka kwani hili faili uliloshika lina kila kitu. Sina hata haya ya kukueleza mengi; yote utayakuta humo".

Mpaka sasa nilishatambua kuwa Harrison hakuwa mtu mwenye ujuzi wowote katika mambo ya kijasusi ila alikuwa ametumiwa tu kwa sababu ndiye mtu pekee ambaye angeweza kutekeleza jambo hili bila kushukiwa, na kweli kwa muda wa miezi sita alikuwa amefaulu kutotambulikana.

"Sawa, bwana Harrison. Nafikiri nitaanzia toka mwanzo ninavyofikiri ndivyo mambo yalivyokuwa mpaka kufikia hali hii.

"Mnamo miezi sita iliyopita Rais wa Chama cha wapigania uhuru kiitwacho PLF, Ndugu Cicil Chimalamo, alitembelea Urusi kwa nia ya kutafuta msaada wa kijeshi; yaani silaha kwa ajili ya mapambano yaliyokuwa yameanza dhidi ya serikali ya Afrika Kusini.

"Kwa vile Ndugu Chimalamo alikuwa na habari zote kuhusu nguvu za kijeshi za serikali ya Afrika Kusini ilizonazo alitoa maombi yake kwa serikali ya Urusi ili aweze kupatiwa msaada wa silaha za kisasa walizonazo Makaburu. Ombi hili la Ndugu Chimalamo lilikubaliwa na serikali ya Urusi na akaahidiwa kupatiwa silaha hizi katika muda wa miezi sita. Na kwamba katika muda huo silaha hizi zitakuwa zimewasili Dar es Salaam".

Akiniangalia kwa makini, nilitoa pakiti yangu ya sigara ya aina ya Tropicana, nikatoa sigara mbili, moja nikampa na nyingine nikavuta mwenyewe, kisha nikaendelea.

"Kwa kutokana na mbinu za kisasa za kijasusi za mashirika ya kijasusi ya nchi za Magharibi habari hizi zilinaswa. Ziliponaswa habari hizi ndipo nchi za Magharibi zilipopasha habari serikali ya Makaburu tishio lililokuwa linakuja dhidi yao. Hapo ndipo serikali ya Makaburu ilipokaa chini na kufikiri nini la kufanya. Uamuzi wa Makaburu ukawa wa kufanya ujahiri huu ndilo lilikuwa tatizo. Lakini baada ya kulishughulikia suala hili ambalo nafikiri walitupiwa wakuu wa shirika la ujasusi, yaani "BOSI", walifikiria mbinu za hali ya juu na kuamua kuwa kwa kutumia mbinu hizi wangeweza kufaulu kuziteka silaha hizi kabla hazijafika mikononi mwa wapigania uhuru. Bashiri yangu ni sawa na vipi?".

"Mpaka sasa hujakosea kitu", alijibu.

"Makaburu ni wajanja sana na wanawajua wakuu wa vyama vya wapigania uhuru vizuri sana. Hivyo waliamua kumtumia mkuu mmoja wa wapigania uhuru ambaye walikuwa wanajua kuwa hakuwa na msimamo kamili, kwa vile walimjua alikuwa hapiganii hasa ukombozi wa waafrika wanaoonewa huko Afrika Kusini bali alikuwa akipigana ili apate cheo. Ukubwa na kujaza tumbo lake ndio ilikuwa nia yake. Hivyo waliamua kumtumia bwana Ray Sikazwe wa Chama cha SANP, ambaye ndiye alipatikana na sifa hizi walizozitaka. Walipofikia hapa kilichokuwa kimebaki ni namna gani watamwingia na kuweza kumridhisha kweli akisaidiana nao katika kuhujumu vyama vingine angepata kila alichokitaka. Hapa ndipo walipohitaji msaada wa nchi za Magharibi na hapo ndipo wewe Harrison ulipoingizwa katika njama hizi".

Nilinyamaza kidogo kiasi chs kupitisha mate.

"Kampuni yenu ya Euro-Afro ni kampuni kubwa sana, na ina rasilimali nyingi katika Afrika Kusini. Inamiliki madini ya maangamizi, chromiumu na platinumu katika Afrika Kusini. Na Afrika Kusini ndiyo nchi pekee isiyo ya kikomunisti inayotoa madini haya ambayo yanahitajika sana katika viwanda vya nchi za Magharibi. Hivyo serikali ya Makaburu ilizungumza na nchi za Magharibi zizungumze na kampuni yenu ikiwa na kisingizio kuwa kama wapigania uhuru hawa wakipata silaha hizi si serikali ya makaburu tu itaangamia, bali nchi za Magharibi zilizo na rasilimali zao nchini humo nazo zitapoteza mali zao. Kwa hivyo swala hili lilikuwa muhimu kwa nchi za Magharibi kama ilivyo kwa serikali ya Makaburu.

"Kwa vile Kampuni yenu inamiliki makampuni mengi katika nchi mbalimbali za kiafrika na mojawapo ikiwa ni Tanzania, hivyo ilionekana ndiyo kampuni pekee ambayo ingeweza kusaidia katika suala hili. Hivyo wakubwa wako waliarifiwa juu ya suala hili na hatari zake kama halitaweza kushughulikiwa haraka na kwa kikamilifu. Kwani hatari hii isingekuwa kwa Afrika Kusini tu ila pia Kampuni hii ya Kibepari ingeweza kupoteza mali zake zote ikiwa wazalendo watashinda vita vya ukombozi. Kutokana na sababu hizi wakubwa zako walikubaliana na Makaburu kuwa kulikuwa na haja ya kushirikiana ili kulinda maslahi ya Makaburu na nchi za Magharibi. Hapo ndipo ulipopashwa habari namna utakavyoshughulikia suala hili. Mpaka hapo maelezo yangu ni sawa au vipi?."

"Sijui ulijuaje?, endelea maana nashangaa sana jinsi Afrika huru ilivyoendelea katika upelelezi".

"Habari zilipokufikia pamoja na plani yote ndipo ulipomwita bwana Ray Sikazwe na kumweleza kama ulivyoelekezwa. Ndipo ulipomdanganya kuwa serikali ya Makaburu iko tayari kufanya mazungumzo na chama chake ili wafikie uhuru wa walio wengi kwa mazungumzo bila mapambano, ila kwanza atimize sharti moja. Sharti hilo ni kusaidiana kati ya majasusi wa "BOSI" ambao wataingia Tanzania kama wanachama wa chama chake na kundi lake la wapigania uhuru lililokwisha kufundishwa mbinu za vita katika kuziteka silaha za chama cha PLF ambazo zilikuwa zikitegemewa kuwasili mjini Dar es Salaam mnamo miezi sita hivi".

"Kwani unadhani Makaburu hawawezi kutafuta suluhisho la namna hii, baada ya kutambua kuwa umefika sasa wakati wa kuanza kuwachukulia waafrika kama binadamu wenzao?", Harrison aliuliza.

"Mimi najibu kuwa baso, kwani kama nia yao ingekuwa hiyo wasingetaka suluhisho na chama kimoja tu na kwa siri, wangelitangazia ulimwengu na kuomba vyama vyote vinavyohusika na tatizo la Afrika kusini vishiriki vyote kwa ujumla bila sharti lolote, la hasha, Harrison. Hizi zilikuwa mbinu tu za kuhujumu harakati za mapambano ya chama cha PLF ambacho kinaendelea na mapambano makali dhidi ya serikali ya Makaburu".

"Sawa nafikiri umenipa msingi wa mambo kama yalivyopangwa na serikali ya Afrika Kusini ikisaidiwa na nchi za Magharibi ambao ndio sisi. Lakini tulifaulu katika kuziteka nyara silaha hizi bila tatizo, je umekuja kugundua ni nani wanahusika?, ingawaje juzi tulipata habari kuwa wewe ni mpelelezi hatari lakini hatukuamini ungeweza kugundua kitu".

"Nitakueleza sasa. Nilipoanza upelelezi wangu siku ya kwanza tu niliona mwanga kwani mlikuwa mmefanya kosa. Kosa lenyewe lilikuwa ni kumwua kiki. Nilipokuta Kiki amekufa, tulianza kuchunguza habari zake tukakuta mambo yote aliyokuwa ameeleza juu yake si kweli, hivyo tukagundua alikuwa jasusi wa Makaburu waliokuwa wamefaulu kumweka katika ofisi ya za kamati ya Ukombozi ya OAU, na ni yeye aliyeweza kufanikisha jambo hili".

"Na mlijuaje kuwa mimi na sikazwe tunahusika?"

"Kosa jingine. Sikazwe nilipomwuliza kama anamfahamu Kiki alisema aliwahi kumwona mara moja tu wakati alipofika ofisini kwake na kumpeleka kwenye kamati ya Ukombozi ya OAU ili wamsaidie kazi. Sasa tulipofahamu kuwa Kiki alikuwa na rafiki msichana aitwae Zabibu nilimtafuta.

"Nilipofika kwake wakati mmemtuma mtu wa kwenda kumwua nikamkomboa. Yeye huyu binti alinieleza kuwa Sikazwe alikuwa rafiki mpenzi wa Kiki pamoja na wewe. Hii ilidhihilisha kuwa Sikazwe alisema uongo hivyo mara moja nikaanza kumhisi kuwa yumo katika mpango huu. Nilipojua kuwa kati ya makampuni yaliyo chini ya Euro-Afro ni pamoja na Intercontinental Motors ambao ni wakala wa magari ya "Benzi" nchini hapa nikawa na uhakika kabisa wewe unahusika. Maana magari yaliyotumiwa yalikuwa maloli makubwa ya aina ya Benzi ambayo ni sawa na yanayotumiwa na jeshi letu. Na magari yote ya jeshi kwa siku ile yameweza kufahamika yalikuwa wapi. Hivyo ikaacha sababu moja tu magari yaliyobeba zile silaha yalitoka kwenye kampuni yenu ya Intercontinental Motors ya jeshi pamoja na kuyaweka namba za bandia. Juu ya mavazi ya kijeshi wapigania uhuru wengi wanayo hivyo, hilo halikuwa tatizo kwenu. Una swali jingine?"

"Nafikiri umenielewesha vya kutosha na ninakupa hongera kwani kweli wewe ni mpelelezi maarufu si Afrika tu ila Ulimwengu mzima. Maswali mengine niliyokuwa nayo nimekwishajua majibu yake baada ya kuzungumza na wewe na kuamini mimi mwenyewe kuwa wewe huwezekani".

Ghafla mlango ulifunguliwa na Issack akaingia bastola mkononi.

"Karibu Issack samahani kwa kuchelewa nilikuwa na Bwana Tonny Harrison hapa ambaye ni mwakilishi wa kampuni ya Euro-Afro ambaye ndiye alikuwa kiongozi wa tukio la bandarini".

Niliangalia saa yangu nikaona ni saa mbili.

"SWali na mwisho Harrison, silaha mmezificha wapi?".

"Sikazwe ndiye anajua, na kama umeweza kufikia hapa sidhani utashindwa hatua ya mwisho".

"Haya simama twende zetu. Issack kaleta gari hapo mbele ya mlango".

Issack alitoka na Harrison bila matatizo alisimama na kuangalia sebule na vitu vilivyokuwemo kwa huzuni. Alitangulia mimi nikafuata nyuma. Nilipofika mlangoni nilizima taa, nikawa na faili kwapani na bastola ikiwa imemlenga Harrison. Nilirudisha mlango na kuelekea kwenye lango.

"Askari na mbwa wangu wako wapi?", Harrison aliuliza tulipofika kwenye lango.

"Sasa hivi wako sehemu ambayo mimi na wewe hatujafika lakini siku moja tutafika".

Issack alikuwa ameegesha gari mbele ya lango, Harrison alifunga mlango wa nyuma mimi nikamfuata na kukaa naye.

"Kwa usalama wako usijaribu kitu chochote", nilimweleza huku Issack anaondoa gari.

"Mimi hata bastola sijui kuinua, watu hawa waliniahidi ulinzi mkali na kwamba ingekuwa vigumu operesheni hii kushindwa. Kumbe wameniuza. Usiwe na wasiwasi na mimi, sijui mbinu yoyote mbele ya bastola".

Nikajua wakati wake wa kusema ukweli umefika.

"Vipi boshi?", Issack aliuliza.

"Kituo cha usalama kwa watu kama hawa".

Issack kwa sababu alielewa ni kituo gani cha usalama alikwenda moja kwa moja na kupiga honi tulipofika kwenye lango. Mlinzi alikuja akafungua lango sisi wote wawili tukatoa vitambulisho vyetu. Akastuka mara moja na kuturuhusu kuingia. Nilimwongoza Harrison mpaka kwenye ofisi ya kituo hiki cha usalama.

Nilipofika nilimkuta afisa wa zamu nikatoa kitambulisho changu, naye akastuka. "Ndio Mzee".

"Huyu mtu awekwe chini ya ulinzi mkali mpaka utakapopata maelezo tena".

Niliomba kitambulisho chake nikachukua jina, namba na cheo chake.

Alikuwa na cheo kikubwa. Kisha nilirudi ndani ya gari.

"Moja kwa moja ofisini, maana saa tatu na nusu ndipo kazi kubwa ya kukata na shoka inaanza".

"UHURU UTALETWA KWA MTUTU TU"

Tulipoingia ofisini tulikuta wanatusubiri kwa hamu.

"Chifu anataka kukuona", Eddy alinieleza.

"Mwambie Maselina haiwezekani, nitamwona baadaye. Sasa hivi hakuna nafasi maana tukichelewa hapa mambo yote yatakuwa yameharibika. Mwambie asitoke ofisini mpaka saa sita. Asipotuona ajue basi makubwa yametupata, akituona ajue tumerudi na ushindi. Umesikia Linda?".

"Nimesikia".

"Sherriff, Eddy na Isaack mko tayari kwenda kwenye uwanja wa mapambano", niliwauliza.

"Bila wasiwasi", walijibu kwa pamoja.

"Na mimi?", Zabibu aliuliza.

"Wewe utabaki hapa na Linda. Tutaonana saa sita kama tukiwa salama.

"Mimi nataka twende wote, kama ni kufa tukafe wote"

"Kwanini unataka ukafe naye kwani yeye ni nani wako", Linda alimuuliza kwa ukali.

"Acheni upuuzi, nyinyi bakini hapa, haya mambo ya kuleteana haraha, mtatupa mkosi bure".

"Twendeni zetu", niliwaeleza wenzangu nasi tukaondoka ndani ya ofisi na kuingia ndani ya gari.

Eddy ndiye alichukua usukani na Isaack akaa naye mbele. Mimi na Sherriff tulikaa nyuma.

"Twende moja kwa moja nyumbani kwangu tukachukue silaha zaidi. Halafu tutapita nyumbani kwa Eddy kuchukua silaha tulizoacha kule. Tuna saa moja ya kujitayarisha kabla ya kuingia kwenye uwanja wa mapambano.

"Itabidi tutoke kwa Eddy mnamo saa tatu na nusu. Hii itatupa nafasi ya kuwa nje ya nyumba ya Sikazwe saa tatu na nusu. Maana ndipo yeye ataondoka kuelekea huko walikoziweka silaha".

"Kisha niliwaeleza mazungumzo yote niliyoyasikia kati ya Harrison, Sikazwe na Max.

Kwa hiyo tutakuwa watu wanne tukikabiriana na zaidi ya watu mia", Isaack alisema kwa mshangao.

"Ndiyo sababu watu kama sisi tunaitwa ni hatari. Siku moja Isaack utakapokuwa komando kama mimi utakuwa na uwezo wa kukabiliana na maadui mia peke yako. Kwa hiyo mimi naona kama ni afadhali sana kama tuko watu wanne dhidi ya watu mia. Tukitumia hamasa na maadili na moyo wa kimapinduzi sina shaka Mungu atatusaidia na tutashinda na kufichua hizi njama za Makaburu na mabeberu ya jumuiya ya ulimwengu", niliwatia moyo.

"Nikiwa niko na wewe bos, huna sina wasiwasi wowote", Eddy alisema.

"Hata mimi", Sherriff aliongeza.

"Kama ni hivyo, hata mimi ninafurahi kuwa nina jeshi lililohai na kamanda wake".

"Kutokana na ulivyoeleza komredi, watu hawa walikuwa wamepanga kuzichukua silaha hizi kwa meli ndogo kama spea ziendazo Mtwara", Sherriff alieleza.

"Sawa".

"Baada ya kufika Mtwara wangepanya nini?", aliuliza.

"Swali zuri. Watu hawa walikuwa wamejitayarisha vizuri sana. Hili kampuni kubwa la Euro-Afro lina meli zake. Meli yake moja itakuwa inapakua mizigo Mtwara kuingia kesho. Hivyo walikuwa wamepanga kutoa silaha hizi kwenye hii

meli ndogo na kuzipakia katika meli kubwa ambayo ingelikwenda kuzitelemsha Afrika Kusini...

"Mipango yote hii iko ndani ya faili nililompa Linda ampelekee Chifu. Meli hiyo ingekuwa inangojwa bandari ya East London kutelemsha zana hizi. Sikazwe angeondoka kesho kwa ndege akidai anakwenda Botswana lakini angekwenda Pretoria ambako mimi nafikiri wangemtia ndani mana nia yao haikuwa kufanya kama walivyomdanganya ila tu walitaka awasaidie kuziiba silaha kwa sababu ilikuwa rahisi kwake".

"Kwa hiyo mpaka sasa Sikazwe anakazana bure tu", Isaack alisema huku akicheka.

"Wajinga ndio waliwao", Eddy alijibu. Tulifika nyumbani kwangu, nikabadilisha mavazi kuvaa mavazi ya kikazi yaani koti na suruali yenye mifuko mingi ili kuweza kubeba silaha za kutosha.

Baada ya hapo tukaelekea kwa Eddy ambako tulijitayarisha kwa kikamilifu. Kwa bahati nzuri tulikuwa na majoho mekundu matano tuliyoyateka kwa hawa majahili. Kila mtu alichukua joho moja, maana hii ingetusaidia kuwaingilia wakidhani ni wenzao. Tulipata vile vile kofia tatu ambazo niliwagawia wenzangu. Nakwambia tulipojaribu kuvaa tulifanana na wao kabisa. Hivyo tulichoomba ni kuwa tukute bado hawajabadili mvao wao unaowatambulisha. Baada ya kuona kila kitu kimekamilika tulijiandaa kuondoka huku roho zetu zikipiga haraka haraka.

SURA YA KUMI NA TANO

ILIKUWA saa tatu na dakika ishirini tulipoegesha gari yetu kando kando ya bahari huku tukiangalia nyumba ya Sikazwe. Tulimsubiri aanze safari yake hapo saa tatu na nusu. Gari lake lilikuwepo hivyo tuliamini yupo.

Saa tatu na nusu kamili kama alivyosema tuliona mlango wa mbele wa nyumba unafunguliwa Max ndiye alitoka kwanza akiwa amevalia joho jekundu na kofia. Roho yangua ilijawa na furaha. Baada ya muda kidogo Sikazwe akiwa amevaa suti nyeupe alitoka akafunga mlango, halafu wote wawili wakaingia ndani ya gari. Max ndiye aliyeingia upande wa dereva. Sikazwe akaa kwenye viti vya nyuma.

"Lo Sikazwe ameanza kupata heshima ya "VIP", Sherriff alisema na wote tukacheka.

"Yule aliyetoka kwanza alikuwa Max; anaonekana ndiye Kamanda wa jeshi hili la majahili, na haikosi ndiye aliyekwenda bandarini kama Meja Paul Liboi", niliwaeleza

"Bila shaka", alijibu Sherriff.

"Hamna taabu bosi".

Gari la Sikazwe liliondoka na kuingia Kenyatta Drive. Tulingoja mpaka lilipofika kwenye kona ya Barabara ya Bagamoyo ndipo tukamfuata. Nakwambia mimi nikimfuata mtu hata awe na ujuzi wa namna gani hawezi kutambua. Tulifuatana moja kwa moja wakashika barabara ya Upanga, halafu wakaingia barabara ya Azikiwe kisha wakaingia Azania Front na kutokea City Drive. Muda wote huu sisi tuliwafuata taratibu.

Kisha walishika barabara inayopita kwenye ofisi za usalama barabarani nikajua wanaelekea Kurasini. Nilishangaa kwanini hawakupita Intercontinental Motors kama walivyokuwa wamepanga, lakini nilihisi wamebadilisha mipango.

Walipovuka tu ofisi za polisi wa usalama barabarani, walisimama. Mara mtu akatokea kwenye kijinjia akaja na kuzungumza nao. Mimi niliwapita kasi mpaka kwenye mzunguko wa barabara hii na barabara ya Kilwa, Nikazungukia kulia na kuingia Railway Clab na kutoka. Sisi tukawa kama tunatokea mtaa wa Gerezani. Niliendesha polepole na mara nikawaona wanatokeza kuelekea barabara ya Kilwa nasi, tukawafuata.

Tulipofika kwenye njia panda ya Kilwa na barabara iendayo kwenye ofisi za Mamlaka ya Bandari ya Tanzania wao walichukua njia iendayo kwenye ofisi za Mamlaka ya Bandri.

"Nafikiri wamezificha Shimo la Udongo", alisema Isaack.

"La hashu, mbele ya ofisi za NOTCO na UDA kuna bohari la Intercontinental Motors, kwa hiyo bila shaka ndiko wanakokwenda", alisema Eddy.

"Sawa kabisa Eddy, umenitoa usingizini, saa zote hizi nafikiria wapi wameficha silaha hizi kumbe sehemu yenyewe iki wazi kabisa", Sasa sikiwa na haja ya kuwafuata karibu karibu. Tuliwaacha wakaenda mpaka wakapotea kwani sisi tuliingia ofisi za Mamlaka ya Bandari, na tulipoona wamepotea ndipo sisi tukatoka.

Bohari ya Intercontinental Motors lilikuwa nyuma ya mabohari ya kampuni ya NOTCO. Hivyo niliegesha kwenye ofisi za NOTCO. Mlinzi wa hapa alikuja kutuuliza. Mimi niliona huyu anaweza kuleta kidamisi hivyo alipoinamisha kichwa kwenye gari nilimpiga ngumi ya uso ambayo ingemfanya alale kwa muda wa masaa kama manne hivi kabla hajapata fahamu. Kisha wote tulitelemka na kumbeba na kumpandisha kwenye lori moja lililokuwa limejaa mizigo.

"Haya mabohari ya NOTCO yana walinzi hivyo itabidi tuzunguke tutokee upande wa barabara ya Kilwa ili kuepusha rabusha kabla hatujafika maana jinsi tulivyo watu wanaweza kufikiri sisi ni majambazi", Eddy alitoa ombi.

"Hapana, sasa hivi bado mapema hata tukionana nao watafikiri ni walinzi wa usalama tu. Ili tuwe kwenye hali ya usalama zaidi lazima wote tuwafanye wakalale kwa muda".

"Nami nilikuwa nafikiri hivyo maana wakisikia mapambano yatakapoanza wanaweza kuja kujiunga na kufa bure, au kupiga simu polisi wakaja kutuingilia kabla hatujafunga kazi sawasawa.

Hivyo rafiki zangu walinzi wote wa sehemu hii walilazwa usingizi wa masaa, sio wa NOTCO tu ila wa UDA, Shirika la Usagishaji na ofisi zote za karibu. Tulipoona kazi hii ndogo tumeimaliza tuliondoka hapo na kuelekea kwenye uwanja wa mapambano.

Tulitoka kwenye kichocho kimoja kati ya mabohari ya sehemu hii na kujikuta uso kwa uso na bohari ya intercontinental Motors. Tulikuta nje kuna malori matatu yanapakiwa kwa pamoja. Kulikuwa na watu wasiopungua ishirini, walikuwa

wanapakia mizigo kwa kupeana. Tuliona gari la Sikazwe lakini yeye hakuwemo, hali hii ilitujulisha kuwa yumo ndani.

Penbeni kidogo ya magari haya kulikuwa na walinzi. Walikuwa hatua kama ishirini kutoka kwenye magari yaliyokuwa yanapakia kwa kila upande; baadhi yao walikuwa wamejibanza kwenye ukuta wa mabohari haya na mengine wote wakiwa na bunduki mkononi. Habari nzuri wote walivaa majoho mekundu na kofia. Nilihisi kuwa kulikuwa na askari wasiopungua ishirini hapa nje.

"Nafikiri wote mmeona ulinzi ulivyo. Kitu ninachotaka ni kufanya mashambulizi kimya kwanza mpaka tutakapolazimika kuwashambuliwa watu wa ndani. Kwa upande huu giza linatusaidia hivyo walinzi wa huku haitakuwa taabu kuwapata. kuna walinzi kama sita waliobana upande huu. Mimi na Isaack tutashambulia kushoto, Nyinyi Sherriff na Eddy mtashambulia upande wa kulia. Nawatakia kheri".

Tulipeana mikono kimya kimya kwani hatukujua nini kitatokea. Mimi nilikuwa wa kwanza kujitokeza kwenye michongoma na kubana kwenye huu ukuta wa bohari jingine. Kama hatua tatu kulikuwa na mlinzi anavuta sigara huku macho yake yakiwa kwenye gari. Nilimsogelea kimya kimya. Nilipokuwa karibu kabisa nilimsemesha.

"Sijui watamaliza saa ngapi kupakia, mimi najisikia kuchoka".

"Sijui hata..." Aligeuza uso kunijibu, nikamkata karate ya shingo upesi upesi na kumlaza chini. Nikamwashiria Isaack alipojitokeza nikamwona Eddy naye ananyata kwenda upande wa kulia. Nilimnyooshea kidole kimoja kumweleza mmoja tayari nimepata. Yeye akanitolea alama ya vidole ya V kuonyesha ushindi.

"Wewe Isaack simama hapa hapa uwe kama wewe ndiye mlinzi wa hapa, mpaka nitakapokuonyesha ishara nyingine".

"Sawa", alijibu.

Mlinzi mwingine alikuwa hatua kumi hivi na hakujua nini kimetokea. Kwa vile nilikuwa nimevaa kama yeye alifikiri mimi ni mwenzake hivyo nilikwenda tu kama mmoja wao mpaka nilipomfikia.

"Vipi kuna wasiwasi wote?", nilimwuliza.

Aliinua kichwa.

"Hakuna....."

Kabla hajamaliza nilimkata karate ya katikati ya kichwa akafa palepale. Nilimwegemeza vizuri kwenye ukuta nikamwacha kama mtu aliye hai.

Nilimwunulia Isaack vidole viwili na yeye akawainulia Eddy na Sherriff ambao sasa nilikuwa siwaoni. Kumbe Eddy na Sherriff walikuwa wameenda kwa haraka zaidi, maana Isaack alinionyesha vidole vitatu kuonyesha wenzetu tayari walikuwa wameua watatu.

Hii ilinitia moyo sana. Upakiaji uliendelea bila wasiwasi. Mtu wa mwisho kwa upande huu alikuwa amebana kwenye kona kabisa ya ukuta wa bohari hii. Nilimwendea huku nikiwasha sigara. Na yeye alipoiona aliweka bunduki yake chini akatoa sigara.

"Sina moto afadhali umepita huku", aliniambia.

Mimi niliwasha kiberiti akaimana ili kuwasha sigara. Palepale nikamkata karate ya shingo. Bila hata kukoroma akakata roho. Nikamwegemeza ukutani halafu nikamfanyia ishara Isaack aje.

"Sawa wewe utasimama hapa mimi nawafuata walinzi wale watatu waliosimama mbele ya magari. Kama watashtuka mimi nitajitupa chini wewe wawahi". Halafu nikatoa funguo za gari.

"Pita hapa kichochoroni panda gari mpaka ofisini mwambie Chifu aje pamoja na Mkuu wa Polisi pamoja na askari watakaokuja kulinda na kuzihifadhi zana hizi baada ya mapambano. Umenielewa?".

"Sana. Nakutakia kheri".

Nilianza kutembea kuelekea kwa wale watu. Kabla hata sijafika nilisikia mlio wa 'SMG' kwa upande wa akina Sherriff. Nikajua mambo yameiva. Nikainua SMG yangu na kuwateketeza hawa walinzi waliokuwa mbele ya magari. Isaack hakupata hata muda wa kupiga risasi ila nilimwona anaingia uchochoroni na kupotea. Mimi niliruka juu ya gari lililokuwa karibu, nikakuta watu wanne walikuwa wanapanga masanduki ya silaha.

"Kumetokea nini?", niliwaauliza.

Wote waligeuka na kuniangalia. Pale pale nikawaachia risasi za kuwaua kisha nikaruka chini. Milio ya bunduki ilifanya watu wote watoke ndani ya bohari na kusambaratika hovyoy. Watu wote waliokuwa hapa juu walikuwa wamesharuka

chini. Niliweka sanduku moja kama kinga nikaanza kutungua mtu mmoja mmoja na bastola yangu nyenye sailensa.

Kwa vile hawakusikia mlio kutoka sehemu yangu watu walipiga risasi zao kuelekea upande kwa upande wa akina Sherriff. Nilipoangalia juu ya lile gari jingine nilimwona sherriff ameseimama juu na kuwashambulia adui kwa namna ya ajabu.

Nilimfanyia ishara akaiona na yeye akanifanyia ishara ya kuonyesha kuwa Eddy alikuwa chini anajaribu kuingia ndani. Kuona hivyo nilimfanyia ishara kuwa na mimi nakwenda ndani hivyo atuchunge wote. Tulikuwa tumeuwa idadi kubwa ya askari waliokuwa wamebaki ni wachache tu.

Niliruka chini huku nikiachia risasi ovyo hata niliweza kufika kwenye ukuta wa bohari lao. Nilitupa SMG nikajitupa kwenye mlango na kujiviringisha mpaka ndani ya bohari na kama umeme nikarukia nyuma ya sanduku kubwa na kuanza kujaza risasi bastola yangu. Huko nje nilisikia bado Sherriff anaendelea kumimina risasi ili kuwazuia wasitoke nje.

Nilipoinuka niliona kama kumbaki watu kumi tu ndani; wengine wote tulikuwa tumewateketeza. Nilimwona Eddy anaviringisha na kuingia ndani. Wale watu walimwona na kabla hawajapiga risasi niliwahi wawili, wengine wote wakarudi kujificha nyuma ya masanduku.

Eddy aliruka mpaka nilipokuwa.

"Asante bosi umeniponya",

"Usinishukru ndio sababu tuko wote. Kwanza kazi mliyoifanya wewe na Sherriff sikuitegemea. Kazi imekuwa rahis kabisa".

"Kuna watu kama wangapi humu ndani?".

"Hawazidi kumi, na wote wako upande wa Mashariki. Nafikiri wanamlinda Sikazwe na Max".

Huko nje kulikuwa kimya; Tukajua Sherriff anasubiri sasa kashi kashi kutoka kwetu.

"Sasa Eddy lazima tuwafanyie ujanja ili tuwapunguze. Mimi nitasimama juu ya hili sanduku ili niwadanganye. Walivyo wajinga walinzi wao watainuka ili wanipige risasi. Mimi nikiita tu jina kaa tayari na hii SMG yako kisha anza kumimina risasi. Mimi nitakuwa nimeisharuka kitambo, hivyo utawapata kama

mchezo. Usiogopea kuwa unaweza kuniumiza ninakuhakikishia kuwa nitakuwa sipo".

"Lolote usemalo bosi", Eddy alijibu huku anatayarisha bunduki yake.

Niliinuka kama umeme juu ya sanduku nikawaona wote mara moja.

Nikaita

"Sikazwe?".

Hapo hapo kama umeme nikaruka nyuma ya sanduku jingine. Walinzi wanne wainuka ili kunitupia risasi huku wakiwa wamejitokeza hadi vifua. Eddy alimimina risasi na kuwashindilia wote risasi katikati ya vifua vyao wakafa pale pale. Nilimwonyesha Eddy vidole kuwa wamebaki watatu, kwani nilipokuwa nimeruka juu ya sanduku niliona wako watu saba.

"Gamba, nilisikia sauti ya Sikazwe anaita.

"Unasemaje?", nilimwuliza.

"Naomba tuzungumze, vita umeshinda.

"Sawa Sikazwe, lazima ujuwe kuwa ukombozi wa Afrika Kusini utaletwa kwa mtutu wa bunduki tu, si mazungumzo.

"Walinidanganya".

"Hawakukudanganya, shida yako ni kwamba wewe ni kibaraka; yaani unapenda cheo kuliko watu wako. Matokeo yake ndiyo haya. Hata Makaburu wafanye njama za namna gani, mwisho wake wazalendo watashinda.

Wakati tukijibishana na Sikazwe, Eddy alikuwa anatambaa chini kuelekea pale walipokuwa.

"Tafadhali tuzungumze?", aliomba.

"Umechelewa, maana umeshaipaka matope Afrika, hivyo tutakupeleka mbele ya wanamapinduzi wa Afrika ndio watakao kuhukumu".

"Huwezi kunichukua hai".

Kumbe wakati huu tunajibishana Max naye na askari mwingine walikuwa wamejivuta karibu kabisa na mimi. Ghafla nikahisi kuna kitu karibu nami.

"Bosi", Eddy aliita ambaye pia alikuwa amewaona.

Kusikia tu hivyo niliruka pale nilipokuwa na wakati huo nikawaona Max na yule kijana mwingine karibu kabisa na mimi wameinua bastola tayari kufyatua. Nilijiviringisha hewani namna ambayo hata wao walishangaa risasi zao zote zikanikosa, wakati ule ule nikaachia za kwangu nikawapata wote nao wakaanguka chini.

Sikazwe aliinuka akasimama juu ya sanduku akachukua bastola akataka kujipiga risasi. Bastola tatu zililia kwa wakati mmoja na kuupiga mkono wake. Kumbe Sherriff nae alikuwa amefika mlangoni na kuona kitendo alichotaka kukifanya akakizuia. Eddy nae aliona akazuia wakati na mimi niliona nikazuia asijipige risasi.

"Bado tunakutaka Sikazwe ukiwa hai ili ukajibu maswali ya wanamapinduzi na wapenda maendeleo ya Afrika", nilimwambia huku bado anashangaa jinsi risasi tatu zikitoka pande tofauti zilivyoweza kupiga kiganja chake tu.

Mara tunasikia usiku mzima umejaa kelele za milio ya magari ya polisi.

"Chifu yuko njiani", niliwaambia wenzangu ambao sasa tulikuwa tumemzunguka Sikazwe.

Lo, Bosi ile jiviringisha uliyotoa pale hewani sijaona hata ndani ya sinema", Eddy alinisifu.

"Mimi nilichoka kabisa; sasa naamini yote niliyoelewa. Nilifikiri mengine wanakuongezea", Sherriff alisema.

"Kuwa komandoo siyo mchezo", niliwajibu nikatabasamu.

Milio wa tahadhali ya magari ya polisi ulisogea kabisa.

"Ndio sababu sikumwona Isaack", Eddy alisema.

"Ndio sababu", nilijibu.

Tulisikia milango ya magari inafungwa kwa nguvu. Mara tukamwona Chifu na Mkuu wa Polisi wanaingia.

"Karibu Chifu, kazi imekwisha. Na mtu wenu huyu hapa na mwingine nafikiri tayari una habari naye. Ndani ya malori hapo nje kumejaa silaha, na zingine zimo humu. Mkienda bandari ndogo (dhow wharf) mtakuta meli ndogo iliyotayarishwa kwa ajili ya kusafirisha silaha hizi, sisi hatuna zaidi", nilimweleza kwa niaba ya wenzangu.

"Kazi nzuri vijana, mmeokoa jina la Tanzania, na mmeitoa Afrika katika aibu", Chifu alijibu huku wakitupa mikono ya pongezi.

Mkuu wa polisi alitoa pingu akamfunga Sikazwe huku sura yake ikionyesha ukali.

Mara nikamwona Zabibu anakuja anakimbia akifuatiwa nyuma na Isaack. Niliwakonyeza Sherriff na Eddy, tukatoka pale haraka haraka tukawaacha Chifu na wenzake wanamshughulikia Sikazwe.

"Oh mpenzi Willy", Zabibu alinirukia shingoni.

"Hamna taabu wote tu wazima", nilimjibu.

"Ashukuriwe Mungu", Zabibu alijibu.

"Isaack gari liko wapi?".

"Oh Bosi, linakusubiri wewe".

"Twendeni zetu, acheni wazee hao wafanye shughuli zao sisi yetu tumemaliza", niliwaeleza wenzangu.

Sherriff, Eddy, Isaack, Zabibu na mimi tuliondoka na kwenda kwenye gari letu huku askari polisi tuliowapita wakitushangaa na kutupigia saluti. Tuliingia ndani ya gari letu, huku gari moja la polisi lenye mlilo wa tahadhali limetutangulia.

"Je unajua tunakwenda wapi?", aliuliza.

"Sijui lakini nafikiri imebidi tupewe heshima ya 'VIP' Isaack alijibu.

Mara gari nyingine ya polisi ikatusindikiza kwa nyuma.

"Lo, utafikiri Marais", Sherriff alitania.

"Mara moja kwa miaka si mbaya", nilijibu.

"Mimi mnitelemshe kwa Margaret", Sherriff alisema.

"Ala, mipango imeshafanywa nini?", niliuliza.

"Oh, mwenzangu siku nyingi", Eddy alijibu.

"Sawa baba, kazi na dawa", nilijibu huku nikimbusu Zabibu.

Nilipoangalia saa yangu nikaona ilikuwa yapata saa sita kasoro robo.

Ilikuwa asubuhi ya Jumapili. Jua lilichomoza kutokea baharini huku miali yake ya asubuhi ikichukua rangi ya maji ya bahari na kuipitisha kwenye vioo vya chumba

changu cha kulala. Mwanga huu ulimulika Zabibu usoni ambaye alikuwa bado amelala. Hakika mwanga huu wa asubuhi ulimfanya azidi kupendeza. Asubuhi vile vile kulikuwa na upepo baridi uliotoka baharini na kutufikia sehemu hizi za Upanga. Kwa kifupi ilikuwa asubuhi njema ambayo sitaisahau.

Niliangalia saa yangu nikaona inapata saa moja kasoro dakika tatu. Nilinyanyuka na kufungua radio ili kusikia taarifa ya habari ya saa moja. Kunyanyuka kwangu kulimwamusha Zabibu ambaye alinitolea tabasamu la kukata na shoka. Na mimi nikamrudishia lile la pekee ambalo huwa nalitoa kwa nadra sana.

"Tusikilize taarifa ya habari", nilimwambia.

Baada ya mlio wa tindo sauti ya kike ikasema.

"Sasa ni saa moja kamili". Halafu ikafuatiwa ya kiume.

"Ifuatayo ni taarifa ya habari kutoka Radio Tanzania Dar es Salaam msomaji Godfrey Chalamila. Kwanza habari kwa ufupi. Majasusi wawili walioshiriki katika njama za kuiba silaha za chama cha PLF bandarini wamekamatwa.

Mwili wa msichana mwanamapinduzi Veronika Amadu aliyeuawa katika harakati za kufichua njama za wizi wa silaha utasafirishwa kwenda Freetown, Sierra Leone.

Serikali imetaifisha makampuni yote yaliyokuwa chini ya Kampuni la kibepari la Euro-Afro.

Habari kamili; Wapelelezi shupavu wa Afrika jana usiku waliwakamata majasusi wawili na kuuwa wengine wengi na kuzikomboa silaha na kuzikomboa silaha za chama cha PLF zilizokuwa zimetekwa na majasusi waliokuwa wakiifanyia kazi Afrika Kusini. Majasusi hawa ni Ray Sikazwe, aliyekuwa rais wa chama cha SANP na Tonny Harrison aliyekuwa mwakilishi wa kampuni ya Euro-Afro.

Serikali imetamka kuwa watu hawa watafikishwa mahakamani siku ya Jumatatu kujibu mashitaka ya ujasusi na hujuma. Wakati huo huo kamati ya ukombozi ya OAU imelaani njama hizi za Makaburu na kusema kuwa lazima Makaburu wajue kuwa Afrika iko macho na haiko tayari kucheze. Taarifa hiyo iliendelea kusema kuwa chama cha PLF kitaongeza harakati za mapambano huko Afrika Kusini ambayo ndiyo njia pekee ya kuweza kupata uhuru wa walio wengi. Vile vile taarifa hiyo imesema kutakuwa na kikao cha kamati ndogo ya siasa mjini Dar es Salaam ili kutafuta njia ya kuviunganisha vyama vyote vya ukombozi vya Afrika Kusini, ili moto wa mapambano uweze kuwaka zaidi.

Mwili wa mwanamapinduzi shupavu hayati Veronika Amadu aliyeuawa katika harakati za kupambana na majasusi wa Makaburu ili kukomboa silaha zilizokuwa zimeibiwa bandarini utasafirishwa kwenda MJINI Freetown, Sierra Leone ambako ndiko kwao. Serikali imetoa ndege aina ya Boeng 737 ambayo itachukua na ujumbe wa kijeshi utakaosindikiza maiti hiyo pamoja na wanamapinduzi wengine. Imefahamika toka mjini Freetown kuwa mwanamapinduzi huyu atazikwa kwa heshima zote za kijeshi. Vyama vya wanamapinduzi na wapenda maendeleo duniani kote vimesema vitapeleka wawakilishi wao kwenye mazishi ya shujaa huyo.

Serikali imetaifisha makampuni yote yaliyokuwa chini ya kampuni ya kibepari ya Euro-Afro, kwa kile ilichokiita "Kujihusisha kwa kampuni hiyo na serikali ya Makaburu ili kupiga vita harakati za ukombozi. Hakuna fidia itakayotolewa. Na huo ndio mwisho wa taarifa ya habari".

Nilifunga radio baada ya taarifa ya habari maana ilinikumbusha Veronika.

"Utakwenda kwenye mazishi?", Zabibu aliuliza.

"Ndio".

"Tutakwenda wote?".

"Hamna taabu. Mambo yatatengenezwa.

TAMATI